



# ISABELA

## Katika Mpango Hasi

©jamvi la simulizi 2013
Richard MWAMBE

*"...Wakati mwingine binadamu tunajikuta katika hali ambayo ni wewe tu, kwa kile kidogo utakachokifanya utakuwa umelisaidia kundi kubwa la watu. Kwa nini kupoteza nafasi hiyo?"*
*Kumbuka hakuna upendo mkuu kuliko huu wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake."*

**Richard MWAMBE.**

# 1

## Kasulu-kigoma

Vumbi jekundu lilikuwa likitimka huku na kule katika eneo la kituo kipya cha mabasi cha Kasulu, kila mtu alificha uso wake ili vumbi hilo lisije kumletea madhara yoyote, lakini, watoto walionekana kuifurahia hali hiyo walikimbiakimbia huku na kule kutaka kudaka makaratasi na mifuko ya nailoni iliyokuwa ikipeperushwa na upepo huo, kwao ilikuwa ni mchezo mzuri na wa kufurahisha sana, hawakufikiri hata mara moja kuwa vumbi hilo lingeweza kuwaletea madhara au hata upofu, kwao haikuwa hivyo kwani hawakujali hata kesho ikoje, ni jinsi gani ulivyo mzuri ulimwengu wa watoto.

Katika moja ya migahawa iliyopo stand hapo palikuwa na vijana watatu walioonekana kubishana kitu fulani na kati yao ilionekana hakuna uelewano kabisa, lugha waliyoitumia kuzungumza ilikuwa dhahiri si ya hapa ila ni ya nchi jirani. Vijana hao waliovalia nadhifu walionekana watanashati haswa, suruali zilizowakaa vizuri katika matumbo yao ziliwafanya kuonekana bila shaka yoyote kuwa ni kutoka nchi jirani. Baada ya mabishano hayo yaliyochukua takribani dakika kadhaa walinyanyuka kutoka katika mgahawa huo na kutoka nje kila mtu alionekana kuwa na mawazo tofauti na ya mwingine,

walitoka na kuonekana wakipanda magari tofauti kwa minajiri ya kuelekea Kigoma mjini na kuliacha eneo lile.

Vumbi bado lilikuwa halijatulia katika eneo hilo na watoto wale walikuwa bado wanacheza wakiwa na furaha kabisa huku wengine wakiwa wameshikilia kaptula zao zisiwadondoke. Wengine wkiendelea kucheza kabumbu wakiwa na ndoto za kuwa wachezaji nyota wa dunia siku moja.

Vumbi lile lilitenganisha kwa muda dunia zilizokuwa hapo, kwa wakati huo kila mmoja hakujua nini kinaendelea upande wa pili.

Magari yaliyofika kituoni hapo yaliondoka katika kwa nyakati tofauti mengine yakielekea Kahama, mengine Manyovu, mengine Kigoma mjini basi ilimradi kila kitu kiliendelea.

Vumbi lilitulia na hali ikawa tulivu katika eneo hilo lote, watoto wale sasa iliwabidi wabadilishe aina ya mchezo kwani ule wa kwanza haukuwa na vitendea kazi tena.

Isabel, msichana mfupi, kibonge mwenye macho ya kuvutia, mweusi kidogo mwenye kucheka na kila amuonaye huku akiacha vibonyo vya kuvutia mashavuni mwake akauondoa mtandio wake usoni na kupepesa macho huku na huku na kushuhudia utulivu wa hali ya juu kituoni hapo.

“Kaka samahani hakuna basi lililokuja hapa?” alimrushia swali kijana mmoja aliyekua akiuza vocha na kufanya kazi ya kung’arisha viatu katika eneo hilo.

“Ha! We dada mabasi manne yamekuja na kuondoka ulikuwa wapi? Hukuyaona? Itabidi usubiri bahati nyingine” kijana yule alimjibu Isabel. Isabel alitafakari kidogo imekuwaje hakuyaona mabasi yale, kumbe alipojifunika mtandio ule ili kuzuia vumbi kausingizi katamu kalimpitia ndiyo maana hakujua hata nini kiliendelea kituoni hapo, alitafakari kidogo cha kufanya, kisha akanyanyuka kutoka katika benchi lile akajikung’uta vumbi iliyotua katika suruali yake na kuuendea mgahawa fulani ili apate chochote na kisha aamue afanye nini.

Ndani ya mgahawa aliketi kwenye moja ya viti vya plastiki katika mgahawa huo na kuagiza soda na keki, alipokuwa akiendelea kunywa soda yake alihisi kama amekalia kitu fulani kigumu lakini alipuuzia, baada ya muda alipitisha mkono wake kitini alipokaa na kushika kitu hicho kilichokuwa kikimnyima raha ya kuketi kisha akakitoa na kukitazama ili ajue ni kitu gani.

“Mh” aliguna, alijikuta na bahasha ndogo mkononi ndani ina kitu kigumugumu hivi, baada ya kutazama uku na huku hakuna aliyemuona aliitia bahasha ile katika mkoba wake wa laptop na kumalizia soda yake. Alitoka na kupanda Daladala kuelekea mjini, akiwa ndani ya daladala ile alikuwa na mawazo mengi sana, lengo lake la kwenda mjini ilikuwa ni kuangalia kama

kuna treni ya Dar maana mabasi yamempita kituoni kwa kuendekeza usingizi.

♠ ♠ ♠

**J**osephat Msengiyumva, Jomse kwa jina la kifupisho aliivua miwani yake yake myeusi, maalum kwa kupunguza mwanga wa jua na kuchukua kitambaa kujifuta vumbi kidogo usoni, akiwa amejiegemeza kwenye nguzo ya umeme akiangalia mapito ya wapita njia, mfuko wake wa shati ulitikisika kidogo, akaingiza mkono na kutoa simu,meseji ya maandishi ilifika muda si mrefu

*'Mr Jomse unayo ile memory card?'*

Jomse alishtuka kidogo na kubaki butwaani, akili ilipomrudia aliijibu meseji ile kuwa hana hiyo memory card. Kichwa kilimzunguka na hakujua kama swali aliloulizwa lilikuwa la mzaha au la 'mzaha katika kazi,' alijiwazia, akacheka kidogo kisha akarudisha simu sehemu yake. Mara meseji ikaingia tena,

*'Na jamaa anasema hana, hapa na mi' sina,'*

Jomse alishusha pumzi ndefu na kujiondoa pale aliposimama, akasogea pembeni pasipo na watu na kupiga simu

"Mbona siwaelewi nyie jamaa, kwani wa mwisho kuwa nayo alikuwa nani?" Jomse aliuliza kwa ukali na

baada ya kusubiri sekunde kadhaa akiisikiliza sauti ya upande wa pili aliendelea,

“Nasema hivi! Mrudi palepale kwenye mgahawa mkaangalie, msilete ujinga unafikiri madam akijua tutasema nini? Haya nasubiri jibu!” aliwakaripia wenzake na kukata simu kwa hasira na kuirudisha mfukoni.

Jomse alijishika kichwa kuonesha amechoka ghafla.

Kadi ndogo ya kielektroniki ya kuhifadhia kumbukumbu *(memory card)* iliyokuwa kwenye kijibahasa cheupe ilianza kuwachanganya akili vijana wale, hawakujua wafanye nini, kazi waliyopewa, maelekezo na picha zote zipo ndani ya card hiyo, shughuli pevu.

Mathias Ndirikumana au *‘Mandi’* kama anavyojulikana kikazi alikuwa wa kwanza kufika katika mgahawa ule, alipoingia moja kwa moja alitupa jicho sehemu mbalimbali za kibanda hicho kwa ufundi sana lakini hakuona dalili ya kijibahasha kile

“Dada, tulipoondoka hukuona tumeacha kitu chochote hapa?” alimtupia swali mama lishe yule ambaye alikuwa bize kwa kuosha vyombo.

“Hapana kaka, ni kitu gani?” mama lishe alijibu na kuuliza kwa wakati mmoja

“Aaah, tumesahau bahasha ndogo na hapa tulikuwa nayo, kama umeiona niambie hata pesa nitakupatia, ni ya muhimu sana,” Mandi alimueleza yule mama lishe ambaye alionesha wazi kuwa kitu

hicho hajakiona hata kidogo kwa jinsi alivyoshikwa na mshangao. Mandi alionesha uso wa kuchanganyikiwa, kila wakati alikuwa akijifuta jasho usoni, mara ashike kiuno, mara atikise kichwa.

“Vipi umeipata?” sauti ilitokea nyuma yake, alipogeuka alikutana macho kwa macho na Tonton ambaye alifika mahali hapo muda huo.

“Hapana Ton, sijaiona” alimjibu

“Ah! Huyu dada anasemaje?” Ton aliuliza

“Anasema hajaiona kabisa,” Mandi alimjibu Tonton, Tonton alishikwa na hasira nakuanza kumfuata yule dada lakini alizuiliwa na mkono wenye nguvu wa Mandi

“Tulia Tonton, mbona una papara,” Mandi alimtuliza Ton, na Ton alitulia na kuketi kwenye moja ya viti vilivyopo mgahawani hapo.

“Dada! Unakumbuka mi nilikaa hapo kwenye kiti cha pepsi, nilipotoka nani alikaa?” Ton aliuliza, kwa kuwa yeye ndiye aliyekuwa na bahasha hiyo mfukoni.

“Hapo, alikaa mdada mmoja hivi, naye ameshaondoka na daladala kwenda mjini, lakini sijui kama yeye kaichukua” mama lishe alimjibu Ton, Mandi na Ton walitazamana kisha wote wakageuka kwa dada yule kabla hawajaongea lolote sauti ya mtoto iliwakatiza

“Mama! Kwani hawa wanataka nini?” mtoto yule alimuuliza mama yake,

“Wanatafuta bahasha yao wameipoteza, maswali mengi kama unaelewa kinachoendelea, kwenda

kacheze huko si ushashiba," dada yule alimjibu mtoto huku akimsukuma akacheze

"Ah! Mi najua, alishika yule dada aliyekaa hapa, hapa kwenye hiki kiti," mtoto alieleza na kisha kukimbia kuendelea kucheza mpira na wenzake.

"Dada huyo msichana alikaa hapa yukoje?" Ton alidakiza swali kwa dada yule.

"Mfupi, kibonge hivi, alikuwa amevaa suruali ya jeans nyeusi na tshirt nyekundu, ila sikumbuki ilikuwa imeandikwa nini ana begi jeusi la mgongoni," mama lishe aliwajibu vijana wale. Bila kuchelewa Mandi na Ton waliondoka kituoni hapo na kukodi tax.

"Kigoma mjini tafadhali" Mandi alimueleza dereva tax huku akifunga mlango na kujiweka vizuri katika kiti cha nyuma. Ton alichukua simu yake na kutuma sms kwa Jomse kumueleza juu ya tukio hilo

*'Sasa tufanyeje?'*

Jomse alirudisha sms ile kwa Ton,

*"Nafikiri tujaribu kumfuatilia ikiwezekana kumpata tuchukue hiyo memory card."*

Wazo lilikubaliwa na wote watatu na moja kwa moja Jomse ambaye wakati huo alikuwa mjini moja kwa moja alielekea kituo cha mabasi cha Mwanga ili kujaribu kama anaweza kumtambua msichana yule na jinsi gani ya kupata memory card ile.

Vurugu za wapiga debe na wabeba mizigo katika kituo hicho cha mabasi zilishamiri mchana ule, wanaoshuka na wanaopanda mabasi walikuwa ni wengi. Jomse alisimama karibu kabisa na kibanda cha simu, kutokana na urefu aliokuwa nao haikuwa vigumu kuwaona wote waliokuwa katika pilikapilika kituoni hapo. 'Msichana mfupi, kavaa fulana nyekundu na suruali ya jeans nyeusi' Jomse alijesemea moyoni maneno hayo huku akiangalia kila daladala inayoshusha abiria katika eneo hilo.

Mandi na Ton nao waliingia katika eneo hilo na kumshukuru dreva tax, Ton alitoa noti nyekundu moja na kumpatia kijana yule kisha wakajichanganya katika kundi la watu na kuanza msako wao.

Jomse alikuwa makini akiwa na gazeti lake mkononi alijifanya anafungua kurasa hii na ile lakini hakuwa akisoma chochote ndani ya gazeti hilo, aliang'aza macho huku na kule kuangalia kama atamuona msichana yule, huku akili yake ikizidi kuchanganyikiwa juu ya upotevu huo wa ile memory card, wasiwasi wake ulikuwa ni jinsi gani wataonekana wazembe kwa sababu hata kazi waliyopewa bado hawajaanza kuifanya na memory card hiyo wameshaipoteza, Jomse alijua wazi kuwa madam akisikia jambo hilo watapata shida sana kwani wataonekena wazembe kupita maelezo.

Mandi na Ton waligawana kila mtu upande wake ili wote waweze kuona kama watampata msichana huyo, walikuwa na wasiwasi na daladala waliyoipita

njiani, walijua hakika atakuwa katika hiyo, na walipanga watafanya kila hila wampate ili wapate watakacho.

Toyota Hiace ya buluu iliingia kituoni hapo na kutafuta maegesho ili ishushe abiria wake, watu walikuwa wengi ndani ya gari hiyo na walianza kushuka mmoja mmoja,

*‘muwe makini katika kufanya hili,’*

Sms iliingia katika simu ya Mandi na Tom kwa wakati mmoja.

*‘Msitumie nguvu ila akili ndiyo inahitajika’*

Sms nyingine iliingia kwa wote wawili.

Isabel akiwa ndani ya daladala alijisikia baridi kidogo akafungua begi lake na kutoa sweta aina ya ‘kaba shingo’ na kulivaa kabla hajashuka katika gari ile, alipohakikisha limemkaa vizuri, taratibu alishuka garini nakuangalia huku na kule kisha kujichanganya na watu wengine kituoni hapo.

Msichana anayekadiriwa umri wa miaka kumi na minane alishuka katika daladala upande wa pili, Jomse alimgundua haraka msichana yule aliyevalia sweta jekundu na sketi nyeusi, Jomse alimkazia macho lakini alijiuliza kwa nini maelekezo aliyopewa hayakulingana na mtu mwenyewe alivyo, alimtupia jicho mara

nyingine na kutoa simu yake mfukoni akaandika kitu Fulani

*'Kwenye mitumba'*

Meseji ziliingia kwa Mandi na Ton, mara moja walimuona msichana yule lakini wote walishangaa kuona hajavaa suruali kama walivyoelekezwa. Ton alisogea taratibu eneo la muuza mitumba ambapo binti yule alionekana akichagua vibrauzi vya hapa na pale, alipomuangalia kwa makini aliona kuwa hilo ni windo tofauti na wanalolitaka, alijaribu kuangalia vizuri huku na huku kama atamuona mwingine lakini eneo lote alikuwa ni binti yule tu aliyevaa vile.

*'Ni huyu kweli?'*

Ton aliwatumia meseji Jomse na Mandi, hapo nao wakapata shaka wasije kumbana mtu tofauti, waliumiza vichwa wafanyeje kwa hilo. Lakini katika eneo hilo hakukuwa na msichana yoyote aliyevaa vile walivyoelekezwa.

Baada ya kuchagua vibrauzi viwili yule msichana alinunua mfuko wa rambo na kuweka kisha akachukua begi la mdogo wake na kuingiza humo na kuliweka mgongoni safari ikaendelea. Mandi alimfuata nyuma nyuma msichana yule huku akitafuta mbinu ya kulikwapua begi lile, mpango ulipangwa kiufundi sana. Mara ghafla gari aina ya Toyota mark II ilifunga breki

karibu kabisa na msichana yule, Jomse alichomoza na kumvutia ndani kwa haraka kabla hatahamaki gari ile iliondoka kwa kasi. Mandi aliangalia gari ile ilivyotokomea, watu walikusanyana eneo lile kuangalia kilichotokea akina mama wakipiga kelele za msaada

“Dada!!, dada!!” mtoto mmoja wa kiume alikuwa akilia kwa uchungu pembeni mwa barabara.

Isabel akiwa na begi lake mgongoni aliona tukio lote lilivyotokea, alipigwa na bumbuwazi alibaki kajishika mdomo, naye alijichanganya na watu wengine katika eneo hilo. Mandi alimtazama Isabel kwa makini kana kwamba kuna sehemu ambayo amekwishawahi kumuona, Isabel alipogeuka alikutana macho kwa macho na Mandi lakini hakumtilia maanani akijua tu ni moja ya wapita njia, Mandi alimwita Isabel

“We dada njoo umsaidie mtoto huyu,” Isabel alikwenda na kumchukua mtoto yule aliyekuwa akilia sana, Isabel alimtazama mtoto yule alivyojawa na machozi, hakuwa na kitambaa alichokifanya ni kulivuta sweta lake kwa juu na kumfuta machozi mtoto yule, Mandi akiwa bado hajaondoka eneo lile alimuona Isabel alipofanya jambo hilo na mara moja aliiona fulana ile nyekundu iliyochomoza kwa chini baada ya kulivuta sweta lile juu, na lipomwangalia vizuri alimuona kweli kavaa jeans nyeusi, Mandi alipagawa alitoa simu yake mfukoni na kutuma meseji

*“Wrong number, rudi haraka namba sahihi umeiacha,”*

Alirudisha simu mfukoni na kuanza kumfuatilia Isabel. Isabel alimkabidhisha mtoto yule kwa askari polisi mmoja wa kike ambaye alifika eneo hilo na yeye kuendeea na safari yake.

Mandi alikuwa bado akimwangalia Isabel wapi anakoelekea, Isabel aliangalia saa yake ya mkononi na kuona muda unamuacha alisimamisha bodaboda na kupanda kisha akampa maelekezo fulani dereva. Mandi naye akachukua bodaboda iliyofuata na kuifukuzia ile nyingine

“Hakikisha haikupotei” Mandi alimsisitiza muendesha bodaboda. Isabel akiwa hajui kama anafuatiliwa alikuwa anawaza tu kama ataiwahi treni ambayo ilikuwa iondoke jioni hiyo kuelekea Tabora mpaka Dar huku akiwa ameshasahau juu ya ile bahasha.

♠ ♠ ♠

**J**omse na Ton walimpekua binti yule kila kona ya mwili wake na begi lake kisha wakambana maswali mengi, lakini msichana yule alibaki kulia tu maana hakuna alichokielewa walichokuwa wakimuuliza

“Ina maana tumekosea?” Ton alimtupia swali Jomse ambaye alibaki akimkodolea macho Ton,

“Labda tumeshindwa kujua suruali ni ipi na sketi ni ipi!” Hapo wote walijiona hawana akili kwa hilo

“Simama!” Jomse alimuamuru dreva wa gari ile

“Haya binti shuka, samahani” Jomse alimpa noti ya shilingi mia tano ili apande daladala kurudi mjini. Simu ya Jomse illita na muda uo huo ya Ton nayo iliita

*“What!?”* ilisikika sauti ya Ton na kudakiwa na Jomse kwa mshangao pia

“Tufanyeje sasa?” Jomse aliuliza.

“Tuache hapa” Ton alimwambia dreva, wakampa hela yake na akaondoka, hawakukaa hata dakika mbili defender ya polisi ilipita na kusimama mbele yao

“Habari!” polisi mmoja aliuliza,

“Salama sana, za kazi” Ton alijibu

“Mmeona gari moja salon nyeupe imepita hapa kuelekea huku ?” waliuliza

“Hapana afande hatujaiona sisi ndiyo tumefika sasa hapa barabarani tunasubiri daladala” Ton alijibu, mara tax ikapita eneo hilo na Jomse akasimamisha wote wawili wakajitoma ndani na kurudi mjini.

Jomse na Ton walifika eneo lile walilomtekea yule binti na kukuta hali imetulia kabisa kana kwamba hakuna kilichotokea muda mfupi uliyopita. Walishuka katika tax ile na kumlipa dereva kisha kilammoja wao akachukua njia yake maana hiyo ndiyo mbinu kubwa waliyokuwa wakiitumia.

*‘Stesheni ya reli’*

Meseji ya simu ilisomeka kwa Jomse na Ton mara moja, kila mtu alichukua usafiri wake kuelekea

stesheni. Mandi alihakikisha hampotezi Isabel katika macho yake, alipomuona akishuka katika bodaboda ile na yeye alishuka kisha kutembea kwa miguu kuelekea katika jengo la stesheni ambako Isabel alielekea huko pia. Jomse na Ton walifika eneo hilo kwa tofauti ya dakika kama tano kati yao na kujichanganya na wasafiri waliokuwa wakiingia ndani ya jengo hilo ili kupanda treni kuelekea pande tofauti za nchi.

Isabel akiwa hajui lolote alipanga foleni kama ilivyo ada kwa wasafiri katika eneo hilo, alishtuka kumuona Mandi tena katika eneo hilo na sasa akiwa anamtazama sana

"Ooh samahani mdogo wangu, kumbe wote tunasafiri!" Mandi alimsemesha Isabel ambaye kwa wakati huo akili yake ilikuwa mbali sana akiwaza hili na kuwazua lile, Isabel alitoa tabasamu fupi na kuendelea na hamsini zake.

Watu walikuwa ni wengi katika eneo hilo, kelele na shughuli nyingi ziliendelea hapo, polisi na vibaka waliendelea kuwindana pasi kukamatana. Lango la kuingia ndani lilifunguliwa na watu wakaanza kuingia kuelekea katika mabehewa tayari kwa safari

"Ee dada, nilikuuliza kumbe tupo wote safarini?" Isabel alimwangalia Mandi hakumjibu chochote aliendelea na safari yake kuelekea ilikosimama treni ile. Alipoona Mandi anazidi kumsumbua alijichanganya upande wa pili wa abiria wengine na

kutokomea, alimuacha Mandi akimsindikiza kwa macho tu.

Akiwa hana hili wala lile, Isabel alijikuta akichomolewa begi mikononi mwake na kijana aliyepita kwa kasi isiyoelezeka.

“Mwizi! Mwizi! mwizi kamata huyo,” kelele za watu zilisikika wakati Isabel akilia kwa uchungu kwa kuibiwa begi lake ambalo ndani yake kulikuwa na laptop na vitu vyake vichache, alishindwa afanyeje alibakiwa na begi lake la mgongoni tu, Isabel alilia sana kwa kupoteza begi lake. Wananchi wenye hasira walimkimbiza kibaka yule ambaye alikimbia na kuruka kwenye wigo wa stesheni hapo na kuonekana akipeleka begi lile kwenye gari moja nyeusi iliyopaki eneo la nje la stesheni hiyo, lakini kabla hajafika alipigwa dafrao na mmoja wa wapita njia

“We kijana vipi mbona huangalii?”

“Samahani bwana mkubwa watu tupo kazini, majanga haya!” aliongea kwa sauti ya kitejateja, kutahamaki alijikuta yuko chini akifuatiwa na kipigo kikali cha wananchi wenye hasira,

“Ua! Ua kabisa huyo, wamezidi hao!” sauti za watu zilipishana, mwenye jiwe, rungu, fimbo ilimradi tu kumuadhibu kiumbe yule. Jomse na Ton waliangalia tukio zima lilivyoendelea hawakufanya chochote, polisi ndiyo walioweza kumuokoa kijana huyu aliyekuwa hatamaniki kwa damu iliyochanganyika na vumbi, yule polisi aliokota begi lile na kumpiga ‘Tanganyika jeki’ yule kibaka mpaka kituo cha polisi kilichopo stesheni

hapo. Mandi sasa akifuatana na Isabel walifika katika kituo hicho kidogo na Mandi alikuwa ndiyo msemaji mkuu kuelezea polisi kila kilichotokea na kuomba ikiwezekana begi hilo akabidhiwe mwenyewe, baada ya mazungumzo machache polisi walikabidhi begi lile lakini kabla Isabel hajalichukua tayari lilikuwa mikononi mwa Mandi.

“Bingo!” Ton alisikika huku akimpiga ngumi mgongoni Jomse ambaye alibaki kutabasamu tu. Ton na Jomse walikuwa wakifuatilia hatua kwa hatua kila jambo liliokuwa likitokea, walitoka pale waliposimama na kuelekea lango kuu la stesheni ili kuona jinsi watakavyopata begi lile toka kwa Mandi. Isabel alimuomba Mandi lile begi “Usijali twende tu, watakupora tena vibaka wa hapa mi nawajua sana ntakupa ndani ya treni” Mandi alimjibu Isabel huku akiongoza katika treni ambayo tayari lilisahawashwa injini yake na kupiga honi tayari kwa safari, Mandi alimnyayua Isabel na kumpandisha kwenye ngazi kisha yeye mwenyewe kufuatia huku akining’iniza begi lile kwa nje, Jomse na Ton waliiona trick ile na kuielewa vema.

“Oya begi hilo,” bwana mmoja alimwambia Mandi na kulivutia ndani kabla Ton na Jomse hawajalifikia.
*‘Huyu mzee choko kweli,’* Mandi alijisemea moyoni.

“Kaka mi naenda daraja la tatu, naomba mkoba wangu” Isabel alimwambia Mandi kwa sauti yake ya kivivu.

“Usijali hata mi nipo ukohuko daraja la tatu” Mandi alimjibu Isabel na wote wakafuatana kuelekea daraja la tatu. Katika korido ya treni walipishana na watu mbalimbali waliokuwa wakitafuta vyumba vyao ili wapumzike. Isabel kila wakati aligeuka nyuma kumwangalia Mandi, aliridhika kumuona Mandi naye akiwa katika harakati za kupenyapenya kufika huko *‘kajamba nani’* . Baada ya kuvuka mabehewa kama manne hivi Isabel aligeuka kumwangalia Mandi hakumuona, Isabel alichanganyikiwa kwa mara nyingine alianza kurudi alikotoka akihema watu walikuwa wakimwangalia na kumuona kana kwamba kapungukiwa, mara alikutana na Mandi kama behewa la tatu hivi

“Nakuja dada usiwe na wasiwasi nilikuwa naongea na rafiki zangu hapa tumepoteana miaka mingi” Mandi alimueleza Isabel kisha wakaendelea kwenda huko daraja la tatu “Kaka mi naona unipe tu begi langu tutapoteana humu” Isabel alimueleza Mandi. Mandi alijifanya hakusikia, Isabel aliwatazama wale vijana wawili waliokuwa wakiongea na Mandi na wao pia walimtazama sana Isabel, woga ulimuingia na hofu ikamtawala sana hapo Isabel akaona usalama wake ni mdogo.

Watu walikuwa wamejaa sana hata pa kuweka miguu hapakupatikana. Isabel na Mandi walijibanza kwenye kanafasi kadogo sana. Kwa mwendo wa taratibu treni hiyo ilianza kuuacha mji wa Kigoma, si Mandi wala Isabel aliyekuwa akiongea na mwenzake.

Mandi akajikohoza na kuvunja ukimya uliyotawala kati yao.

“Binti” mandi limwita Isabel, akaendelea kumwambia, “Upo confortable hapo?”

“Nitafanyaje sasa hata kama sipo confortable?” Isabel alimjibu Mandi huku akilini mwake akijiuliza kwa nini Mandi ameling’ang’ania begi lake.

“Huku sio kuzuri binti, twende tutafute daraja la pili huwa kuna vyumba vinakuwa wazi” Mandi alimuomba Isabel

“Naogopa! We nenda tu utanikuta hapahapa” Isabel alijibu huku akichukua begi lake kwa Mandi lakini Mandi hakumpa, aliendelea kumlazimisha waende daraja la pili.

“Ukunihakikishia usalama wangu nitakwenda” Isabel alimwambia Mandi na Mandi akufanya ajizi alimhakikishia usalama, Isabel alikubali na wakaondoka na pamoja mpaka mabehewa ya mbele, Mandi hakukosea, chumba kimoja kilikuwa tupu ndani yake kuna nafasi ya watu sita.

“Tuingie hapa tupumzike” Mandi alitoa ombi kwa Isabel, ijapokuwa Isabel alikuwa na moyo mzito kwa hilo lakini hakuwa na jinsi alimuamini sana Mandi na kumuona kama Malaika mlinzi kumbe hakujua hila yake.

“Sawa, hamna shida” Isabel aliingia chumbani na Mandi wakaketi kila mmoja kwenye kitanda chake kwa mtindo wa kutazamana, Mandi alijilaza kwenye kitanda wakati Isabel alikua kimya kabisa upande wa

pili katika kitanda kingine. Mara kwa mara Mamdi alikuwa anachati kwenye simu na mtu au watu wa upande wa pili.

*“Tupo second sleeping class namba 32”*

Ton alipata meseji kutoka kwa Mandi, akatabasamu na kumpa simu Jomse kisha wote wawili wakaanza kuelekea huko

“Sasa tutafanyaje kuchukua lile begi?” Ton alimuuliza Jomse

“Unakuwa kama mtoto katika kazi! Makofi mawili tu si anatuachia hilo begi” Jomse alimjibu Ton huku wakiendelea na safari yao.

Treni ya express kama wanavyopenda kuiita ilikuwa tayari ipo katika mwendo wa kasi, ikipiga honi nyingi kuomba watu na magari waachie njia kwa kuwa yenyewe haikuwa na vituo vingi kama ile ya *oldinary*.

Kila mtu ndani ya treni hiyo alikuwa akiendelea na shughuli zake, wengine walikuwa wamelala, wengine walikuwa ndani ya behewa lenye la mgahawa wakila hiki na kile, wengine wakicheza karata ilimradi tu safari iwe fupi. Kati ya mamia ya watu waliobabwa katia treni hiyo ni mtu mmoja tu aliyekuwa hajui mpaka hapo kama atafika salama au la, akiwa ameketi katika kitanda na usingizi ukianza kumnyemelea kama kawaida yake akagutushwa na mlango ukigongwa akainua macho kuutazama kitasa kilionekana kukunjwa kuelekea chini, mlango ukaachia bila ubishi

Jomse na Ton wakajitoma ndani kisha wakafunga mlango nyuma yao. Isabel aliona sasa amekwisha, aliogopa kuona wanaume wote wale wanakuja pale ndani hali yeye ni msichana peke yake, aliwakumbuka vijana wale 'rafiki wa Mandi' alijisemea moyoni. Mandi aliwakaribisha na baada yamazungumzo mafupi aliwaomba kama wangeweza kutoka ili wakamilishe kazi yao, wote waliafiki wakanyanyuka, Mandi akanyanyuka na begi akamwita Isabel waende wote.

"Hapana mi siendi nyie nendeni, ila kaka Mandi niachie begi langu utanikuta apa hapa" ulikuwa mtihani mgumu kwa vijana hawa Jomse akambania jicho Mandi kuwa amuachie lile begi, Mandi akampatia, Isabel alishukuru sana kulipata begi lake kichwani akiwaza kuwa wakiondoka tu na yeye abadilishe behewa aliona kuwa atakuwa salama zaidi akiwa daraja la tatu kwa kuwa linakuwa na watu wengi. Alipohakikisha kuwa mlango umefungwa alitulia kama dakika kumi akiomba Mungu kisha akainuka akiwa na begi lake moja mgongoni na lingine mkononi alijiingiza mkono katika mfuko wa jeans aliyovaa na kuikuta ile bahasha ipo hakujua ndani ina nini alitamani kufungua lakini aliona si mahali pake kwanza atafute sehemu ya usalama, aliusogelea mlango na kushika kitasa akakikunja alipouvuta mlango alikuta mlango haufunguki, umefungwa na funguo kwa nje. Isabeli alidondoka kwa kizunguzungu akiwa hajui afanye nini alijua kuwa vijana wale lao moja labda wanataka kumbaka, alilia kwa uchungu,

hakuona la kufanya zaidi ya kujirusha dirishani *'bora nife kuliko aibu ya kubakwa'* alichungulia nje kwa kutumia dirisha lile aliona jinsi kasi ya treni ile ilivo aliogopa kwani ni vumbi na upepo mkali vilisababishwa na kasi ya treni ile, cheche za moto zilionekana katika giza lile kutokana na msuguano wa vyuma vya reli na vyuma vya magurudumu ya gari moshi hilo. Isabel alifumba macho tayari kujirusha nje kupitia dirisha hilo, mara mlango ukagongwa na kujaribu kufunguliwa lakini haukufunguka Isabel aligeuka huku akihema na alishikwa na woga mkuu ila alijifariji kwa kuwa alijua kama wangekuwa wao wenyewe si wanajua kuwa wameufunga wasingeutikisa, mara akasikia chokochoko za funguo na mlango ukafunguka. Isabel akakutana uso kwa uso na afisa polisi

"Asante Mungu umesikia sala zangu," Isabel alibwabwaja bila kujielewa, "Wamenifungia, wanataka kunibaka," aliendelea kubwabwaja, polisi yule kijana alimuangalia Isabel kwa jicho la uchu akajikuta anamtamani hivyo akajikuta hana budi kumsikiliza.

"Nani anayetaka kukubaka? Yuko wapi?" polisi yule alimsaili Isabel. Isabel alimueleza polisi yule hali yote ilivyo mpaka dakika hiyo na kumuelekeza jinsi walivyo na muonekano wao.

"Ok! Unaitwa nani mrembo?"

"Naitwa Isabel."

“Mi naitwa konstebo Kirama au niite ‘K’, Usihofu, upo kwenye mikono salama kabisa, hakuna wa kukudhuru” polisi yule alimpa matumaini Isabel.

“Chumba namba 32 afande ova…” radio call iliita katika behewa la mwisho kabisa la treni hiyo.

“Nimekusoma afande, ova…”

“Msaada wa haraka tafadhali,ova…”

“*Read and clear, work in progress*, ova”

Mazungumzo baina ya polisi hao kwa kutumia redio zao maalum yalimfariji sana Isabel, hapo aliona umuhimu wa kuwa na vituo vya polisi kila panapohitajika.

# 2

"Sasa kale kasichana kasitusumbue ni kukasachi na kuchukua mzigo, kwanini tupoteze muda, watu tuna mambo mengi!" Jomse aliwaaeleza wenzake

"Mandi umekaa nae muda wote umeshindwa kumlaghai? Au ulitaka ubadili mawazo, sema," Ton alimwambia Mandi kwa utani na Mamdi akaishia kucheka.

"Ok vijana, tupo kwenye treni cha kufanya ni kuchukua mzigo na kuteremka lakini hii ngoma haisimami mpaka Tabora" Jomse aliendelea kuzungumza

"Tufanye hivi, tujigawe mmoja aende kwenye injini, mwingine aangalie usalama na mwingine akambane yule mrembo akijifanya jeuri ni kichapo hakuna huruma tena" Ton aliongeza.

"Mandi wewe uende kwenye engine hakikisha unamlazimisha operator apunguze mwendo ili tukipata mzigo wetu tuondoke mara moja," Jomse alimteua Mandi kwa kazi hiyo maana alijua keshamzoea Isabel kwa hiyo hatoweza kufanya kazi ipasavyo.

Mpango ulikamilika kila mtu akachukua idara yake, haikuwa kazi kwa Mandi kufika kwa operator.

Mzee Kasimu, mzee wa makamo opareta wa treni za reli ya kati kwa miaka takribani ishirini na saba, hakika alikuwa mzoefu wa kazi yake, alistuka kumuona kijana huyu mwenye ngozi maji ya kunde, mrefu kidogo mwenye umbo la kiume hasa.

"Kijana vipi umepotea njia?" alimuuliza

"Hapana baba, mimi ni mgeni wako, Mashine yako ipo kasi sana tunaomba upunguze mwendo" Mandi alimuamuru opereta.

"Unasema?! We unanifundisha kazi mimi? Mbona nyie vijana wa siku hizi hamna adabu nani kwanza kakuruhusu kuingia huku?" Mzee Kasimu alifoka

"Shhhh, mzee usilete maneno mengi, mi sio mzaramo," Mandi alimtuliza huku akimuonesha mtutu wa bastola.

"Haya punguza mwendo" Mandi aliamuru. Mzee Kasimu tangu azaliwe hajawahi kuona bastola, kijasho chembamba kilimtiririka, alitetemeka kwa hofu. Alianza kugusagusa vitufe mbalimbali kwenye *dash board* yake na engine ikaanza kumtii.

"Unajua kijana, sisi tunakwenda kwa muda, sasa mimi sielewi kwa nini unataka nipunguze mwendo, ni hatari tunaweza kusababisha ajali," Mzee Kasimu alilalama

"Nimesema punguza mwendo, sicheki na wewe hapa," Mandi alionesha ukali kidogo. Hali ilikuwa

ngumu kwa mzee Kasimu kijasho kilimtoka hata alihisi suruali inalowana bila yeye kuwa na taarifa.

♠ ♠ ♠

**T**on aliendelea kusavey karibu kabisa na behewa alimokuwa Isabel ili aone kama kuna dalili yoyote ya askari au hatari yoyote kabla hajamruhusu Jomse kuingia katika chumba hicho. Kwa mbali aliwaona askari wawili wenye silaha wakielekea upande ule kutokea behewa la nyuma. Ton alitulia kama mtu anayefikiri jambo Fulani, korido yote kwa muda huo ilikuwa na watu wachache sana, wale polisi walifika kwenye ule mlango na kuutikisa kidogo ulionekana umefungwa wakapita na kuendelea mbele. Ton alituma meseji kwa Jomse kumpa taarifa, Jomse akafika na kuingia mara moja akamkuta Isabel peke yake amejilaza kitandani, akaingia kwa upole kana kwamba anataka kuiba kitu Fulani, Isabel akashtuka.

“Usishtuke mrembo! Ni mimi, nahitaji unipe ule mzigo wangu, bila ubishi kwani sintoona kazi kukuua endapo utaleta ujeuri,” Jomse alimtamkia maneno hayo Isabel ambaye kwa wakati huo alikuwa amejikunyata kitandani.

“Mzigo gani? Mi nna mzigo wenu nyie?” Isabel alijibu huku akilia. Jomse alimtazama Isabel kwa jicho la gadhabu.

“Sikia wewe kasichana, unazidi kunitia hasira wakati unajua nini ninachokihitaji kutoka kwako, sasa nakuua kama unajitia ubishi.” Kabla Jomse hajafanya

lolote alijikuta akipigwa double kick kwa nyuma iliyotaka kumtolea dirishani, Jomse aligeuka na kukutana na ngumi mbili za uso, damu zilimtoka mdomoni, Jomse alianguka chini akiwa hoi kutokana na kipigo kile cha harakaharaka pasi kutegemea, Jomse alijikuta ujanja wote mfukoni kwani kwa dhoruba aliyopewa na konstebo Kirama, mtoto wa Arusha aliyepitisha utoto wake huko Mererani katika machimbo ya tanzanite, alibaki hoi sakafuni. Akiwa pale chini Jomse alijigeuza kujibu mashambulizi lakini akajikuta akikanyagwa kwa nguvu shingoni na kurudi tena chini.

“Tulia! Hivyo hivyo. Mnataka nini kwa huyu msichana” Kirama alimuuliza Jomse ambae hakuonekana kutoa ushirikiano, Kirama alimuongezea kipigo akiwa pale chini, Jomse alibaki kutambaa kila alipotaka kunyanyuka alipigwa mateke ya mbavu mpaka akapoteza nguvu kabisa.

Isabel alitumia mwanya huo kutoka ndani ya chumba kile alipofika mlangoni hamad! alikumbana na Ton, Ton alijaribu kumshika lakini Isabel alimuwahi kwa kumtandika na begi lenye laptop usoni, Ton alipoteza umakini kwa sekunde kadhaa alipozinduka hakukuwa na Isabel wala kivuli chake.

Bila kuangalia anakokimbilia Isabel alijikuta akitokea katika behewa la mizigo, alisimama kwa utulivu na kuchanganya akili, afanye nini, wazo likamjia, akachagua sehemu na kujibanza kutokana na ufupi wake alitosha kujipachika katikati ya mabegi na

masanduku, mpaka hapo Isabel hakujua vijana wale wanataka nini kwake, aliingiza mkono mfukoni na kuichukua ile bahasha mfukoni mwake na kuichana kitu kidogo cheusi kikadondoka, kutokana na giza katika behewa lile alitumia simu yake ya kichina kumulika, haikuchukua muda akakipata, alikigeuzageuza kwa makini *'memory card'*, Isabel alitikisa kichwa kuashiria kuwa sasa ameelewa nini wanachomtakia, lakini alijiuliza 'kwa nini watumie nguvu zote kwa kidude hiki si wangenieleza tu ningewapa' Isabel aliamua kurudi katika lile behewa ili akawakabidhi hiyo card hakuona haja ya kukimbizana kwa sababu hiyo, mwanzoni alijua labda wanataka laptop yake au kumbaka, alisonya na kuendelea kuelekea behewani, ikiwa amebakisa hatua chache kuufikia mlango wa chumbakile alisikia sauti ya kitu kama bunduki kutoka katika chumba kile, Isabel alisimama na kurudi kwa kasi kule alikotoka.

Mlio ule uliwaamsha watu wa vyumba vingine na wakatoka kuona nini kilichotokea

"Huku,"

"Hapana ni huku," walisikika wakibishana wenyewe kwa wenyewe, korido yote ilijaa watu wa behewa lile wakikimbia huku na huku hata wengine wakinusurika kutumbukia kwenye maungio yaliyopo kati ya behewa moja na lingine, kwa mtindo uo huo Ton na Jomse walitoka ndani ya chumba kile na kujichanganya na watu lakini wao bado walikuwa wakimtafuta Isabel kwa kuwa kiu yao bado ilikuwa

haijaisha mpaka watakapompata. Hasira juu ya msichana huyu iliwatawala kila kona ya miili yao, na katika kujichanganya huko kila mmoja aliendа upande wake kuendelea kumtafuta Isabel.

♠ ♠ ♠

Polisi walifika chumba namba 32 na kusukuma mlango taratibu huku mitutu ya SMG zao ikitangulia kabla yao ndani ya chumba kile, mlango ulikubali kufunguka taratibu na polisi wale walijitoma ndani kwa tahadhari kubwa.

Mwili wa afande Kirama ulibaki umelala kati ya vitanda vile ukiwa ndani sare yake nadhifu ya kipolisi ukivuja damu nyingi katika ubavu wa kushoto, risasi iliharibu vibaya ubavu wa afande Kirama. Afande Benso alipiga goti moja chini huku akiweka vizuri bunduki yake mgongoni, machozi yakimlengalenga aliusogelea mwili wa afande Kirama na kuugusa shingoni na moyoni kuona kama kuna dalili ya uhai, alipougusa aligundua bado mwili huo una joto
“machela haraka!” aliwaeleza wenzake na mara moja wakawasiliana na wengine. Dakika chache machela ilikuwa tayari imefika wakauweka mwili wa afande Kirama na kurudi nao behewa la mwisho kwa huduma ya kwanza kabla hawajaufikisa hospitalini. Watu walibaki wakiangalia yote yaliyojiri walipohojiwa na polisi juu ya tukio lile nini wanachojua walijibu tu “hatujui kitu, tumesikia mlio huo tukaanza kukimbia” lakini mioyo yao ilisema *‘sitaki ushahidi’* . wananchi

katika treni ile walishindwa kutoa ushirikiano kwa jeshi la polisi kama kawaida ya watanzania wengi.

“Jamani maelezo haya tunayohitaji yatasaidia kumpata muhalifu, sasa nyie hamtaki kutuambia kitu sasa mlitoka vyumbani kufanya nini!” afande Benso aling’aka kwa hasira na kuendelea

“Maisha ya mtanzania yashapotea, tunahitaji kumpata muuaji na yupo umuhumu miongoni mwenu” Watu waliokuwepo eneo lile wakatawanyika mmojammoja na kurudi vyumbani mwao, afande Benso kwa kushirikiana na polisi wengine wakafunga ule mlamgo wa namba 32 kwa utepe maalum wa njano ulioashiria hilo ni eneo la hatari liko chini ya uchunguzi wa kipolisi.

Treni iliendelea na safari yake kwa mwendo wa kasi, watu wengine katika mabehewa mengine hawakujua hata ni kitu gani kimetokea, waliendelea na mazungumzo na kuangalia luninga zililiwapa burudani murua ya muziki wa DRC Congo.

“Kituo cha polisi kati Tabora, tukusaidie nini” simu ilipokelewa upande wa pili huku Tabora

“Koplo Kibona naripoti kutoka ndani ya treni ya reli ya kati inayotoka Kigoma kwenda Dar es salaam” Koplo Kibona alikuwa hewani akitoa taarifa ya tukio

“Tumekusoma afande… endelea” sauti ilijibu

“Afande Kirama amepigwa risasi na watu wasiojulikana, na watu hao tunahisi bado wapo humu ndani ya treni, hali ya afande ni mbaya tunaomba msaada wa haraka” Koplo Kibona alimaliza

"Copy" sauti ilijibu na simu ikakatika.

Koplo Kibona na afande Benso walijaribu kutafuta mawasiliano na opereta wa treni hiyo lakini simu ilikuwa inaita tu na haipokelewi. Wakaamua kwenda huko kuona kuna nini kimetokea.

♠ ♠ ♠

**M**sako mkali ulianza ndani ya treni hiyo behewa moja baada ya jingine ili kuweza kuwakamata waliofanya unyama ule, wale wote waliofanania na unyama huo walichukuliwa kwenye behewa moja na kupewa vitisho ili waseme ni nani aliyehusika. Polisi walipojaribu kupitia orodha ya wasafiri ilionekana chumba namba 32 hakikuwa na abiria aliyetumia, hivyo ilikuwa ngumu kwao kugundua ni nani alikuwa ndani humo. Vitisho vya hapa na pale, kuwafinya kidogo waliwakamata haikusaidia kitu. Ton alikaribia behewa la mizigo ambamo Isabel alijificha humo, alitembea taratibu na kwa hadhari kubwa huku akiangalia huku na kule, akapita behewa la kwanza mpaka la pili, kwa mbali aliona polisi wakija upande huo, akajibaza nyuma ya mlango kwa utulivu wa hali ya juu sana, polisi wale walipita wakiwa wanaongeea habari ile.

Isabel kutoka pale alipojibanza aliona polisi wale walipokuwa wakija roho yake ilitamani atoke ili awape habari ile na ile memory card lakini roho nyingine ilikataa kabisa asifanye hilo ila aikabidhi katika mikono salama. Aliumiza kichwa sana kutafakari kwa nini watu

wale waitafute memory card ile kwa nguvu zote, Isabel alikosa jibu alichofikiri ni kuwa treni ikisimama tu awahi kushuka na atoroke nayo ili ajue kuna nini ndani yake.

**SIKU CHACHE ZILIZOPITA**
**Bujumbura**
**Burundi**

**G**ARI aina ya Ramborghin iliingia kwa mwendo wa taratibu katika eneo la maegesho la Motel du Afrique, mwanamama mrefu, mwembaba aliyevalia nadhifu suti yake ya bluu bahari, mawani myeusi na kofia kubwa ya kiingereza ya rangi ya bluu bahari aliteremka taratibu kwa madaha huku akitoa tabasamu lenye bashasha, mlango wa upande wa pili alishuka kijana nadhifu akiwa ndani ya suti nyeusi kichwani hakuwa na nywele hata kidogo alitembea polepole akimfuata mama yule kwa nyuma, alionekana kama ni mlinzi wa mwanamama huyo. Mwanamama yule ambaye tabasamu lake halikujificha muda wote, alipanda ngazi taratibu kabisa na akasimama kama sekunde tano hivi mtu mwingine mwenye asili ya kizungu lakini alionekana amekaa sana Africa kutokana na rangi ya ngozi yake alifika kwa mwanamama yule na kumpa mkono kama ishara ya kusalimiana kisha akamkaribisha ndani ya motel hile ya kifahari. Wakiwa katika meza ya duara mwanamama yule alikutana na watu kama wanne hivi

na baada ya kutambulishana mmoja kwa mwingine mzungumzo yaliendelea.

“Yeah! Ni kazi ngumu kidogo lazima ikamilike ili tupate tunachotaka” mwanamama yule alilieleza jopo lile, baada ya kupumzika kidogo na kunywa maji akaendelea

“Au mnaona tutashindwa? Mbona mwaka ule tuliweza hapa Burundi na Rwanda, na sasa huko Uganda kaskazini kazi inaenda vizuri, kwa nini tushindwe hapa jirani, wamezubaa, wamelala” alimaliza

“Ni kweli madam, lakini kumbuka nchi hile haiingiliki kama tunavyofikiri, kila nikijaribu kufikiri tutawezaje na kutana na vikwazo vingi” mwanaume mmoja aliongea kwa hisia

“*Security* yao ipo makini sana, na isitoshe wananchi wake ni wazalendo mno, kwa hiyo tuna kazi ngumu sana mbele yetu” mjumbe mwingine alitia chumvi

“Sasa kama tunaanza kuweka mashaka, tutaweza?” yule mzungu aliuliza

“Wakubwa wametuma kazi na sisi tumekubali, pesa nyingi inatumika, tufanyeje?” aliuliza tena yule mzungu

“Acheni waoga nyie wanaume. Mkutano wetu ulopita tuliona watu wa kuwafanyia kazi kwanza, ambao wao wanaweza kuwa kikwazo kwenye mpango wetu *‘Mpango hasi’* kama walivyouita, si ndiyo jamani, tukawasiliana na watu wetu waktuambia nani na nani,

sasa kazi ya kwanza nikuwafutilia mbali, iwe kwa sumu, au kwa ajali, au kwa vyovyote vile ndani ya miezi sita *plan A* ikamilike" mwanamama yule alifoka
Akaingiza mkono kwenye pochi yake na kutoa flash akampa yule mzungu ambaye aliingiza kwenye laptop yake ndogo na kukopi mafaili fulanifulani kisha akamrudishia. Kikao kiliendelea kwa ufupi sana na baada ya hapo wote walitawanyika kila mtu katika njia yake. Mwanamama yule alitoka ndani ya Motel ile kama kawaida akasindikizwa na kijana wake yule mkakamavu ambao muda wote alikuwa amesimama pale kwenye ngazi, aliingia kwenye gari ile na kuondoka kwa kasi kuelekea kusikojulikana.

♠ ♠ ♠

**J**oseph Msengiyunva akiwa katika mazoezi yake ya karate ndani ya ua wa nyumba yake, kijasho kikimtoka kutokana na nguvu alizotumia katika mchezo huu anaoupenda tangu akiwa mtoto. Hata alipokuwa jeshini katika jeshi la serikali palae Burundi kazi yake kubwa ilikuwa ni kuwafundisha mchezo huu askari wenzake ambaye walikuwa hodari sana. Lakini nyuma yake alijihusisha na watu wenye kazi za kijasusi kuwasaidia hapa na pale katika kazi ngumu walizohitaji zifanyike haraka na kwa makini.
Baada ya kumaliza mazoezi yake aliingia ndani kuelekea maliwato kwa ajili ya kujimwagia maji kabla hajaanza ratiba nyingine. Alipofika sebuleni kwanza

kabisa alifungua compyuta yake ndogo na alipoingia mtandaoni alikuta kuna barua pepe mpya imeingia

*'JOB'* ndivyo ilivyoandikwa na hakukuwa na neno lingine. Jomse aliitazama ile barua pepe na kuvuta kiti kisha akakaa vyema nae akaijibu vile vile *'JOB'*.

Alipoenda kuoga na kurudi akiwa mezani anapata chai barua pepe nyingine ikaingia

*'Job 7:15'*, baada ya kusoma hiyo naye akatuma jibu

*'Holy bible'*, muda si mrefu alipata barua pepe iliyosema

*'Fellowship'* akasoma na kusubiri kidogo barua pepe nyingine ikaingia

*'Bujumbura Cathedral Library'* .

♠♠♠

Saa moja na robo asubuhi Jomse alipandisha taratibu ngazi za kuingia kanisa kuu la Bujumbura, baada ya kumaliza ngazi hizo alipita kushoto na kuelekea iliko maktaba ya kanisa hilo, aliingia na kutazama huku na huku hakuna aliyemjua, alielekea kati shelf la vitabu vya dini na akachagua Biblia Takatifu moja kwa moja alifungua agano la kale kitabu cha Job, alipofungua tu akakuta kijikaratasi kimepachikwa hapo, *'utamkuta Gitega Stadium mbele ya mlango mkubwa, muombe atakupa moto'* . Jomse alitoka katika maktaba ile na kukodi tax

"Uwanja wa mpira wa Gitega tafadhali" alimueleza dreva. Na dreva aliijua kazi yake sawasawa. Dakika chache alikuwa mbele ya mlango wa uwanja huo, kijana mmoja alikuwa ameketi kwenye jiwe akisoma

gazeti, Jomse akamsogelea na kumgongea kidole kama ishara ya kuomba kitu, kijana yule akatoa kiberiti cha gas na kukiwasha.

Gari nyeusi ilisimama mbele yao na wote wakaingia ndani na kuelekea kusikojulikana.

“Jomse, kutana na Mandi” kijana yule akamtambulisha Jomse kwa Mandi ambaye alikuwa analiendesha gari hiyo

“Na mimi naitwa Ton au Tonton kutokana na mwili wangu mdogo.” Naye alijitambulisha na wote wakacheka sana. Gari ile ilisimama katika nyumba Fulani na wote wakashuka na kuingia humo.

# 3

MZEE kasimu alikuwa chini amelala kimya hakujua hata kinachoendelea duniani, damu zikimtoka kifuani bila kujali. Mandi alishampiga risasi mzee huyu baada ya purukushani katika chumba kile cha injini. Sasa Mandi hakujua hata afanyeje kupunguza mwendo wa treni lile ambalo muda huo lilikuwa kwenye kasi ya ajabu. Mandi alijificha kuangalia kinachoendelea, mara akasikia sauti za watu wakiongea na kutahamaki aliwaona koplo Kibona na afande Benso wakiingia na bunduki zao. Wote walipigwa bumbuwazi baada ya kuona mwili wa mzee Kasimu ukiwa bila uhai.

“Ni nini hiki kinachotokea?” afande Benso aliuliza kwa mshangao

“Upppphhhh!!!!” Koplo Kibona alishusha pumzi ndefu na kujishika kiuno kisha akasema

“Nikimkamata huyu au hawa, kama ni embe dodo ntawala na maganda”

Waliuweka vizuri mwili ule na kuuhifadhi, kisha wakapiga redio kwenye behewa lao la usalama kutoa taarifa.

“Sasa hili dude nani ataliongoza!? Maana opereta ndiyo huyu kauawa, nani anayefanya unyama huu?”

Koplo Kibona alichukia, akaongea huku akirusharusha mikono yake. Alimuacha pale afande Benso akimuomba awasiliane na stesheni-masta ili amuelekeze anagalau cha kufanya ili kusimamisha kabisa treni ile. Koplo Kibona alitoka kwenye injini na kuelekea mabehewa ya nyuma ambayo yote yalitawaliwa na habari ya mauaji hayo, lakini hakuna aliyejua kama treni hilo lilikuwa likienda bila opereta.

Ton na Jomse walikuwa bado kwenye maficho yao kila mmoja akikwepa polisi lakini walishangaa kwa nini Mandi hajafanikiwa kumfanya operetta yule apunguze mwendo. Jomse alitulia na kila alipoitafuta simu ya Mandi haikuita kabisa, Ton nae vivyo hivyo. Koplo Kibona na askari wengine walii\kutana kwenye behewa lao la mwisho wakitafakari la kufanya huku hali ya afande Kirama ikiwa si yakuridhisha.

♠ ♠ ♠

**I**sabel alikaa sana katika maficho yake, alijaribu kufikiria cha kufanya na aliumia sana alipojua kuwa yule askari kijana aliyekuwa naye mle ndani kapoteza maisha kwa ajili yake, Isabel akaanza kulia, na liposikia Koplo Kibona akiongea na wenzake kuwa opereta ameuawa ilimchanganya zaidi 'yote haya kwa ajili yangu' alijisemea moyoni, aliumia sana alipojua kuwa muda wowote treni ile inaweza pata ajali na mamia ya watu kufa alijiona kuwa yeye ndiye chanzo cha kila kitu.

Akaomba Mungu ampe njia au wazo la kufanya lakini hakuamini kabisa kama polisi wale

akiwashirikisha watamsaidia au watamuweka ndani tu. Isabel akapata wazo, akaichukua ile memory card na kuitazama ukubwa wake akatoa simu yake nyingine ambayo ina uwezo wa kusoma card za mtindo huu akaipachika na kuiwasha simu akaona kuna faili Fulani lakinihaikuweza kufungua faili lile kutokana na format iliyotumika. Isabel alikuna kichwa, afanye nini akapata wazo akashusha begi lake la mgongoni kwa hadhari kubwa na kuchukua waya maalumu wa simu hiyo ambao unaweza kuunganisha ili kufanya kazi fulanifulani, akaupachika na kuunga katika laptop yake. Aliiwasha laptop kwa kufunika na likitambaa alililoliokota hapo ili mwanga usionekane na atakayepita njia. Akafungua ile *Memory card* nakukuta kuna faili moja tu lenye kichwa cha habari *'Mpango Hasi'*. Isabel alisoma taratibu faili lile huku akitetemeka na kuhisi kamasi jembamba likimtoka. Kila mara machozi yalidondokea kwe baobonye la *laptop* ile. Aliendelea kusoma mpango mzima Isabel alijikuta akiacha kusoma mara kwa mara faili hilo. Mpango hasi, mpango uliyoandaliwa na kikundi Fulani ambacho leno lake ni kuja kufanya mapinduzi nchini Tanzania kama ilivyofanyika huko Rwanda na Burundi mwaka 1994, mpango huo ulionesha utaratibu wote wakutimiza azma hiyo kwa hapa Tanzania lakini kuna watu ambao lazima wauawe kabla mpango huo haujaanza rasmi kwa kuwa watu hao watakuwa vikwazo katika mpango huo. Isabel alisoma majina yale yapatayo kama kumi na tano hivi. Isabel alibaki

mdomo wazi, sasa alijua kwa nini watu wale wanaitafuta memory card ile. Isabel alifikiri afanye nini kuliokoa taifa lake alipendalo kutoka katika mpango huu ulioitwa mpango hasi 'sasa taifa liko mikononi mwangu' alijiwazia lakini hakuwa na la kufanya. Kila wazo la kuwapatia polisi taarifa ile lilipomjia alilifuta mara moja. Akarudisha akili tena katika majina yale ambayo yaliandikwa katika orodha ile, majina yale yaliandikwa na mbele yake kuliandikwa sehemu mtu huyo anafanya kazi na ni kazi gain, Isabel alisoma majna moja baada ya jingine, majina mengine alishawahi kuyasikia lakini mengine ni mageni sana kwake.

Macho ya Isabel yakavutiwa na jina moja tu kwa jinsi lilivyo *'Kamanda Amata TSA1'* , Isabel alilisoma mara kwa mara lakini aliona labda huyu anaweza kutatua kitendawili hiki baada ya kusoma kirefu cha ile TSA *(Tanzania Secret Agency)* shauku ilimjaa Isabel lakini atampataje mbona hata simu haijui. Kwa kuwa msichana huyu alikuwa mtundu sana alipata wazo haraka, akachukua moderm yake na kuiunganisha kisha akawasha mtandao na kuiita kurasa maarufu duniani *'facebook'*, alipoingiza nywila zake kurasa ikafunguka na moja kwa moja alikwenda kwenye *search bar*, aka-*click find friend* akaingiza jina *Amata* akabofya *add friend* na hapo hapo akaingia kwenye meseji na kumuandikia

*'Amata, TSA1…*

*mimi naitwa Isabel, hivi sasa nipo katika treni ya kutoka Kigoma kuelekea Dar es salaam. Kuna watu wanataka kuniua naomba msaada wako haraka. Si mimi tu tupo watanzania zaidi ya elfu tatu ambao muda si mrefu tutakufa kwa ajali mbaya ya treni. Polisi mmoja na muendesha treni wameuawa, magaidi tunao humu ndani'*

Alipomaliza kuandika hiyo meseji akatazama kuna *notification* moja alipoicheki akakuta Amata amekubali urafiki, Isabel alijikuta anataka kuruka kwa furaha. Meseji yake ikajibiwa haraka

*'Isabel,*
*Hunijui na wala sikujui hayo matatizo waeleze polisi ndiyo kazi yao na si mimi'*

Isabel aliumia sana akajua kuwa labda alikuwa anawasiliana na mtu mwingine, hakusita akaandika tena.

*'kuna mpango kabambe, mpango wa mapinduzi katika nchi yetu, mpango huu unaitwa mpango hasi. Lakini kabla haujaanza plan A ni kuwauwa watu watakaokuwa vikwazo na wewe ni mmoja wao. Mimi nimeokota memory card ndimo nimesoma na kujaribu kila jina na lako ndiyo nimelipata katika mtandao'*

Isabel aliweka mikono yake mashavuni akiomba meseji ile ijibiwe haraka. Kwa upande wa Amata aliona swala kama hili si la kuletea mchezo, maana michezo kama hii ya dhihaka ameizoea ila hapendi kuipuuzia.

*'Nitumie hilo faili'*

Isabel akasita lakini afanyeje, akaanza kufanya haraka kutuma faili lile, lakini kabla halijawa tayari alijikuta kashikwa bega alipogeuka alipokea kofi moja kali, Isabel laptop ilimtoka mikononi na kudondoka chini, akatoka pale alipokuokota ile laptop kabla hajaifikia Ton alimpiga teke la mbavu liliomfanya aanguke jirani kabisa na ile laptop bila kuchelewa alibonyeza tarakimu Fulani kabla hajamaliza Jomse alimkanyaga mkono, Isabel alilia kwa uchungu akanyanyua mkono mwingine na kubofya fasta na meseji ile ikaenda, lakini bahati mbaya faili lile halikuweza kwenda. Ton aliichukua laptop ile na kuivunja vipande viwili walijaribu kupekua begi lake lote lakini hawakupata walichokitaka. Isabel akaona hapa mambo yameharibika alijivuta kutoka alipo huku akilia akaidaka ile simu akaifungua haraka na kutoa ile memory card. Kabla Ton na Jomse hawajamuona Isabel aliimeza ile memory card. Mara simu yake iliita akaitoa mfukoni na kuipokea kisha akaitupia karibu na mizigo ikiwa imepokelewa.

“Iko wapi?” Ton alipga makelele huku akimpiga mateke Isabel, Isabel alilia kwa uchungu akiwa pale chini anagalagla

“Utasema husemi, unafikiri kuna mtu wa kukutetea hapa? Nakuua” Jomse alimtishia na bastola yake. Mara polisi walifika eneo lile “Polisi… weka mikono juu!” alitoa amri huku akiwa kamnyoshea Ton bunduki ya SMG. Jomse alifyatua bastola yake kwa haraka, Koplo Kibona alipaishwa na kujigonga juu kabla ya kudondoka chini akiwa mfu. Kimenuka!

Hali ya hewa ikawa mbaya, polisi walirusha risasi kuwashambulia Jomse na Ton lakini kazi haikuwa rahisi kwani vijana hawa walikuwa wana mafunzo maalum ya kijeshi. Walitoweka eneo hilo na kukimbilia kwenye mabehewa ya watu wengine. Wale askari polisi nao waliwafuata uko huko.

♠ ♠ ♠

**K**amanda Amata, *Tanzania Secret Agency* namba 1, alisikia kila kitu kilichoendelea kwenye treni ile kupitia simu ya Isabel. Alitamani muda huo ajikute ndani ya treni hiyo baada ya kusikia kilio cha uchungu cha Isabel kupitia simu ile, afanyeje? Alinyanyua simu yake haraka na kumpigia nkuu wake wa kazi

“Hello” Amata aliita

“Hello mbona usiku sana kuna nini wakati mimi nimekwambia upumzike, Amata” Madam Selline au kama wenyewe wanavyomwita ‘S’ aliinuka na kuketi kujibu simu hiyo

“Dharula, Madam, kuna habari nimepata sasa, kwenye treni ya Kigoma kuja Dar kuna mauaji yanaendelea na huyu mtu kawasiliana na mimi moja kwa moja, msaada wako” Amata alisubiri jibu lakini akaona ukimya umetawala. Simu ikakatika, Amata alikunja uso wa lawama kwa mkuu wake wa kazi. Simu ya Amata iliita tena

“Kamanda samahani nilimpigia RPC wa Tabora na IGP kuhusu hilo nimepata taarifa, kutokana na uzito wa shughuli yenyewe naomba fanya unachoweza uende sasa hivi, helkopta ya polisi inakusubiri *airport.*”

Amata hakusubiri simu ya ile iendelee. Alikurupuka kitandani na kufungua kabati lake akachukua bastola yake moja na vikasha vya risasi kadhaa akatupia kenye mkoba wake. Akavaa jeans yake nyeusi, fulana nyeusi, buti za usalama, akapachika kisu chake kiunoni… kamili! Akachukua kofia-ngumu yake ya puendeshea pikipiki. Akaivaa.

Muda mchache tu alikuwa barabara ya Kawawa akielekea Magomeni, usiku huo hakukuwa na magari, ilimchukua muda wa dakika kumi tu kuwasili uwanja wa ndege terminal one, alikuta tayari rubani na msaidizi wamewasha injini tayari kuondoka.

“Kamanda… twende!” rubani wa Helkopta alimwita Amata na bila kuchelewa Amata alijirusha ndani safari ikaanza.

Wakiwa hewani Kamanda Amata alijilaza kwenye kijitanda cha kamba akitafakari hili na lile akijiuliza

imekuwa Isabel atumbukie katika tatizo kama hilo alijipa moyo kuwa akifika atajua kila kitu, moyoni alimsifu sana Isabel kwa kutumia akili siyo tu ya kuzaliwa lakini naya shule pia. Lakini mara nyingine alijiona mjinga sana akaona ingekuwaje kama amewekewa mtego kwa mtindo huo na ye kanasa kijinga namna hiyo, alijicheka na kujiona kweli yeye mjinga, lakini bado alijiuliza kwa nini usiku ule aliendelea kubaki akicheza na mtandao labda Mungu ana alikuwa na mpango wake katika hili.

“Kamanda, tukushushe Tabora stesheni au kituo cha polisi kati Tabora, maana tumeambiwa tukusikilize wewe” rubani wa helkopta alimweleza Amata

“Itafute treni yenyewe, nataka kushuka kwenye treni” Amata aliwajibu

Helkopta la polisi lilikata anga, kwa kuwa rubani alikuwa analiongoza kuelekea katika makao makuu ya polisi ya mkoa Tabora, ilibaidi abadili uelekeo na kuitafuta treni ile ilipo kwa wakati huo.

“Kapteni Scopa, Chopper namba PLS 12 H ova” rubani yule aliongea kwenye chombo maalumu cha kuongelea alichokivaa masikioni mwake

“*Tunakupata Kepteni, tupe habari ova*” sauti kutoka makao makuu ilimjibu

*“Tunabadili uelekeo, kadiri ya maelekezo ya Kamanda ova”*

*“Uelekeo wapi Kepteni?”*

*“Ameomba tuelekee mahali treni ilipo ili kazi ianze mara moja ova”*

*“Read and clear ova”*

*“Work in progress”* mabadilishano ya taarifa hiyo yalikamilika na kepteni Scopa alimpa ishara msaidizi wake Baba Lao ageuze uelekeo. Chopper lilibinuka upande upande kuelekea magharibi mwa mji wa Tabora ilikuwa yapa saa saba kasoro usiku giza nene lilikuwa limefunika anga.

Kamanda Amata alitoa bastola yake ndogo na kuijaza risasi na magazine iliyobaki aliihifadi vizuri, aliweka vizuri kisu chake na kuvaa soksi zake za mikono tayari kwa kazi, aliicheki saa yake na kuibonyeza kuweka kitu Fulani vizuri, alivaa kofia yake aina ya nyeusi aina ya mzula akatia big G yake mdomoni.

Kepteni Scopa na msaidizi wake walikuwa bize kuliongoza *dude* hilo huku wakisikiliza muziki wa Les Wanyika walionekana wakiipenda sana kazi yao. Kwa mbali walianza kuiona treni ile ikiendelea kuikata reli kwa kasi ya ajabu ambayo ilimfanya kepteni Scoba kuhofu,

“Kamanda” aliita

“Hii treni ya umeme au?mbona inakimbia namna hii?” aliuliza

“Kuna itilafu kwenye Injini naenda kurekebisha” Amata alijibu

“*All the Best*” Scopa alipokea jibu hilo na kutoa saluti kwa Kamanda Amata

Tayari Chopper ya polisi ilikuwa ikienda sambamba na treni hiyo

“Weka Chopper juu ya treni” Amata alitoa amri huku tayari akiwa mlangoni, upepo mkali ulimsumbua macho. Scopa aliipeleka Chopper ile juu, na Kamanda Amata alivizia kuona kasi ile ya treni kama inawiana na Chopper ili aweze kurukia juu yake.

♠♠♠

**H**ekaheka zilendelea katika stesheni ya treni ya Tabora, polisi tayari walikuwa pale usiku ule wakiwa na hasira dhidi ya majambazi hao kwa kuwaumiza wenzao

“Ama zao ama zetu” walisikika wakitamka neno hilo mara kwa mara. Stesheni masta alikaa tu ofisini kwake haelewi kinachoendelea ni jinsi gain ataikoa treni hiyo ambayo sasa ilikuwa inakwenda kwa kasi isiyo ya kawaida tena bila operetta, mara kwa mara alisimama na kukaa chini, aliweka mikono kichwani na kuitoa kisha kuiweka mfukoni, mara alikwenda haja ndogo na kurudi, alishika hiki akashika kile ili mradi tu hali ilikuwa ni mkanganyiko hasa alipofikiria kuwa endapo treni hiyo itapata ajali katika mwendo kama huo ni wangapi watabaki Yatima, wangapi watabaki Wajane na walemavu ndiyo usipime, aliteseka sana moyoni na kila alipopiga simu katika treni hiyo simu haikujibiwa kabisa.

Alitoka nje ya ofisi na kuangalia hekaheka zilizopo hapo nje, waandishi wa habari walishafika, vijana wa msalaba mwekundu walikuwa pale tayari kwa lolote,

polisi walitanda kila kona ya stesheni ile wenye mbwa, farasi, acha wale wenye bunduki za aina mbalimbali. Stesheni masta Bw Nimrod Msigwa alivuta hatua ndogondogo kushuka ngazi za jingo lile la stesheni huku akionekana wazi hajui ni wapi anaenda.

Punde tu RPC wa mkoa wa Tabora aliingia eneo hilo naye kushuhudia kinachotokea baada ya kupata simu toka makao makuu ya Polisi huko Dar es salaam. Alikutana na stesheni masta Bw Nimrod na kusabahiana lakini wote walionekana wakiwa na mawazo mengi walisimama pamoja kimya wakiangalia hekaheka za hapa na pale hakuna aliyemsemesha mwenzie. Mafundi nao walijaribu kurekebisha reli huku wakiimba nyimbo zao.

“Samahani, Bw Nimrod, kwa uzoefu wako unafikiri treni hii itafika hapa saa ngapi?” kamanda wa Polisi wa mkoa Tabora Bw. Sylvester Matinde alimtupia swali Bw Nimrod ili kuvunja ukimya ule

“Kawaida ingeingia hapa saa kumi na moja alfajiri ndiyo ratiba ykae lakini kwa jinsi ya hali ilivyo itafika mapema zaidi ila siwezi kujua ni saa ngapi” alijibu

“Sasa kama watu wa reli mnachukua hatua gain kuokoa vifo vitarajiwa?”

“Kama unavyoona mafundi wapo kazini, wanatengeneza njia moja tu ya reli ili kama ikifika hapa basi inyooshe njia na wao watafanya utaratibu wa kuipunguza kasi, wenyewe wanajua kazi yao, usiwaguse” Stesheni masta alimalizia jibu lake.

Kamanda wa polisi aliendele kuongea machache na watu wake na kuwapanga hapa na pale mara nyingi aliwasiliana na vijana wake walioko ndani ya treni hiyo japo kwa taabu kidogo lakini waliendelea kuwasiliana.

# 4

## Kigali-Rwanda

SIMU ya mezani iliita usiku huo chumbani kwa Madam Rose, kabla ya kupokea simu hiyo aliangalia saa yake ya ukutani na kugundua kuwa ilikuwa tayari ni saa saba za usiku, alikunja sura kwa kuwa hakupenda kupokea simu mida hiyo…

"Hello!" aliita kwa mapozi kama kawaida yake

*"Madam, we are in trouble!"* sauti ya upande wa pili iliongea kwa kutweta kama mtu aliyekimbizwa na mbwa wakali.

*"What?"* Madam Rose aliuliza kwa hasira huku akitoka kitandani kwake na kusimama dirishani akiangalia nje

"Vijana tuliyowapa kazi wameharibu kwa uzembe wao" sauti ile iliendelea

"Khaaaa!" alinguruma Madam Rose na kuendelea

"Imekuwaje?" aliuliza

"Amenipigia simu Mandi kuwa wapo kwenye treni ya kwenda Dar, lakini ile memory card imepotea na wanamuhisi msichana mmoja kuwa kaichukua, sasa wameshaingia matatizoni na Polisi. Tutapona?" sauti ile iliongea kwa kukata tama

"*Come on*! Ni wajinga sana, nimewapa tiketi za ndege wawahi Dar, sasa wanapoteza muda, mbona

tutaonekana wote *hopeless*," Madam aling'aka kwa hasira. Sauti ya upande wa pili ilitulia bila kusema kitu

"Frank! Frank!" Madam Rose aliita kwa hasira

"*Yes* Madam, nakusikia" sauti ile ilijibu

"Unashauri nini katika hili?" Madam aliomba ushauri kwa Frank maana alihisi wazi kuwa endapo watakamatwa basi halihaitakuwa shwari hata kidogo maana wanaijua serekali ya Tanzania jinsi isivyotaka mzaha katika dulu za usalama.

"Madam hakuna jinsi, inabidi tuwaokoe wenzetu ili tuuokoe mpango wetu" Frank alijibu sasa kwa kujiamini

"Ok Frank fanya hivyo halafu tuwasiliane, lakini hawa jamaa ni wapumbavu kabisa. Na ukiwaokoa uwalete hapa moja kwa moja" Madam Rose aliendelea kufoka kwenye simu, alipomaliza aliitupa simu hiyo na yeye mwenyewe kujitupa kitandani kwa hasira.

♠♠♠

**F**rank, alipiga simu kwa vijana wake walioko huko msitu wa Nyakanazi ambao wao wapo tayari kwa lolote na muda wowote, vijana waliochoka maisha ambao kwao kuua haikuwa shida ilikuwa kama chai ya asubuhi tu. Maisha yao waliyajenga huko Biharamuro katika mapori ya Nyakanazi kikubwa ni kuteka mabasi na kupora mali za wasafiri, kila kukicha walipambana na polisi katika shughuli zao hizo lakini hawakukoma kabisa. Katika kimbizanakimbizana hiyo wengine walikimbilia mbali huko sehemu za Nguruka,

Kazulamimba mpaka Uvinza. Kote wakijifanya wababe kupora mali za wananchi. Wengine waliishia jela, wengine waliuawa kwa risasi za polisi au wananchi wenye hasira, lakini wengine walisalimika na kufanya makazi yao katika mapori hayo. Hakuna mtu aliyejua wanasubiri nini siku zote hizo, hata wao hawakujua wanachokisubiri ni kipi na kitatokea lini.

Simu ya mmoja wao iliunguruma katika mfuko wa koti lake

"Nani tena usiku huu anapiga au ndiyo wanga wenyewe" aliongea maneno hayo kwa sauti ya kilevi, huku akijipapasa kuitoa mfukoni

"Eee lete maneno mdosi" alimwambia mtu wa upande wa pili

"Ee nakupata mdosi"(…)"Vijana wapo gado kaka, hawana *kwere*"(…)"Niambie kiongozi"(…) "ok nimekupata, kuwaokoa tu, tunajua kazi yetu vizuri, hii ndiyo rescue mission… tega sikio utapata habari" yule kijana alikata simu na kuwaamsha wenzake.

"Oya Masela, inabidi tufanye *rescue*, mabradha wametaitiwa kwenye gogo, sasa tuhakikishe tunawatoa hai mwana" aliwaeleza wenzake ambao tayari muda huo walikuwa wameshaanza kukoroma.

"Donge lipo? Sio tunafanya kazi ya kanisa" mmoja wao alimuuliza

"Donge lipo we twende kazini" akampa jibu.

Vijana wale walinyanyuka na kupotelea msituni, mara walitoka na jeep ya kijeshi wakiwa na zana mbali mbali

tayari kutekeleza waliloagizwa, bangi zilikuwa zikifanya kazi muda huo.

Kilometa mia moja kabla ya stesheni ya Tabora vijana wale walianza kufungua vyuma vya reli ili kuipoteza njia, wao hawakujali kama wangapi watapoteza maisha ila walichojali wao ni kuwaokoa watu wao watatu tu waliotumwa. Kazi iliendelea kwa nguvu zote kulfungua mataruma hayo.

“Madogo fasta madogo, kaza kaza” kiongozi wao aliwaelekeza vijana wake. Kisha akachukua simu yake na kupiga namba ileile

“Ee mdosi, sasa waambie walengwa wasogee behewa moja kutoka kwenye injini, kwa maana kwenye ajali yoyote ya treni behewa la pili hua halianguki, hapo tutawapata na kutokomea nao” yule kijana alionghea kwenye simu na kutoa hayo maelekezo. Kazi ilikamilika trauma mbili moja ya kushoto na nyingine ya kulia zilishaondolewa, vijana wale walijificha porini umbali kama wa mita mia tano wakiangalia na kusubiri kuona kitachotokea.

Gurudumu mia mbili za chuma ziliendelea kusumbuana na vyuma vigumu vya reli ya Mjerumani usiku ule. Kasi ya ile treni haikuwa ya kawaida, watu wote walitulia kimya wakiwa hawajui watafanya nini kila mtu aliomba kwa Mungu wake aepushe balaa hilo, wakati wengine wakiwa katika maombi lakini wengine walikuwa hoi bin taabani. Afande Kirama alikuwa ameshapoteza fahamu muda mrefu. Koplo Kibona nae alikuwa tayari ameshaitwa jina lingine *‘Marehemu’*.

Mzee kasimu nae alikwishaiaga dunia baada ya kupigwa vibaya na Mandi pale alipojifanya kuleta ubishi, na mwili wake wakati alipokuwa akianguka aligonga nobu ya kuongezea mwendo kasi wa treni hiyo hivyo treni iliendelea kuongeza kasi bila mpangilio. Kengele za hatari zilianza kugonga ndani chumba cha opareta wa treni hiyo. Hakuna la kufanya, Polisi aliyeachwa hapo hakujua chochote cha kufanya alibaki aking'aa macho tu.

Mandi aliendelea kujibanza palepale katika moja ya vijichumba vidogo vilivyopo katika injini hiyo, aliendelea kuangalia nyendo zote za askari yule hakuna alichokitaka zaidi ya bunduki yake aina ya SMG. Yule askari alikuwa akitembea huku na huko na mara nyingi alikuwa akikaa kwenye kile kiti kirefu cha operetta akitazama huko treni iendako. Mandi alitoka katika maficho yake na polepole alianza kunyata kumfuata askari yule pale alipoketi.

Kwa kuwa viatu vyake vilikuwa na soli ya mpira hakuweza kusikika katika sakafu ile ya chuma. Yule askari aliketi vile vile kwa utulivu akiwa ameshika bunduki yake lakini alishamuona Mandi kupitia katika kioo cha mbele kilichokuwa kikiangazwa na mwanga hafifu kutoka katika moja ya balbu ndogo iliyopo katika kijichumba fulania katika injini hiyo. Yule askari alijifanya kama anainzia hivi lakini alikuwa akimwangalia Mandi kwa kificho. Mandi alipojiandaa kumvamia akiwa karibu kabisa alijikuta akipigwa kwa kitako cha bunduki. Maumivu yalimfanya mwanaume

huyo kuyumba na kujishika paji lake la uso ambalo mpaka hapo lilishavimba kutokana na pigo lile. Yule askari alitoka pale katika kile kiti na kurukia chini, kabla Mandi hajatulia alipigwa mateke mawili ya kuzunguka na alipotaka kujiweka sawa alijikuta akipata ngumi za mfurulizo zilizompelekea kwenda chini damu zikimtoka mdomoni na puani. Kwa kasi ya umeme Mandi alijinyanyua kisarakasi na kupiga mapigo ya judo yaliyompata yule askari kifuani na kumfanya akohoe kidogo na kutema damu. Mandi alijirusha kwa ufundi na kuzamilia kuuwa lakini askari yule aliepa na migugu ya Mandi ikatua katika dash board ya treni ile mguu mmoja uliinasa kamba ya bunduki nayo ikaanguka chini. Alipotaka kuichukua yule askari aliipiga teke ikasogea mbali kidogo, Mandi akatua palepale ilipokuwa ile bunduki. Alipofika chini tu yule askari bila kuchelewa alimpiga teke lililotua usoni na kumgeuza Mandi kuwa chali. Mguu wa pili wa yule askari haukufanya ajizi ulitua kwenye koromeo kwa mtindo *'kutimba'*. Mandi aliushika mguu ule na kujaribu kuutoa kutoka katika koromeo lake.

Kutokana na misuli yenye nguvu ya mikono ya Mandi aliweza kuuondoa mguu ule na kuuzungusha kwa nguvu zake zote. Maumivu makali yalimpata askari yule. Akapiga yowe la uchungu na kuangukia upande wa pili. Mandi alijinyanyua na kuifuata ile bunduki kabla hajafika alihisi kupigwa na kitu kama chuma kisogoni. Yule askari pale alipoangukia kulikuwa na kasha la vifaa vya ufundi *'tool box'*, kumbe

alichukua spana na kumrushia Mandi. Kwa pigo lile Mandi aliyumba na kujigonga katika bomba la chuma lililopo ndani ya cabin hiyo.

♠ ♠ ♠

"Shusha zaidi! Tena! Tena! Tena! Apo-hapo haya ongeza kasi" Kamanda Amata alikuwa akitoa maelekezo kwa kepteni Scoba aliyekuwa akiliongoza *chopper* lile la polisi-anga. "Kisha hakikisha unakuwa mbele ya treni, mbele sana ili kuangalia usalama wa reli kisha nipe taarifa" Kamanda Amata alimuelekeza kepteni Scoba huku akimpa kifaa cha mawasiliano na kumpatia na yeye kimoja akakibana katika mkanda wake wa begi. Amata alitua vizuri kabisa juu ya paa la moja ya mabehewa ya treni hiyo ambayo ilikuwa ikienda kasi sana. Akatulia kidogo kuliacha *chopper* lile liende, na baada ya hapo alianza kutembea kwa mtindo wa *'jogging'* kuelekea kati ya behewa na behewa ili apate nafasi ya kuingia ndani.

♠♠♠

"Tutoke kwa nje tupande juu ya paa ili kama jamaa wameshahujumu sisi tutapona kwa kurushwa pembeni" Ton alimwambia Jomse ambaye alionekana kutokubaliana na hilo.

"Hatuwezi kuondoka mpaka tuhakikishe tumeipata ile *memory card*" Jomse alisisitiza

"Tutaipataje hata hatujui ilipo?" Ton aliuliza

"Anayo yule msichana, tumeshamzimisha twende tukaubebe mwili tumpekue kwa utulivu" Jomse

alimwambia Ton, lakini Ton alionekana kutoafiki wazo hilo.

“Mandi, hatuna *information* yoyote toka kwake” Ton alimwambia Jomse

“yule nae bwege, achana nae kama kakamatwa atajua yeye” Jomse alijibu kwa mkato

“Sio hivo Jomse we unafikiri akikamatwa na sisi tutapona? Sote tupo kwenye *mission* moja lazima tumtafute, atatoa siri akibanwa na polisi.” Ton alimueleza Jomse. Jomse aliona kweli amekosea kutoa jibu lile, akakubaliana na Ton. Mara simu ya Jomse ilipokea meseji *‘Rescue mission imekamilika, nendeni behewa la pili kutoka katika injin haraka’*

“Twende” Jomse alimvuta Ton, na wote kwa mwendo wa kunyata walitoka katika maficho yao na kuelekea huko walikoagizwa kwa tahadhari kubwa. Jomse alipendekeza wapite kwa nje, Ton mara hii akaafiki, kwa kutumia dirisha moja walifanikiwa kutoka na kupanda juu ya paa wakiwa na nia ya kutembea juu ya paa mpaka behewa la pili lakini pia ikiwa ni moja ya kuwakwepa Polisi ambao bado walikuwa wakipekua behewa moja baada ya jingine.

Wakati hayo yakiendelea Kamanda Amata kwa kutumia upenyo kati ya behewa la usalama na la abiria aliteremka taratibu katika maungio hayo na kukanyaga sawia panapotakiwa, moja kwa moja aliingia behewa la polisi kwanza.

“Simama apo hapo ulipo, weka mikono juu…” Polisi mmoja mwenye *short gun* mkononi alimuamuru

Amata. Bila kupinga Amata alinyanyua mikono yake juu. Kutokana na hali iliyogubika katika treni hiyo Amata alijua wazi akileta mchezo atafyatuliwa maana polisi walishaona kila mtu sasa ni adui kwao.

"Samahani nimekuvamia" huku akitoa kitambulisho ambacho mara nyingihuwa akioneshi ovyo.

"Samahani Kamanda!" askari yule aliomba msamaha na kutoa *salute* ya kiukakamavu. Amata aliuangalia mwili wa Afande Kibona uliokuwa umelazwa kwenye machela na kufunikwa kwa shuka maalum kwa kazi hiyo, kisha akamwangalia afande Kirama ambaye alionekana kupoteza fahamu. Amata alitoa bastola yake na kuiweka vizuri tayari kwa kazi. Alianza kupita behewa moja na jingine akiwa na bastola yake mkononi. Mabehewa mawili ya mwanzo yalikuwa tupu akafika behewa la mizigo ambalo lilikuwa na giza. Akatembea kwa hadhari kubwa sana, taratibu akitazama huku na huko aliweza kuona vizuri kutokana na mawani yake aliyovaa ambayo humuwezesha kuona gizani. Aliona mtu kalala chini, alipomwangalia vizuri ni msichana, damu nyingi zikimtoka mdomoni na puani, uvimbe ulikuwa katika uso wake. Amata alirudisha bastola yake katika kikoba chake na kuufikia ule mwili kwa haraka, pembeni aliona *laptop* iliyovunjika vipande, simu iliyokosa betri na mfuniko.

"Isabel…" alijikuta akiita hata kama hakuwa na uhakika kuwa ni yeye. Alichukua begi alilolikuta hapo

na kutia vile vipande vya laptop na ile simu kisha akajaribu kuangalia hapa na pale katika begi hilo akakuta kitambulisho. Alipokisoma ndipo alipo hakikisha kuwa ni yeye.

Akamyanyua kutoka pale chini. Haikuwa rahisi kwa maana Isabel alikuwa kibonge kwelikweli, alipomuweka vizuri katika mikono yake alitembea mpaka behewa la usalama na kumuhifadhi vizuri, lile begi nalo aliliweka pazuri, akatoa kifaa chake cha mawasiliano.

“Scoba, Scoba!” aliita.

“Yes kamanda, tupo mbele sana hali ni shari kamanda”

“Geuza *chopper* uje haraka behewa la usalama” Amata alimuamuru Scoba

“Nimekusoma Kamanda”. Scoba aligeuza chopper na kurudi, haikuchukua muda walikuwa tayari wameifikia treni hiyo. Kupitia dirishani alimuelekeza Scoba kushusha *chopper* ile mpaka mlangoni. Kwa kushirikiana na yule askari mmoja walihamisha mwili wa koplo Kibona kuuweka katika chopper, kisha afande Kirama na Isabel, kazi haikuwa rahisi sana kwa kuwa vyombo vyote vilikuwa katika kasi kubwa lakini kwa kusaidiana walikamilisha zoezi hilo. Amata alipiga *salute* kwa Scoba kuonesha shukrani na Scoba aliondoa *chopper* kuwawahisha hospitalini Tabora.

Amata pamoja na askari aliyebaki walianza safari ya kwenda behewa baada ya behewa. Mabehewa manne ya mwanzo yalikuwa tupu, kwa sababu Koplo

Kibona marehemu aliwaamuru abiria kukaa sehemu moja ili kuweza kufanya ukaguzi kuwapata wauwaji.

Zoezi lilikamilika lakini hakuna aliyeshukiwa kuwa na hatia hiyo, hata wale waliohisiwa nao waliachiwa kutokana na kuwa hakukuwa na ushahidi uliokamilika. Abiria waliruhusiwa kurudi mabehewa ya nyuma ili kutoa na nafasi kwa operesheni hiyo kwenda mabehewa ya mbele.

Wakati huo Jomse na Ton walilala juu ya paa la behewa la kwanza wakisubiri kitachotokea kama walivyoamuriwa. Walimtumia ujumbe Mandi ili kama yupo hai afanye mchakato kama huo. Mandi alikuwa hoi baada ya kupambana na polisi yule ambaye sasa aliwekwa chini ya ulinzi wake.

“Simama juu!” yule askari alimuamuru Mandi kisha akaendelea, “Ongoza njia twende”

Mandi akiwa mikono kichwani aliongoza njia kuelekea kwenye mabehewa mengine huku nyuma yake akifuatiwa na yule askari. Baada ya behewa moja kulipita walipofika behewa la pili mbele yao kulikuwa na askari wawili wakija upande huo. Mandi aliona sasa amekwisha. Hana jinsi, iliyobaki ni kujitetea awezavyo. Alishusha mikono na kugeuka kwa kasi, kwa pigo moja tu alilompa yule askari alifanikiwa kuipata bunduki ile na kuiweka sawa kwa mashambulizi. Kabla hajafanya lolote aliona kitu kama jinamizi likipita juu kwa kukanyaga mabega ya askari wale. Pigo moja la usoni lilimpepesua Mandi na bunduki ikamtoka mikononi. Mandi alijiinua kwa ustadi na kusimama wima

kumkabili Amata ambaye alikuja hapo kama mzimu. Mandi alipiga kareti ambazo Amata alizipangua kwa ufundi sana. Akaona hapa anapambana na mjuzi. Alipiga pigo jingine na Amata alimkamata vizuri na kumtwanga kichwa ambacho kilimtonesha ile nundu yake.

“Aih!” alitoa ukelele wa maumivu. Akajitoa katika mikono ya Amata akarusha ngumi ambayo Amata aliiona na kuikwepa kisha kwa kutumia viganja vya mikono yake alimsukuma nyuma na kumrukia teke la kichwani lililompepesua na kumpeleka chini. Akajigonga vibaya kwenye meza iliyopo hapo.

“Mkamate, tia pingu” Amata aliamuru

Kabla hawajamfikia, Mandi alijinyanyua na kujirusha nje kupitia dirishani. Kitendo kisichotegemewa. Amata alitikisa kichwa na wote wakakimbilia dirishani kuangalia. Mandi alinasa kidogo mguu na hivyo kupoteza uelekeo. Alijipiga katika ubavu wa behewa na alipochomoka tayari gurudumu za chuma zilishadaka mikono kilichofuatia ni kifo kibaya cha kukanyagwa na treni, mwili wake ulisambaratika huku na huko.

“Amejichagulia kifo chake, muache aende” Amata aliwaambia wale polisi. Amata na wale polisi walifika kwenye injini lakini hawakuweza kuona cha kufanya.

Amata alipojaribu kuchezea ile nobu ya kupunguza kasi alikuta imejam haifanya kazi tena.

“Oya, mchuma umekufa huo hauwezi kusimama wala kupungua kasi, cha kufanya tuokoe ndugu zetu” Amata aliwaeleza wale polisi,

“Kivipi kamanda?” mmoja wa wale askari aliuliza

“Tutenganishe mabehewa kutoka katika injini” Amata aliwapa mbinu. Kwa kuwa wao walikuwa behewa la pili kutoka injini na behewa la kwanza halikuwa na mtu hivyo wakaanza kusaidiana kutenganisha behewa la pili kutoka injini. Kazi haikuwa rahisi maana wote hawakujua mabehewa hayo yaliunganishwa vipi, walijitahidi kufyatua hiki na kile wakianza na mipira ya upepo na nyanya za umeme.

“Jamani hivi humu hakuna Tiitii?” Amata aliuliza “Maana wao wangeweza kutusaidia” aliongeza kusema. Kazi iliendelea kutenganisha kiungio kile, jasho liliwatoka wanaume wale lakini walishindwa. Wakiwa wamekaa upande wa behewa la tatu, Amata alishikwa na hasira na kukanyaga kwa nguvu chuma kimoja kilichokua hapo katika maungio. Mara aliona behewa lile likijiachia, cheche za moto kidogo zikatawanyika huku na huko lakini walishuhudia injini na behewa moja vikienda peke yake, na mabehewa yaliyobaki yalifuata kwa kasi ileile, Amata na wale polisi walibaki kuangalia nini kitachotokea.

♠ ♠ ♠

Kikao cha dharula kiliitishwa katika ofisi ya waziri wa ulinzi eneo la Msasani makao makuu ya JKT. Kikao

hicho kiliwakutanisha watu wachache usiku ule, waziri wa ulinzi mwenyewe, Madam S akiwa ndiyo *top* wa idara ya TSA, na IGP.

“Unajua tatizo lenyewe jinsi alivyoeleza Kamanda Amata bado halijawa wazi, anasema aliyumiwa ujumbe wa facebook na mwanamke usiku ule na katika mabishano yao alifanikiwa kupata namba ya simu na kumpigia ndipo aliposikia kilio cha msichana na sauti iliyomlazimisha kutoa kitu Fulani, kasha mirindimo ya risasi ikasikika.” Madam S aliueleza mkutano huo “Mi nilipiga simu kwa kamanda wa polisi Tabora na akathibitisha kuwa kapokea simu toka kwenye treni kuwa kuna mauaji yanaendelea na kijana wetu mmoja ana hali mbaya baada ya kupigwa risasi na hao majambazi.” IGP aliongeza

“Sasa hao majambazi wanataka nini kwa huyo mwanamke? Mi nafikiri hili swala tuwaachie polisi washughulike kabla hatujaamua kuingiza nguvu kubwa japokuwa tumeshaanza kufanya hivyo” Waziri alitoa rai

“Hebu ngoja tupate mrejesho kutoka Tabora baada ya Amata kukamilisha uchunguzi wake halafu tutawasiliana” Madam S alishauri.

Mazungumzo mawili matatu yaliendelea juu ya usalama wa nchi lakini bado walikuwa na kitendawili cha ni nini kilichotoke katika treni hiyo hata mawasiliano yaende kwa Amata moja kwa moja, lilikuwa ni kama wingu zito kati yao ambalo hakuna

hata upepo wa kuliondoa. Waziri wa ulinzi mara ashike hiki mara kile hakujua afanye nini

“Sasa ni nini kinaendelea? Kwa nini treni hiyo isizuiwe?” Waziri aliuliza

“Mheshimiwa, kwa taarifa tulizo nazo operetta wa treni hiyo ameuawa kwa hiyo hakuna anayeweza kulimudu, hivyo linakwenda tu” IGP alimjibu Mh waziri.

“Ha! Endapo litapata ajali si mamia watakufa… Mama yangu!” yule waziri alishtushwa na taarifa hiyo na alionekana wazi kabisa kuchanganyikiwa bila kuficha. Kimya kilitawala katika mkutano huo na kila mmoja alikuwa anawaza lake na hakujua nini mwenzake anachofikiria. Madam S alikuwa wa kwanza kuvunja ukimya huo kwa kujikohoza kidogo

“Kwa nini tusiwasiliane na mkuu wa polisi Tabora kujua kinachoendelea?”

“Amesema yupo pale stesheni Tabora pamoja na stesheni masta hawana la kufanya kwa sasa ila tu kuna wale mafundi wa reli ndiyo wanatengeneza njia ili kama ikifika hapo isilete maafa zaidi” IGP alitoa jibu

“Hiki ni kitendawili kikubwa, wananchi watakufa mamia kwa mamia, Yesu wangu!” Mh waziri alisikitikia hali hiyo na kutoa maagizo

“Hebu mwambie mkuu wa polisi Tabora ahakikishe anafanya lolote kuokoa maisha ya watu” Waziri alitoa ombi. Madam S katika kiti chake cha kuzungukazunguka alikuwa hana shaka sana

“Tusubiri kitachotokea, naamini Kamanda Amata atafanya kazi, na roho za watu zitapona tu” Madam S aliyasema hayo huku akichezea kalamu yake kwa mikono yake miwili

“Madam S, una uhakika Kamanda atafanya kitu?” Waziri aliliza

“Naamini kwa asilimia tisini na tisa mheshimiwa, ndiyo maana sina wasiwasi na hilo” Madam S alijibu kwa kujiamini kabisa.

“Ok basi fuatilieni tukio hilo hatua kwa hatua mnijulishe, na asubuhi tuondoke wote kwenda Tabora” Waziri alimaliza na kufunga kikao hiko cha dharula.

♠ ♠ ♠

Kutoka ndani ya kichaka kimoja vijana wale wavuta bangi walitulia tu. Kwa mbali waliiona treni ile ikija kwa kasi sana usiku ule.

“Oya jiandaeni sasa hivi kitu kinaitika, we Nyau washa *jeep* hiyo tayari tayari” kiongozi wao aliwapanga vijana wake, na wote wakakaa tayari.

“Kwa hiyo hatupekui kidogo?” mwingine aliuliza huku akivuta pafu la mwisho na kukitupa kipisi kile cha bangi porini.

Kitu wasichokitegemea kilitokea, kishindo kikubwa cha kutisha. Injini ya treni ile ilijipiga kwenye mawe na mchanga na kutoka nje ya reli na kusimama porini ikifuka moshi mweusi, behewa moja liliokuwa pamoja na injini hiyo lilinyanyuka na kujikunja vibaya kisha likajipiga ubavuni mwa injini ile na kubondeka

vibaya. Jomse na Ton walirushwa mbali na kudondoka mchangani. Kutoka porini vijana wale walipigwa na butwaa maana wameona kipisi tu ambacho kimekuja lakini treni iliyobaki hawajaiona kabisa. Walimuona Jomse na Ton wakigalagala mchangani waliwakimbilia na kuwaokota moja kwa moja waliwapakia katika jeep

“Mbona mpo wawili?” yule kiongozi wa wale vijana aliwauliza

“Hata hatuji mwingine yuko wapi, nyie twendeni hayo tutayacheki kesho” Jomse aliwajibu na wote wakapanda katika *Jeep* moja na kutokomea porini.

“Mandi mjinga sana, na yule ndiye atakayetutia matatizoni kwa ujinga wake” Ton alimueleza Jomse wakati gari lile likikata mapori kuelekea kusikojulikana.

“Na mi’ nilishalijua hilo… sasa sijui bwana twende tutulie kwanza tutajua la kufanya” Jomse alimjibu Ton.

Yale mabehewa yasiyo na kichwa yaliendelea kwenda kwa kasi lakini yalionekana kukosa nguvu hasa yalipopambana na miinuko, muinuko wa mwisho ulikuwa mkubwa zaidi yalipanda mpaka katikati yakasimama kisha yakaanza kurudi nyuma. Abiria wote walitulia kimya kabisa wakisubiri mwisho wake. Mchezo huo uliendelea na mwisho mabehewa yale yakasimama bila kuleta shida yoyote. Abiria walipiga kelele za furaha kwa kupona dhidi ya kifo ambacho hawakukitarajia. Wengi waliamini sala zao zimewaokoa. Waliokuwa mbele kabisa, polisi na Amata waliamini ujanja wao umewaokoa. Amata

alikumbatiana na polisi wale kwa shangwe hawakuyaamini macho yao kile wanachokiona. Abiria walianza kuteremka kwa furaha japokuwa treni ile ilisimama porini sana na ilikuwa tayari usiku mwingi, wote hawakuamini kama wamepona walianza kuimba na kucheza kwa furaha. Amata aliwatazama wananchi wale, machozi yakaanza kumtoka *“wengi wangekuwa marehemu, wengine wangekuwa yatima na walemavu, asante Mungu, Asante Isabel”* Amata aliyasema hayo bila kujijua akiwa kasimama kando ya mabehewa hayo akitazama wananchi wale wakicheza na kuimba.

“Tumesalimika, tunaomba msaada wa usafiri kutoka hapa tulipo, *ova*,” Polisi mmoja alikuwa akiongea katika *redio call* kutoa taarifa makao makuu ya polisi Tabora.

“Tumekupata na tunafanyia kazi, ova” sauti ya upande wa pili ilijibu

“Nimekusoma” alijibu.

♠♠♠

Kule stesheni, furaha ililipuka, hakuna aliyeamini walipopokea taarifa hiyo kutoka kwenye chumba cha mawasiliano. Mkuu wa polisi mkoa wa Tabora aliruka kwa shangwe haikujalisha kama alikuwa na kitambi kilichomzidi uzito. Alimkumbatia stesheni masta na kupongezana kwa furaha.

“*Thank God,* watu wetu wamepona” alisikika stesheni masta akipiga kelele kwa furaha sana.

Madam S, IGP na waziri wa ulinzi hawakuamini wanachosikia baada ya simu iliyopigwa na Amata kumfikia Madam S kabla hajaondoka katika eneo hilo la makao makuu ya JKT. Kila mmoja alifurahi kwa furaha ya aina yake.

"*Well done* Kamanda Amata" Madam S alisikika akiyatamka hayo maneno.

"*Ok*, tunamshukuru Mungu, sasa kesho asubuhi wote tukutane tuelekee Tabora kwa ndege ya kukodi" waziri alimaliza na wote wakaagana kuelekea walikotoka.

♠ ♠ ♠

Magari ya jeshi yaliondoka kutoka kambi ya Kaliua KJ 320B kuelekea eneo la tukio ili kuwasaidia abiria wale kuwafikisha mjini, usiku kwa usiku amri ilitolewa na kiongozi wa kambi hiyo na kazi ilianza mara moja bila hata kchelewa.

Watu walikuwa ni wengi sana kiasi kwamba ilipelekea wengine kubaki ili gari zingine zije kuwasaidia, vijana wa jeshi la wananchi wa Tanzania walifanya kazi yao vizuri sana na kwa moyo wa kizalendo kuwasaidia abiria wale japo kuwasogeza karibu na stesheni au kuwafikisha kabisa.

Steshen masta wa Tabora aliamuru vibelenge kadhaa kufuatana ili kuona hali ilivyo na ndani ya kimojawapo mlikuwa na mkuu wa polisi wa Tabora, stesheni masta mwenyewe na viongozi wachache wa chama na serikali, wote walitaka kwenda kujionea wenyewe kile kilichotokea.

Wakiwa bado njiani kwa mwendo wa taratibu, kwa mbali waliweza kuona kitu kikubwa kimezuia reli, operetta aliongeza mwanga wa taa yake kubwa na kupiga honi nyingi lakini hakuona dalili ya kitu hicho kuondoka mahali pale, alipunguza mwendo na walipokaribia walikuta ni injini ya treni iliyokuwa ikitoka Kigoma kuja Tabora

*"Oh my God!"* stesheni masta alisikika akisema kwa sauti. Operetta alisimamisha chombo chake na wote wakashuka kuangalia hali hiyo, walikuta injini ile ikiwa imeacha reli na kusimama kando katika mawe wakati lile behewa lilikuwa limeanguka na kuharibika vibaya. Waliteremka, kwa kusaidiwa na kurunzi walizonazo waliweza kulikagua behewa lile na injini ile, hawakukuta madhara katika injini ile ila tu behewa lilikuwa limeharibika vibaya. Baadhi ya polisi waliingia ndani ya injini hiyo kuangalia hiki na kile wakisaidiana na mafundi, katika chumba kimojawapo ndani ya injini hiyo ndimo waligundua mwili wa mzee kasimu usio na uhai, waliutoa na kuuhifadhi vizuri kasha kuupeleka katika kibelenge kile

"Alikuwa operetta wetu mahili sana" stesheni masta alijikuta akisema mwenyewe huku akiuangalia mwili ule, machozi yalimlenga

"Kwa vyovyote atakuwa kafa kishujaa, kwani mwili wake unaoneka umepigwa sana" aliongezea mkuu wa polisi mkoa.

Waliupakia mwili ule katika kibelenge lakini hawakuweza kuendelea na safari kwa kuwa reli ilikuwa

imeharibika vibaya. Kwa uchunguzi wa haraka walioufanya waligundua kuwa reli ile ilikuwa imefunguliwa

"Washenzi hawa walifungua reli!" mmoja wa mafundi alisema kwa sauti

"Ha! Hawa walidhamiria, mpaka wamefungua reli, no hii ni hujuma" Mkuu wa polisi alizungumza hayo huku mkononi mwake akiwa ameshika moja ya nati kubwa zinazotumika kufungia reli hiyo ya kijerumani.

"Tungewapata hawa jamaa leo wangejuta kuzaliwa" mkuu wa polisi alisema kwa hasira

"Unafikiri bado watakuwa kwenye treni iliyobaki?" Stesheni masta aliuliza

"Sio rahisi, hii ni hujuma kabisa lazima walifanya hivi ili kuwaokoa wenzao, lakini dunia ni ndogo tutawatia mkononi" mkuu wa polisi alimjibu stesheni masta. Vijana wa polisi walijaribu kuangalia huku na kule japokuwa ilikuwa ni giza lakini mwanga wa taa kutoka katika kibelenge kile uliwawezesha kuona vizuri, polisi mmoja alipiga hatua chache pale mbele akaona kitu kama karatasi ndogo iliyokuwa ikisukwasukwa na upepo mdogo uliokuwa ukivuma eneo hilo, akakitazama akataka kukiokota lakini akaona ni upuuzi akaamua kuondoka zake. Walirudi katika kibelenge kile lakini askari wane walibaki kwa ajili ya ulinzi lakini pia walijua wahujumu wale wangeweza kurudi hasa kufuata mafuta.

♠♠♠

Kamanda Amata, alisimama pembeni akiliangalia zoezi zima linavyoendelea la kuwahamisha abiria wale kwa kutumia magari ya jeshi.

“Kamanda, asante kwa kazi, wewe waweza kwenda sisi tutamalizia, na ulinzi tutaimarisha” polisi mmoja alimwambia Amata.

“Hamna shida, lakini nasikitika kuwakosa wale washenzi japokuwa mmoja wao kajiua mwenyewe, sasa hatujui walikuwa wangapi” Amata alimjibu yule polisi

“Hawa jamaa hata mi sijui walikuwa wangapi, nahisi ni yuleyule mmoja” yule polisi alitoa jibu na hisia zake

“Kama ni yule peke yake basi! Lakini sidhani, lazima wako wengine au lazima ana mtandao mkubwa, usijali afande” Amata alimaliza na kuondoka eneo lile mpaka kwenye gari mojawapo la kijeshi aina ya *MAN* ililokuwa limeegesha hapo likipakia baadhi ya abiria.
Kichwa kilimzunguka Amata, hakutaka kukubaliana na wazo lake kuwa mle ndani kulikuwa na jambazi mmoja tu, kwake kama mzoefu wa kazi ile alijuwa wazi lazima watakua kikundi ama ndaniya treni ile au nje yake, alimfikiria sana Isabel ambaye muda huo alikimbizwa hospitali ili kuokoa maisha yake kwa kuwa alijua wazi kuwa ni yeye pekee anayeweza kutoa mwanga wa tukio zima. Amata alitoa karanga zake na kuanza kurushia mojamoja kinywani mwake huku akiwaza ili na lile, moyoni akiomba na kusali Isabel apone ili azungumze naye machache ‘watakuwa washapata ile memory card?’alijiuliza, mara kwa mara alipofikiria juu ya

Isabel alishtuka kwa kuwa hakuwa na uhakika kama atamkuta mzima alijua wazi kuwa kama wale majambazi wana mtandao mkubwa haitakuwa kazi kugundu Isabel alipo 'lakini wamfuate wa nini wakati washapata wanachotaka' alijiwazia 'mh naomba asife' alijiomba mwenyewe na hapo alijikuta anaingiwa na shauku ya kumuona Isabel japo asikie neno moja kutoka kwake labda lintampa muelekeo wa nini cha kufanya.

"Walikuwa watatu bwana we hukuwaona vizuri" baadhi ya vijana abiria walikuwa wakibishana, Amata alijiunga nao katika mazungumzo yao.

"Yule *tall* sura yake sio ngeni kabisa, kama namuonaona madukani pale Mwanga sokoni au itakuwa namfananisha labda" mwingine aliongezea. Amata alivutiwa na mazungumzo hayo alitulia kimya akijifanya kuchocheachochea vikuni kwenye ule moto uliokuwa ukiwaka taratibu ili kuwapa joto usiku ule.
Baada ya mazungumzo yale marefu Amata alikuwa amehifadhi vitu fulanifulani kichwani mwake ili labda itakapobidi vitamsaidia katika upelelezi wake.

Kufumba na kufumbua abiria wote walikuwa wameondoshwa eneo lile, askari wachache walibaki kulinda mabehewa yale na mizigo ya watu. Amata alitazama saa yake tayari ilikuwa inakaribia saa kumi na moja alfajiri, kichwa chake bado kilikuwa kinawazua mengi kikitoa hili na kuweka lile, moyo wake haukuridhika hasa alipomkumbuka Mandi jinsi alivyojiua kwa mbinu ya kijinga namna ile, alijua wazo

kuwa wapo wenzake lakini aliumiza kichwa jinsi gain ya kupata ukweli *'mpango hasi'* alikumbuka neno hili alilotumiwa na Isabel kupitia facebook, Amata alipenda ajue hasa undani wa mpango huo ni nini. Alitamani kama ni upelelezi basi akabidhiwe yeye hilo faili kwani alitaka kulipa kisasi cha kuumizwa Isabel.

# 5

MWILI wa Koplo Kibona ulikuwa umehifadhiwa vizuri kabisa katika sanduku la kisasa liliofunikwa kwa bendera ya polisi, maafisa wa jeshi hilo waliovalia nadhifu kabisa walikuwa wamesimama kwa mstari ulionyooka vizuri na upande mwingine kulikuwa na waombolezaji wengine. Kasisi alipomaliza ibada ya marehemu, vijana sita waliovaria nadhifu vazi la kipolisi walisoge karibu na sanduku lile kwa ukakamavu wa hali ya juu mara ilipigwa buluji maalumu ya kazi hiyo kabla ya kushusha sanduku lile kaburini. Jeshi la polisi liliamua kumzika kiheshima kwa sababu amekufa akiwa katika harakati za kulilinda taifa, baada ya buluji ile kumalizika zilipigwa risasi kadhaa hewani kisha sanduku lile lilishushwa taratibu kaburini.

Amata alisimama kwa mbali akiwa ndani ya suti yake nyeusi iliyomkaa vizuri, pembeni yake alikuwa na Madam S wakifuatilia kwa karibu kabisa matukio yote ya mazishi hayo.

Muda si mrefu shughuli ilikamilika na watu kuanza kutawanyika wengine wakienda kumpa pole mjane wa marehemu.

Isabel alihifadhiwa katika chumba maalum chenye mitambo tiba ya hali ya juu iliyomsaidia kupumua na mingine ikisoma mapigo ya moyo wake jinsi yanavyoendelea, Isabel alilala kimya katika kitanda kile chenye shuka safi lenye maandishi ya buluu yaliyosomeka *MSD*, hakuwa hata anatikisa mkono wla kupepesa macho alitulia kabisa, mara kwa mara muuguzi alikuja kumuona maendeleo yake huku akiandika vitu fulanifulani katika faili lililopo karibu kabisa na kitanda hicho

"Mgonjwa anaendeleaje?"sauti ilimuuliza kutoka nyuma ya kichwa chake, yule muuguzi alistuka sana alijua labda ni mzuka. Kamanda Amata alitabasamu hasa alipogundua kuwa muuguzi yule kapata mshtuko kwa hilo.

"Anaendelea vizuri, ila bado hajarudiwa na fahamu" Muuguzi alijibu kwa utulivu. Amata alilisogelea faili na kulisoma harakaharaka japokuwa watu huamini kuwa muandiko wa daktari ni mgumu kusoma lakini kwa Amata haikuwa hivyo. Alielewa moja kwa moja yaliyoandikwa, Isabel alivunjika mbavu nne za kulia inaonekana alipigwa sana kwa mateke na kitu kigumu sehemu za mbavu, amekutikana na majeraha ya kichwani, fuvu lake limepata shida kidogo kadiri ya uchunguzi imeoneka Isabel alijigonga vibaya kwa paji lake la uso hivyo kusababisha majeraha eneo hilo, damu nyingi imepotea hasa kutokana na majereha aliyoyapata, mkono wake wa kulia

umevunjika hivyo alikuwa tayari amefungwa muogo ‘POP’.

Amata alimwangalia Isabel kwa uchungu sana machozi yalitaka kumtoka lakini hakuruhusu hali hiyo itokee. Mitambo mingi ya kidijitali iliyomzunguka Isabel ilikuwa ikitoa ushirikiano wa hali ya juu kuhakikisha mambo hayataharibika, aliporidhika alimuaga yule muuguzi na kuondoka zake.

♠ ♠ ♠

Kamanda Amata aliketi kwa utulivu kabisa juu ya kiti chake cha kunesanesa akishikashika magazeti ya siku hiyo ili aone chochote kilichandikwa, kila gazeti liliandika habari hiyo kwa manjonjo kweli kweli ili mradi kuvutia wasomaji *‘Majambazi yavamia Treni’* mojawapo liliandika, *‘Polisi auawa ndani ya Treni’* lingine liliandika hivo *‘Treni yatekwa, wawili wauawa akiwemo Polisi’.* Amata alipitia yote hayo na hakuona jipya lililokuwemo zaidi ya habari za kubuni.

“Boss!” sauti ya kike ilimstua Amata akiwa amezama katika moja yha magazeti hayo. Alikuwa ni Gina aliyesimama kaegemea mlango wa kuingia ofisini kwa Amata

“Unatamani kama ungekuwepo eti!?” Gina alimtupia swali Amata. Amata alimuangalia na kutoa tabasamu pana kisha akazama tena katika gazeti hilo.

“Boss!” Gina aliita tena

“Nimekwambia mara nyingi usiniite Boss, we husikii” Amata alimwambia Gina katibu muhtasi wake

“Oh nilisahau, samahani Mr Amata” Gina alijisahihisha na kusogea karibu na meza ile huku akiwa na faili mkononi mwake, Amata alikunja gazeti lile na kuliweka pembeni.

“Nipe ripoti mrembo” Amata alimwambia Gina. Gina akiwa antazama dokumenti fulanifulani katika faili lile alikuwa akimueleza Amata taarifa mbalimbali za kazi alizomuachia lakini wakati huo Amata mawazo yote yalikuwa hayapo hapo alifikiri tu kama angekuwa *‘Mungu’* angemponya Isabel ili ajue nini kilitokea katika mkasa ule wa jana usiku.

“Mr Amata, inaonekana haupo kabisa hapa kimawazo, au hiyo habari imeshakutia kiwewe, tayari unatamani kuanza fujo zako” Gina aliongea kwa hamaki kidogo.

“Ah Gina, unajuaje? Kama waniletee mzigo niufaulishe” alimueleza Gina huku akiwa anacheka kiutani, akatoa karanga zake mfukoni na kula moja moja. Kamanda Amata alipenda sana kutembea na karanga mfukoni tangu utoto wake alipokuwa shule ya msingi Ukonga mpaka ukubwani, tabia hii imepigiwa kelele na watu wengi akiwemo marehemu mama yake lakini alishindwa kuiacha.

### WIZARA YA MAMBO YA NDANI

Kikao cha watu wanne kiliendelea katika moja ya ofisi za jengo la wizara ya mambo ya ndani karibu kabisa na barabara ya Ohio, makubaliano yalikuwa ni

magumu kwa jinsi kila mtu alivyofikiri juu ya tukio hilo.

“Hii ni kazi ya polisi tuwaachie wenyewe” IGP Makabayo, alilieleza jopo hilo

“Hatukatai usemalo lakini linavyoonekana tatizo lenyewe unafikiri polisi wataliweza kadiri ya mipaka yao ya kazi?” Madam S aling’aka kwa kuwa yeye anahusika na usalama wa Taifa moja kwa moja.

“Tuna kitengo cha CID, kazi haiwezi kutushinda hata kidogo” IGP aliongeza

“Ok! Nafikiri hii ni kazi yetu sote, kulinda usalama wa nchi vinatuhusu sisi sote. Haina haja ya kugombana. Tuwaachie jukumu hilo vijana wetu wa polisi walishughulikie, wakishindwa tutaona kwa pamoja tufanye nini” Waziri wa mambo ya ndani alipitisha uamuzi wake.

“Sikatai unalosema mheshimiwa lakini tangalie tunachokifanya tusije kulaumiana baadae” Madam S aliliambia jopo huku akiwa amesimama. Madam S alishaliona swala lile kuwa polisi kama wao peke yao hawaliwezi kwa jinsi lilivyo katika mapana yake, na alishangazwa jinsi ambavyo IGP alivyolitaka swala lile libaki mikononi mwa polisi, Madam S alikubali kwa shingo upande lakini atafanyeje, hakuna jinsi. Kikao kiliendelea na kuona mipango ya hapa na pale.

Maagizo yalitolewa kwa pande zote mbili jinsi ya kufanya kazi hiyo.

“Ok sasa baada ya hapo, nitaomba mambo yafuatayo yafuatwe, moja, hakikisheni yule binti

anawekwa chini ya ulinzi asiruhusiwe mtu awaye yote kumuona kwa sasa bila kibali cha polisi, pili, Madam S mueleze Kamanda Amata juu ya hili na mueleze kwa sasa asijihusishe kabisa na swala hili mpaka atakapopata taarifa tofauti. Nafikiri tumeelewana, jinsi ya kufanya kazi IGP unajua kuwapanga watu wako. Asanteni." Waziri alimaliza na kuagana na wajumbe.

Madam S alibeba faili lake na kutoka nje bila kuaga, hakupenda wala kufurahia juu ya uamuzi uliotolewa na wizara, kwake hakuingia hakilini kabisa.

♠ ♠ ♠

Amata alipata taarifa yote ya kikao kutoka kwa Madam S, hakuwa na la kufanya isipokuwa ni kukubaliana na utaratibu uliotolewa lakini moyoni mwake alikuwa na shauku sana ya kutaka kujua hasa kiini na mpango mzima wa mkasa huu. Alitulia juu ya kiti kile huku akimwangalia Madam S kama mtu ambaye hajawahi kumuona katika maisha yake

"Hii ndiyo shida ya polisi" Amata alimwambia Madam S, ambaye wakati huo alikuwa anaperuzi mambo Fulani katika kompyuta yake pale mezani, sauti hiyo ya Amata ilimgutusha kidogo maana alishasahau kama ofisini mle hakuwa pekeyake.

"Usijali Kamanda, kwa kuwa mambo yenyewe ndiyo yanaanza wakizidiwa watatutafuta" Madam S alijibu huku akicheka kwa kebehi.

"Nina wasiwasi sana juu ya hili, na usalama wa yule binti" Amata aliongeza huku akitikisa kichwa

chake na kupepesa macho kuzunguka ukuta uliopambwa kwa kalenda nzuri na picha moja kubwa ya Madam S alipokuwa chuoni huko Canbella. Alipiga picha hiyo na wasichana wenzake kutoka nchi mbalimbali, Amata aliiendea na kuitoa pale ukutani

“Kamanda! Nini sasa unatoa picha za watu ukutani bila kuomba?” Madam S aliongea huku akinyanyuka na kumfuata Amata.

“Subiri bibi” Amata alipenda kumuita Madam S bibi, kwa kuwa umri wake ulikuwa umekwenda sana lakini bidii yake kazini iliishawishi serikali kumuongezea muda kabla ya kustahafu.

“Hii picha imekaa vibaya au wewe hujagundua?” Amata alimwambia madam S huku akikimbilia upande wa pili wa ofisi hiyo kubwa, kitu kidogo mfano wa kifungo kikaanguka kutoka katika picha hiyo, Amata alisimama na kukiangalia kidubwasha hiko. Madam S alikitazama na kushika kichwa, akakiokota, kilikuwa ni kinasa sauti, kifaa kilichonasa sauti na kupeleka sehemu fulani wasiyoijua. Mwanamama huyo alirudi na kuketi katika kiti chake akitazamana na Amata, hakuna aliyemsemesha mwenzake. Amata akairudisha ile picha pale ukutani na kumpa madam S kile kidubwasha. Naye akakichukua na kukivunjavunja, kisha akajitupia kwenye kiti chake. Akamwangalia Amata na kumuona kuwa ni mtu wa ajabu sana, alijiuliza kidubwasha hiko kimekaa pale kwa muda gani, hakupata jibu, kama waliweka ili kupata siri za ofisi je; hapo alichanganyikiwa kabisa.

“Umejuaje kuwa hiyo picha ilikaa vibaya” Madam S alimtupia swali Amata

“Nilipokuja wiki iliyopita hii picha haikuwa hivi, leo nimeona imeyumba kidogo” Amata alijibu

*“Jesus!”* Madam S alinong’ona, kwa jibu la Amata aligundua kuwa kidubwasha hiko kilipachikwa karibu wiki moja nzima hapo ukutani.

“Haya! Nambie kilichokuleta, nilishakwambia usije hapa bila kuniambia” Madam S alimueleza Amata kwa utani wa mtu na mtoto wake

“Mama nina njaa nimekuja unipe *lunch*” Amata alijibu kwa kudeka

“Gina yuko wapi?” Madam S alimuuliza Amata

“Nimempa kazi moja hivi ofisini, kuna mzigo wa kuufaulisha kutoka bandari kavu ndiyo anatengeneza mazingira” Amata alijibu.

Baada ya mazungumzo mafupi waliteremka ngazi na kuliendea gari la Madam S, walipolikaribia Amata alimshika mkono Madam S kama ishara ya kutofungua mlango wa gari hiyo. Walitoka na kuchukua tax mpaka mgahawa wa Steers na kuketi, juice mbili zikawa mezani na sambusa kadhaa.

Mara wateja walokuwa hapo walinyanyuka mmoja mmoja na kuingia ndani ya mgahawa huo wote walisimama mbele ya luninga kubwa wakitazama habari fulani, Madam S na Amata walibaki palepale lakini hawakujua kwa nini watu wale wamevutiwa na habari hiyo, Amata alitaka kunyanyuka kuelekea huko

ili ajue kilichojiri, Madam S akamvuta mkono na kumrudisha kitini.

“Tumia akili, sio unakurupuka tu!” alimwambia Amata ambaye wakati huo alikuwa akitoa kicheko cha kitoto. Madam S alitoa simu yake kubwa mkobani na kuiwasha simu ile ilikuwa na uwezo wa kukamata matangazo ya televisheni ya kidigitali bila chenga, akabofya vitufe fulani fulani kisha akatulia kuangalia

*“What? Jesus!”* Madam S alipata mshtuko na kumpa simu ile Amata, wote walihamanika na taarifa ile

“IGP?! Ameuawa!!” walijikuta wote wakinyanyuka kwa pamoja na kuacha juice zao, lakini baada ya hatua mbili tatu, Amata akarudi mezani na kupiga *tarumbeta* juice zote mbili na kisha kuondoka eneo lile.

♠ ♠ ♠

Mwili wa IGP, Bw Makabayo, mkuu wa jeshi la polisi Tanzania ulikuwa umelala juu ya machela ukiwa umefunikwa na kitambaa cheupe mpaka kifuani na kuruhusu sehemu ya juu kuonekana. Madam S akiwa anafuta machozi alishikwa bega na Kamanda Amata na kumuegemeza kwake akimbembeleza. Viongozi mbali mbali walifika mchana huo katika chumba cha kuhifadhia maiti cha hospitali ya rufaa ya Muhimbili kushuhudia walichokisikia, hawakuamini lakini ukweli ulikuwa ndiyo huo.

***Ilikuwaje?***

IGP alikuwa katika safari ya kikazi akitoka makao makuu ya jeshi la polisi, jengo la wizara ya mambo ya ndani na kuelekea Lumo Kigilagila kufungua kituo kidogo cha polisi katika mtaa huo, msafara wake ulikuwa na gari mbili tu, mbele ilitangulia *golf* na yeye mwenyewe alikuwa katika Toyota Prado iliyokuja nyuma, walipoiacha barabra ya Nyerere na kuingia barabara ya Jet, kwa mwendo wa kawaida walivipita viwanda eneo hilo kuuzunguka uwanja wa ndege, wakiwa katika kona ya mwisho walipishana na gari nyingine ailiyokuwa ikiyumba njia nzima kiasi kwamba ilibidi gari zingine zisimame. Msafara wa IGP haukusimama bali ulipikwa upande wa kulia hapondipo iliposhuhudiwa kioo cha Prado kikitawanyika nakumwagika kama chumvi, gari iliacha njia na kuingia kwenye mtaro wa maji uliojengwa pembeni mwa barabara hiyo. Polisi waliokuwa kwenye golf walishuka haraka na bunduki mkononi walipofika hapo tayari walikuta IGP hana uhai tena, bila kuchelewa waliwabeba katika golf na kurudi mjini.

Majambazi watatu waliokuwa katika Land Rover 110 waliifanya kazi yao kwa umakini na kasi kama walivyoelekezwa, kwa kutumia bastola maalum ya kizamani *PSS silent pistol*, bastola ya kirussia iliyotengenezwa 1983, inaonekana mtumiaji alifuzu

mafunzo maalum ya kuitumia bastola hiyo inayofanya kazi yake kwa ukimya wa hali ya juu.

♠ ♠ ♠

Hakuna aliyeamini kilichotokea kila mmoja alijiuliza kwa nini IGP Makabayo kukumbwa na umauti katika jinsi ile, kama ilivyo ada kwa jeshi la polisi, mara moja walianza kufanya uchunguzi wa tukio lile, walifuatilia nyendo za gari lile ambalo si mpita njia wala aliye dukani aliiona namba yake kwa jinsi lilivyokuwa mwendo wa kasi, walijaribu kulifukuzia lakini walichoambulia ni kulikuta Tazara karibu na kampuni ya Azam likiwa limeegeshwa pembeni na hakuna mtu ndani yake. Baada ya kufanya yote ambayo kanuni zao zinawataka walilivuta na kulipeleka kituo cha polisi kati na msako wa kuwasaka wauaji ulianza.

Walijaribu kuangalia gari ile ni mali ya nani baada ya kuwasiliana na wakala husika wa magari hayo CMC, jibu walilolipata liliwaridhisha kidogo, lilikuwa ni mali ya mburushi mmoja aliyekuwa akiishi huko Mbalali kwenye mashamba ya mpunga, lakini jambo moja likawachanganya, katika kadi kivuli ya gari hiyo kulikuwa na jina la mtu mwingine kabisa, walipowasiliana na TRA wakapata jibu kuwa hilo gari lilishauzwa na mmiliki alishabadilishwa katika kadi, kadi ilionesha gari ni ya Bw. Costantino Chawala. Baada ya kuchunguza kwa kina hata huyo Costantino Chawala alishafariki siku nyingi nyuma.

# 6

## Bujumbura – Burundi

KIKAO cha watu wachache kilifanyika katika moja ya vyumba maalum ndani ya mgahawa wa Amahoro *(Amahoro Cafe)*, uliopo katikati ya viunga vya jiji la Bujumbura. Maelewano yalikuwa tete. Msemaji mkuu wa kikao hicho, Madam Rose alionekana wazi kukasirishwa na yaliyotokea katika *mission* yao hiyo, Mpango Hasi.

“Kweli kabisa, niliwaamini sana lakini inaonekana mna uzembe wa hali ya juu sana” Madam Rose aliongea kwa hasira huku akipigapiga meza yake, akawatazama vijana wale waliokaa viti vya mbele tu ya meza yake, “Hamjui kazi? Au uzembe tu?” aliwatupia maswali ya haraka haraka. Wote walionekana kushindwa maswali hayo machache lakini yenye fedheha kwao.

“Jomse!” Madam aliita “Hata wewe ninayekuamini na kukuweka mstari wa mbele, leo umeniangusha namna hii!”

“Hapana Madam Rose” Jomse alisema

“Hapana nini; wakati hali yenyewe inajidhihirisha?” Madam Rose aliendelea kuongea kwa hasira. Ukumbi wote ulikuwa kimya kabisa, hamna

aliyethubutu kufungua kinywa chake maana walijua moto utakaomuwakia kutoka kwa Madam Rose.

“Tupo hapa, hata hatujui Mandi yuko wapi, kama kakamatwa; na kupata mateso si atatoa siri yote! Hilo la kwanza, la pili, *Memory Card*, wanaume wapumbavu nyie” Madam Rose aliongea huku akitembea kutoka kona moja kwenda nyingine “Mmepoteza siri yote, eti msichana! Msichana mdogo, anawashinda piga risasi moja ya kichwa mengine yatafuata” alinyamaza kidogo na kuinua bilauri yake iliyojaa maji na kuoiga mafunda kadhaa kisha akaitua mezani. Frank Sabatie akamwangalia mwanamke yule jasiri mwenye maamuzi yasiyopingwa jinsi alivyotingwa kwa mawazo na hofu, mwanamke mwanajeshi aliyekuwa kiongozi wa battalion moja ya katika vita vya msituni, alivuta faili lake na kulifungua kurasa kadhaa.

“Ok! Madama tulia kitini,” alimweleza Madama Rose ambaye alionekana kutokujua nini champasa kutenda katika hili.

“Tuna wasiwasi kuwa siri yetu imeshavuja katika serikali ya Tanzania” Frank alizungumza kwa upole huku akiwa kaikutanisha mikono yake pamoja na kuiegemeza juu ya meza hiyo “Tuko matatani, Watanzania hawana mchezo hata siku moja, kila raia anailinda nchi yake, kutokana na hili kutukia tunapaswa kutumia nguvu kurekebisha makosa.” Jomse na Tonton walikuwa wameketi kimya wakiwasikiliza mabosi wao, hakuna aliyeongea lolote.

“Sasa hivi, plan B, maandalizi ya mpango hasi yameshaanza matekelezo, kwa kuwa ninyi mlivyoleta uzembe tuliunda kikosi kazi kingine cha watu wanne kutoka nchi za Magharibi, kazi ya kwanza tayari imekamilika siku nne zilizopita, na ya pili si muda mrefu itakuwa tayari. Sasa ninyi tunawageuzia kibao, lazima muende Tanzania mkahakikishe yule msichana anauawa kabla hajatamka chochote, fanyeni kila hila, sistoshe hakikisheni mnarudi hapa na ile memory card hapa” Frank aliongea kwa msisitizo swala hilo. Tonton na Jomse walibaki kumwangalia tu wakisubiri amri kutoka kwa wakuu hao, wakuu wa kikosi kazi.

Kila mtu alikuwa kachanganyikiwa kwa jinsi yake, Madam Rose alitakiwa kupeleka taarifa ya *mission* yote baada ya siku chache kwenye kikao cha ma*top*, huko Geneva alishindwa afanyeje baada ya vijana hao kuvuruga katika utendaji, *missing in action!*

♠ ♠ ♠

Jomse aliishusha sigara yake kutoka kinywani na kuikandamiza katika kidubwasha maalumu kwa kazi hiyo kilichowekwa mezani hapo, akachukua bilauri yake iliyojaa pombe aina ya *Primus* na kujimiminia tumboni kabla hajashusha bilauri ile kwa nguvu hata kupasua kitako chake na kufuatiwa na sonyo kali ambalo lilimfanya kila mtu kati mgahawa huo kugeuka. Alinyanyuka na kuchukua suitcase yake, kisha taratibu aliivuta kuelekea barabarani ambako alichukua tax na kupotelea mjini.

Dakika kadhaa, Jomse alikuwa ameingia katika uwanja wa ndege wa kimataifa Bujumbura, tayari kwa safari yake ya kuelekea kunako Bandari salama *'Dar es salaam'*. Safari hii walijua kabisa kuwa wanaweza kushtukiwa hivyo Frank aliwapanga kuondoka kila mmoja kwa staili yake na kuingia Dar es salaam kwa staili yake ili wasijulikane. Walishapewa tahadhari kuwa wawe makini na makachero wa Tanzania na Watanzania wenyewe *'trust no one'*, mara kwa mara sentensi hii ilijirudia kinywani mwa Jomse. Jomse alikuwa na uchungu uliochanganyika na hasira hasa kwa kulaumiwa na Madam Rose juu ya makosa waliyoyafanya, lakini kilichomuumiza kichwa zaidi ni kuhusu Mandi na Isabel, hakujua kabisa kuwa swahiba wao Mandi alikwishakuwa marehemu.

Akiwa ameketi sawia na kujifunga mkanda katika ndege hiyo ya shirika la ndege la Afrika ya Kusini *'SA Airline'*, alikuwa akijisomea gazeti la *Daily Mail* alilolikuta kwenye kijimeza kidogo karibu yake, *'Tanzania's Inspector General of Police died on car accident'* , habari iliyokuwa juu katika kurasa ya habari za kimataifa, Jomse aliisoma kwa umakini mkubwa sana na akaelewa kuwa kazi imeanza.

## *Dar es salaam*
## *Saa sita baadae*

*'Valley View Hotel, chumba namba 407'*, Tonton aliikunja karatasi ile mara baada ya kuisoma, kisha

kuitia mfukoni. Aliishusa miwani yake myeusi na kuifuta vumbi kidogo, kisha akairudisha tena usoni pake. Mtu mmoja alipita nyuma yake na kumpiga kibega kisha kumuomba samahani kwa tukio lile, Tonton alinyanyua *briefcase* yake na kuelekea kule alikoelekea yule kijana. Ilikuwa ni *trick* ya utambulisho kati yao.

"Kila kitu kipo katika mstari" Kijana mmoja alimueleza Ton wakiwa ndani ya Tax, Ton hakujibu kitu alinyamaza tu.

Tax ailifika mitaa ya Jangwani, Ton alilipia Tax hiyo na kuisogelea hotel iliyokuwa akitazamana nayo, juu ya lango kuu kwenye *canopy* kulikuwa na maandishi makubwa yaliyosomaeka Valley View Hotel, alipiga hatua chache na kuifikia meza ya mapokezi.

"Tonton, bila shaka!" mdada wa mapokezi alimwambia Ton. Ton alitikisa kichwa kuonesha ishara ya kukubali. Alipewa funguo zake, na msaidizi akamsaidia *suitcase* yake kuelekea chumbani. Ton aliweka vitu vyake sawa chumbani humo, akajimwagia maji na kujilaza akisubiri muda ufike ili awasiliane na swahiba wake tayri kuanza kazi waliyotumwa.

♠♠♠

Polisi katika Uwanja wa Ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere walikuwa makini kuchunguza kila ashukae na kuingia nchini, ukaguzi wa kina ulifanyika hasa baada ya kupata tetesi ya mpango hasi uliopangwa na vikundi vya waasi kutoka nchi jirani.

Waliamuriwa kumkamata yeyote atakayedhaniwa ili kumhoji kwa kina, haikuwa kazi rahisi maana watu wengi kutoka nchi mbalimbali walifikia uwanja huo.
Majira ya saa kumi na moja na nusu jioni ndege ya shirika la ndege la Tanzania iliikanyaga ardhi yake ya Dar es salaam na kujiegesha sawia kabisa katika ngazi za kuteremkia abiria. Watu walianza kuteremka mmoja baada ya mwingine, vyombo vya usalama vilikuwa makini kuangalia wote washukao katika ndege hiyo. Dakika chache walikuwa wamekwisha na ndipo aliposhuka mkuu wa upelelezi wa makosa ya jinai DCI Salila, akiwa na katibu wake pamoja na watu watatu waliomsindikiza, waliteremka ngazi za ndege hiyo kwa umakini, alipoikanyaga ardhi tu kitu kisichotegemewa kilitokea, DCI Salila alionekana kujishika kifua kwa mikono yake miwili na kuanguka chini, wasaidizi wake walimuwahi kumdaka lakini walichelewa. Walipomuinua tayari alikuwa marehemu Salila, risasi iliyopita upande wa kushoto wa kifua chake iliutoa uhai wake kwa wepesi sana. Damu ilichafua suti yake hasa upande wa pili ilipotokea risasi hiyo. Gari ya wagonjwa iliingia haraka uwanjani hapo na kutoa huduma iliyostahili. Tafrani kubwa ilizuka uwanjani hapo, polisi walitanda haraka eneo la uwanja wa ndege kuhakikisha wanamtia nguvuni aliyetenda hayo. Lakini uwingi wa watu haikuwa rahisi kufanikisha hilo.

Joseph Msengiyumva au 'Jomse' kwa jina bandia, akiwa ndani ya mavazi ya shirika la *DAHACO*

alisitazama tukio zima baada ya kuanguka kwa DCI Salila, huku bastola yake maalum ya kijasusi akiwa ameifutika vizuri uvunguni mwa gari maalumu ya kuvutia ngazi ambazo hutumika kwa kushukia abiria katika ndege kubwa kama ile, bastola tulivu isiyotoa kelele, ndogo inayotosha kukaa kwenye kiganja cha mkono. Hakuna aliyemdhania, kama ni yeye aliyetekeleza mauaji yale. Alisimama mara moja kutoka pale alipojifanya anaangalia kitu Fulani kwenye gurudumu ya gari hiyo na kwa muda huo ndipo alipotekeleza kazi hiyo kwa ufundi wa hali ya juu kabisa. Alitoka pale alipo na kusogea jirani na tukio kwa ajili ya kutoa msaada.

"Kijana, tunaomba msaada wa haraka." Wasaidizi wa Salila waliomba msaada kutoka kwa vijana wa *DAHACO* akiwemo Jomse. Baada ya kumaliza kutoa msaada huo na kuhakikisha kuwa mtu yule tayari ni marehemu alirudi na kuchukua kale kagari akaondoka na kuelekea upande wa pili. Balaa!

♠ ♠ ♠

Inspekta Simbeye alijikuna kichwa chake kana kwamba kulikuwa na chawa anayemsumbua. Lakini la, ni katika kuchanganyikiwa tu na mambo yanayomzunguka katika siku hizo. Taarifa juu ya kifo cha DCI Salila, kilizidi kumzeesha kitini hapo, alijikuta akiongea mwenyewe ofisini huku kaishika bastola yake akiitazama tazama. Hakujua hasa ni kitu gani anataka kufanya. Wakati bado machungu ya kifo cha IGP

Makabayo hayajafutika katika mioyo ya watu, sasa wanapokea kifo kingine cha mtu wa juu katika medani ya usalama hapa nchini. *'Lazima kuna mchezo unaofanyika'* alijiwazia huku akiwa kasimama dirishani na kuangalia nje, kijasho chembamba kilimvuja makwapani na kumfanya kutota kiasi Fulani.
Aliinua simu iliyopo mezani hapo na kuzungusha namba fulanifulani kisha kuweka sikioni kidubwasha hiko cha kusikilizia.

"Nini kinaendelea hapo?" aliuliza.

*"Hatujafanikiwa kumkamata muuaji, lakini watu kadhaa tunao kwa mahojiano"* sauti ya upande wa pili ilijibu.

"Muwe makini na kazi yenu, msipoangalia huyo muuaji atawatoroka na ninyi mkiwa hapo hapo" Simbeye alitoa maagizo.

*"Sawa mkuu, tumekupata"* ilijibu sauti ya upande wa pili.

Inspekta Simbeye alishusha pumzi na kutoka nje ya ofisi yake, shughuli za watu ziliendelea kama kawaida kana kwamba hakuna lolote lililotokea la kuhatarisha amani ya nchi. Akiwa na karatasi mkononi lililomtaka kwa muda mfupi awe amefika katika makao makuu ya polisi pale jingo la wizara ya mambo ya ndani, Simbeye alijikuta anzidi kupata wakati mgumu, ukizingatia dhamana ya ulinzi wa mji huu ipo mikononi mwake. Alirudi ofini na baada ya muda mfupi alielekea kuitikia wito.

# 7

ISABEL aliamka kutoka katika usingizi mzito uliojalizwa ndoto mbaya na nzuri. Macho yake yalijaribu kupambana na nuru ya taa kubwa nyeupe iliyokuwa kiwaka juu tu ya uso wake, alifumbafumba macho na kujaribu kujikinga kwa mikono yake.

Muuguzi wa zamu alifika moja kwa moja na kufungua pazia lile la plastiki na kuingia ndani, kwanza alizimisha lile taa na kumuacha kwa muda. Baada ya dakika kadhaa alimsaidia kukaa vizuri, Isabel alikuwa akijishika ubavuni mwake mara kwa mara kutokana na mvunjiko wa mbavu zake kadhaa. Alijaribu kujinyanyua lakini ilikuwa ni ngumu sana kwake.

“Endelea kupumzika Isabel” muuguzi alimueleza kwa sauti ya upole kabisa.

“Samahani, nesi, nipo wapi?” Isabel aliuliza kwa tabu kidogo

“Hapa ni Hospitali ya Muhimbili” Nesi alimjibu

“Muhimbili! Nimefikaje hapa na lini?” Isabel alizidi kuchanganyikiwa na kumtupia maswali muuguzi yule.

“Ulileta hapa wiki mbili zilizopita, ulipata matatizo ulipokuwa safarini kwa treni” Muuguzi alijibu huku akiwa ameketi katika kitanda kilekile alicholalia Isabel. Isabel aliposikia juu ya treni picha ilirudi na kumbukumbu zikaanza kujirejesha ubongoni taratibu.

“Mandi!” alianza kujisemea taratibu huku aking’ata kidole kimoja cha mkono wake. Mara nyingi alitamka jina hilo *‘Mandi’*.

“Njaa!” alimwambia Muuguzi. Mara tu uji ulileta na akaanza kuubugia kwa fujo sana. Baada ya kuufakamia uji ule kwa fujo, hali yake ya tumbo haikuwa nzuri alisikia kichefuchefu cha hali ya juu, aliomba msaada ka muuguzi na moja kwa moja aliongozwa maliwato.

Kitu kidogo cheusi kilionekana katika matapishi ya Isabel. Alikitazama kwa makini hakujua mara moja ni kitu gani, baada ya kuvuta kumbukumbu ndipo akakumbuka ile *memory card* aliyoimeza kule kwenye treni *‘Nilijua washaichukua!’* akawaza. Aliipekua na kuisafisha bombani kisha akaihifadhi vizuri.

Punde si punde Kamanda Amata aliingia katika wodi aliyolazwa Isabel kwa kificho, kwa kuwa alishaambiwa asijihusishe na lolote katika sakata hilo; awaachie polisi, lakini alijiapiza moyoni kuwa ni lazima ahakikishe anapata maelezo yote kutoka kwa Isabel kabla hajayatoa kwa mtu mwingine. Mara ya

mwisho kuja hapo alimuaomba muuguzi kuwa endapo Isabel ataamka tu basi amjulishe mara moja kabla ya mtu mwingine, na ndivyo ilivyokuwa. Akiwa ndani ya kanzu na *baraghash*, huku miguuni kajitupia makubanzi aliingia bila tabu katika wodi hiyo akiwapita polisi waliopo zamu, maana kila aliyeingia katika wodi hiyo ilipaswa kufanyiwa upekuzi wa kina.

"Dakika tano tu tafadhali" WP aliyekuwa jirani ya kitanda cha Isabel alimueleza Amata, ambaye aliingia hapo kama mmoja wa ndugu. Alisimama kando ya kitanda na kumtazama Isabel, Isabel alimtazama Amata lakini hakumtambua kabisa ukizingatia hawajawahi kuonana hata siku moja. Walibaki wakitazamana. Amata alitabasamu, hakuweza kuongea chochote kwani yule WP alikuwa pale, na Amata hakupenda mtu yeyote ajue juu ya mazungumzo yao.

"Hujambo Isabel?" alimsabahi huku akimuinamia pale kitandani

"Sijambo, shikamoo,"

"Marhaba, wajisikiaje sasa?"

"Mungu anasaidia nimeamka. Mbona mi sikufahamu, we ni nani?"

"Huwezi kufahamu wote wanaokuja kukuona. Ila mi ni mgeni uliyemtegemea sana kuonana nae japokuwa humjui hata kwa sura" Amata alimueleza Isabel, lakini ilikuwa ngumu kwake kujitambulisha kwa uwazi kwa kuwa yule WP angeweza kusikia kwa ukaribu na picha *ingeungua*. Lakini Amata alipenda kusikia juu ya tukio lile kutoka kwa Isabel, hakujua

mbinu gani atumie katika kulifanikisha. Aliumiza kichwa kwa kuwa alijua wazi kuwa asipopata habari hiyo muda huo basi polisi wakija wataondoka na Isabel ili akapate hifadhi na kwa mahojiano.

Mungu si Athumani, yule WP alinyanyuka na kuelekea ofisini kwa wauguzi, ni muda huo mfupi ulitosha kwa Amata kutekeleza azma yake. Aliingiza mkono ndani ya kanzu yake na kutoa kitambulisho kidogo ambacho daima huwa hakioneshi hovyo kutokana na unyeti wa kazi yake, akanong'ona.

"Mimi Amata, nilitaka kuongea na wewe lakini naona haiwezekani. Nitashindwa kukusaidia Isabel" alirudisha kile kitambulisho mahali pake kwa haraka. Isabel alishasoma kwa haraka na kuwa na uhakika juu ya mtu huyo. Isabel alitikisa kichwa kuashiria kuwa alimuamini.

"Niitie nesi tafadhali!" Isabel alimuomba Amata, na Amata akafanya hivyo haraka, nesi alifika pale pamoja na yule WP.

"Nini Isabel?" nesi aliuliza

"Najisikia kutapika."

Yule nesi alimshika mkono Isabel na kumsindikiza maliwato, kwa kuwa Isabel alikuwa hana nguvu za kutosha kutembea mwenyewe, WP alikuwa nyuma yao kuhakikisha usalama wa binti huyo.

Baada ya muda kidogo alikuwa akirudishwa kitandani na kabla hajakifikia kitandani alisimama na kujishikia kwenye nguzo iliyo katikati ya wodi hiyo, akihema kwa shida huku kajishika mbavu zake.

“Kaka, tunaomba utusaidie kidogo” WP alimwita Amata kutoa msaada wa kumfikisha Isabel kitandani. Amata alinyanyuka na kwenda kutoa ule msaada. Akataka amnyanyue Isabel, lakini Isabel alikataa akampa mkono amshike, na hapo ndipo Amata alipogundua hila ya Isabel. Kamanda Amata alihisi kama kitu kidogo kigumu kikikandamiza kiganja chake kutoka kile cha Isabel. Alimsaidia Isabel kutembea mpaka kitandani na yeye kubakia na kile kitu mkononi mwake.

Akiwa kitandani Isabel, alimwangalia kijana huyu na kutoa tabasamu pana.

“Naomba nipumzike, sitaki kuongea na mtu” Isabel alimueleza muuguzi, na Amata aliombwa kutoka nje ya wodi ile maalum.

Kwa hatua za haraka haraka Amata aliiendea gari yake *Toyota Altezza* na kujitoma ndani. *Memory card* ndogo ilikuwa kiganjani pake. Aliitazama na kuigeuzageuza kisha akaihifadhi vizuri katika *wallet* yake, na kuondoka kuelekea moja kwa moja nyumbani kwake ili kwanza akajue nini kilichomo ndani ya *card* ile.

♠ ♠ ♠

Ton aliketi kwenye moja ya viti vilivyopo chumbani kwake, akisubiri maelekezo mengine kutoka kwa asiyemjua. Mara kwa mara aliangalia saa yake na kuona muda ulivyokuwa ukikimbia alinyanyuka na

kuangalia dirishani lakini hakuna aliyemuona kuja wala kumjua. Aliketi na kuwasha luninga ndogo chumbani hapo. Mara simu iliita. Aliinyakua na kubofya kitufe cha kusikilizia.

"Halo" aliita (...) "Ok nakuja" aliijibu hiyo sauti ya upande wa pili, akaliendea kabati na kufungua, akatupa jicho lake hapa na pale na kuivuta bastola yake anayoiamini aina ya *Winchester 73*. Akaitia kotini na kufunga mlango nyuma yake. Alishuka taratibu ngazi za jengo hilo na kutokea barabarani. Moja kwa moja akaliendea Marcedec Benz jeusi lililokuwa limeegeshwa eneo hilo.

Ton alikutana na watu wawili asiyowajua garini mle aliwaangalia kwa hadhari kubwa, aliyekuwa nyuma ya usukani akageuka.

"Ton Ton, kutana na Meno ya Mamba" alimueleza Ton huku akimuoneshea kijana mwingine aliyeketi kushoto kwake "na Anaconda," alimalizia kwa kumuonesha mtu wa kiti cha nyuma. Ton alitikisa kichwa kuonesha amekubaliana nao, akawapa mikono.

"Swahiba huyu ni Ton, mtakuwa naye katika ile opereshen, mnatakiwa muifanye kwa umakini na haraka iwezekanavyo, mambo ni mawili tu; apatikane mzima au ikishindikana auawe" alimaliza kauli yake na kuondoa gari. Ton aliitoa bastola yake na kuiweka tayari kwa kazi na wenzake walifanya vivyo hivyo. Gari lile kwa mwendo wa kawaida lilipita mtaa wa Swahili na kuelekea taa za faya kabla ya kupita njia panda hiyo

kuchukua barabara ya Umoja wa Mataifa mpaka Muhimbili.

*"Yupo wodi maalum. Ndani ya chumba hicho ni yeye, muuguzi na msaidizi mmoja,"* sauti nyembamba ya kike ilisikika katika kidubwasha maalum ndani ya gari hilo. Ikatulia kidogo kisha ikaendelea *"nje mlangoni kuna polisi wawili wenye bunduki, muwe makini sana wasilete matatizo, muda mzuri ni jioni ya saa moja mimi nitakuwa nimetoka zamu ataingia mwingine"* kisha sauti ile ilikatika.

"Mmesikia vijana?" yule dereva aliwauliza, wote wakaitikia kwa vichwa kukubali. Yule dereva aliinua mkono wake kuangalia saa ilikuwa saa kumi na mbili jioni, walipopaki gari katika maegesho ya wageni, Ton na wale wawili wakashuka na ile gari ikaondoka.

"Mmoja ataingia kwa muuguzi kwanza wakati wawili watasubiri nje, kisha ataingia mtekaji baadaye wa mwisho atakuwa makini na askari, tutatofautisha dakika mbili kwa mtu wa kwanza na wa pili, halafu sekunde thelathini kwa mtu wa pili na wa tatu" Ton alitoa maelekezo kwa wenzake na kuonekana wako pamoja kisha wakatawanyika na kukubaliana kuanza kazi baada ya kupeana *signal* Fulani.

♠ ♠ ♠

*"Surprise!"* Amata alimwambia Madam S

"*Surprise* ya nini?" madam S alimjibu huku akifunga faili alilokuwa akilipitia.

“Nilishakwambia Kamanda, ukiwa unakuja ofisini kwangu uwe unanipa taarifa” Madam S alimueleza Amata huku akimnyooshea Amata kalamu aliyoishika mkononi.

“Hapana, nimekuja tu kwa dharula, lakini kuna jambo zito sana nataka tuliongee, tukichelewa itakuwa balaa” Amata alimueleza madam S huku akivuta kiti na kuketi, kisha akaendelea “Kuna mpango mchafu, mpango hasi, kutoka nchi jirani kwa ajili yetu”, Madam S aliduwaa kumsikiliza Amata.

“Unasema nini kamanda!?” aliuliza kwa mshangao

“Watu wanataka kufanya mapinduzi, kama ilivyotokea huko nchi za jirani mwaka 1994 ndiyo mpango uliopo unaosukwa na haohao kwa ajili ya Tanzania” Amata alinyamaza na kumwangalia Madam S usoni.

“Mh! Mbona unanitisha na hizo habari, we umepata wapi?” madam S alimtupia swali Amata.

“Isabel” alimjibu

“Isabel?” madam S aliuliza kwa sauti

“Ndiyo, Isabel kanipa taarifa hii” Madam S aliposikia taarifa hiyo alinyanyuka kitini na kuiacha meza yake kisha akampa ishara Amata ya kumfuata. Walitoka nje na kuingia kwenye gari na kuondoka eneo hilo. Breki ilikuwa katika uwanja wa shule ya msingi ya jirani, wakashuka.

“Umenileta huku kufanya nini?” Amata alimuuliza Madam S

“Nataka kukunulia karanga za kukaanga, hupendi?” alimjibu na kumuuliza.
“Ha ha ha ha!” Amata alicheka kwa jibu hilo.

Wakiwa wamesimama katikati ya uwanja wa shule kamanda Amata na Madam S waliabadilishana mawazo.

“Nafikiri hapa ni sehemu salama zaidi kwa maongezi” Madam S alimueleza Amata

“Ndiyo.”

“Ok, niambiye hiyo habari na mpango wenyewe ulivyo”

“Kuna kikundi cha watu wachache wanaoongoza mapinduzi katika Africa, na nchi zinazoendelea, na ndiyo hao waliotekeleza mapinduzi na mauaji ya kimbali katika Rwanda na Burundi, sasa wamesuka mpango huohuo kwa ajili ya Tanzania” alijikohoza kidogo na kuendelea “Sasa kabla ya kutekeleza mpango huo kuna mambo ya kuandaa mazingira, Madam hivi tunavyoongea kuna watu wameshaingia nchini na si mmoja ni kikundi kutekeleza kazi hiyo”.

“Amata!” madam S aliita, akamshika bega Amata,

“Isabel, anahusika.”

“Hapana, sina uhakika kama anahusika.” Amata alimjibu Madam S

“Yeye amejuaje yote haya? Hata akueleze wewe, na wewe mmeongea saa ngapi? Maana ulishaambiwa usijiingize katika sakata la Isabel”

“Swali zuri Madam, nilikwenda kumtembelea jana jioni…”

“Hawakukuona?” madam S alimkatisha

“Hakuna aliyeniona, nilikwenda kikazi” Amata alijibu. Madam S akacheka kidogo

“Mbona unacheka?” Amata alimuuliza

“Umenikumbusha siku ulipojifanya wewe ni *padri* ukavaa kanzu na *stola* tulipokuwa Nairobi kwenye lile sakata la *‘Mauaji ya Kasisi’*” Amata alirudisha kicheko.

“Nakusikiliza” Madam S akaendelea

“Sasa nilipokuwa pale nilimuonesha kitambulisho changu Isabel, akanifahamu na akafanya ujanja Fulani akanipatia *memory card* bila mtu kujua, ndani ya *memory card* hiyo ndiyo kuna huo mpango wa mapinduzi, *Mpango Hasi* wameuita hivyo”, Amata akashusha pumzi kidogo na kuendelea, “Madam utekelezaji wake umeanza tayari, kifo kinachokuja ni cha kwako baada ya kile cha IGP na DCI”, alimaliza. Madam S alibaki mdomo wazi.

“Amata, una hiyo *memory* hapo?”

“*Yes*, Madam” Amata akatoa kijifuko kidogo cha plastiki na kumkabidhi Madam S.

“Twende” Madam Selline alimuamuru Amata na wote wakarudi garini. Ndani ya gari madam S alifungua kompyuta ndogo iliyotengenezwa maalum katika *dashboard* ya gari hilo. Akatumbukiza *memory* ile na ikaanza kusoma.

Baada ya kumaliza kuisoma, Madam S alishusha pumzi nzito na kujiweka vizuri kitini, hakuamini anachokisoma mbele yake, machozi machanga yalianza kumtoka, kwa kitambaa chake akajifuta.

“Madam,” kamanda Amata aliita

“Kamanda” aliitikia, akatikisa kichwa na kuendelea “Asante Kamanda, kwa kunijulisha kifo changu, tatizo sijui watanitafutia wapi, na sijui adui yangu ni nani. Ningekufa kama kuku mwenye kideli, lakini sasa nitakufa kishujaa. Ama zao, ama zangu” Mwanamama huyo alimaliza kusema kwa masikitiko, akaitoa ile kadi sakima na kuirudisha katika kasha lake.

“Isabel, akachukuliwe jioni hii awekwe hospitali ya jeshi kwa mahojiano” Madam alimwambia Amata, “Na hapo yeye atatueleza kila kitu, kisha tutajua tunaanzia wapi. Sasa twende kwa waziri mwenye dhamana”, alimalizia. Kamanda Amata alikaa nyuma ya usukani wa gari ya Madam S, alipotaka kuwasha gari ile, Madam S akamshika mkono Amata.

“Nakupenda Amata, nakupenda sana”

“Oya, pancha hiyo!!!” kijana wa pembeni barabarani hapo aliwatahadharisha kwa ukelele. Amata na Madam S walishuka na kuangalia kweli tairi lilikuwa *flat*. Wakatafuta uwezekano wa kulirekebisha ili waendelee na safari. Vijana walichangamkia tenda haraka haraka. Loh! Mlipuko mkubwa ulitokea, gari la Madam S ilipaishwa juu huku ikiwaka moto. Hali ilikuwa ya taharuki eneo lote hilo. Watu walikimbia huku na huko. Vilio vilisikika kila kona. Madam S alichanganyikiwa, alitaka kukimbilia kwenye gari lakini Amata alimshika na kumzuia alimvuta pembeni palipokuwa na tax na kumuingiza katika moja yazo.

“Shit!” madam S alitamka kwa hasira, “Walitaka wanimalize namna hii! Saa ngapi wameweka bomu kwenye gari yangu, saa ngapi? Nani kafanya hivi, n’tamtia mkononi tu.” Madam S alishikwa na hasira kali iliyoshindwa kujificha, Amata alijaribu kumpoza kidogo.

“Madam, tulia Madam, tuendelee na ratiba yetu kama ilivyo maadam tumepona maana kwenye orodha si umeona hata mimi nipo, wangefurahi kutumaliza pamoja” Amata alizungumza hayo huku akitoka na Madam S. Moja kwa moja safari iliishia kwa katika ofisi ya waziri wa ulinzi na jeshi la kujenga taifa. Madam S alioneka kuchanganyikiwa kabisa.

“Vipi mbona ghafla hivyo?” aliuliza Mheshimiwa.

“Tumenusurika kifo mheshimiwa,” Amata alimueleza waziri wa ulinzi kila kitu kama kilivyokuwa. Baada ya habari hiyo, mheshimiwa waziri alionekana kuchanganyikiwa kidogo, alitikisa kichwa chake na kumeza funda la mate.

“Hali imekuwa mbaya, tukicheza tutakufa wote huku tunajiona. Hatua za haraka inabidi zichukuliwe, na hii *memory* ifike kwa Mheshimiwa Rais haraka iwezekanavyo, hakuna jinsi.”

Waziri wa ulinzi aliitisha kikao cha dharula ofisini kwake cha wakuu wote wa vyombo vya ulinzi na usalama mchana huo. Punde tu wote walifika, Amata aliondoka kupisha kikao hicho na kurejea ofisini kwake ambako alimkuta Gina anasoma gazeti la *alasiri* ya siku

hiyo. Amata aliingia na kuketi juu ya kiti chake, akamtazama Gina na kutikisa kichwa.

“Tungekuwa tumekufa mimi na Madam S leo”

“Kwa nini?” Gina aliuliza huku akimpa *juice* kwenye bilauri. Amata alimueleza Gina tukio hilo, Gina alionekana kuchoka kwa habari hiyo.

“Gina, sina la kufanya hapa lazima niingie kazini bila ruhusa” Amata alimueleza Gina huku akivuta kitabu chake cha kumbukumbu na kupekua kurasa kadhaa, na kuandika vitu fulani.

“Gina, nashindwa nianzie wapi, naomba hata wewe uwe makini na usitembee kizembe kama kawaida yako. Hakikisha muda wote unakuwa na mawasiliano na mimi ili kujua nilipo na ulipo, kimenuka mama” alipokuwa akimaliza maneno hayo, saa yake ilimfinya mkono kuashiria kuna ujumbe uliokuwa ukiingia. Aliinua ule mkono na kubonyeza namba fulani. Mara mkanda maalum ukawa unatoka ndani ya saa hiyo ukiwa na maadishi…

> *‘tukutane shamba haraka iwezekanavyo mama anataka msaada Tena Sana Aisee’*

Mkanda ule uliishia hapo na kukatika, Amata alijiweka tayari.

“Gina natoka, *signal* yetu iwe ileile, sawa?”

*“Yes Sir!”* Gina alijibu kwa utani kama kawaida yake. Amata alitoka na kuelekea shamba.

♠ ♠ ♠

Gari la wagonjwa ya Jeshi kutoka hospitali ya Lugalo ilifunga breki mbele ya wodi ya mifupa (MOI), vijana wawili waliovalia sare za jeshi na msichana mmoja waliteremka na kuielekea wodi hiyo. Jambo la kushtua! Polisi aliyekuwa lindo alionekana kwenye kiti chake akiwa hana uhai. Yule kijana mwanajeshi alimtazama yule polisi mwenye bunduki mkononi, kisha akapitiliza ndani akifuatiwa na mwenzake.

Walipoingia ndani walimkuta muuguzi akiwa chali juu ya meza yake. Tundu la risasi lilionekana wazi kifuani pake. Chumba hakikuwa na mtu. Walitazamana hawakujua cha kufanya walitoka ndani ya chumba hicho kwa kasi na kuripoti haraka kambini. Isabel ametekwa.

Punde si punde magari ya polisi yalifika eneo hilo lakini habari hazikubadilika. Isabel alikuwa ametekwa. Inspekta Simbeye alijishika kiuno tu, hakujua nini la kufanya. Aliusogelea ule mwili wa yule askari na kuuangalia kwa makini, kisha akaingia ndani ambako vijana wake walikuwa wakifanya mambo mbalimbali ya kiusalama.

“Ina maana we hukuona yeyote aliyekuja?” Inspekta Simbeye alimuuliza daktari wa zamu jioni hiyo.

“Hapana, mi nimetoka hapa niliacha kila kitu sawa. Nashangaa hawa jamaa wameingia saa ngapi”

“Uphhhhhh” Inspekta Simbeye alishusha pumzi, kisha akausogelea mwili wa yule muuguzi, ilionekana

wazi kuwa hata tukio lenyewe bado ni bichi kwa kuwa jeraha lile la risasi lilikuwa bado linavuja damu taratibu. Kazi ilikamilika na miili yote ilihifadhiwa katika chumba cha kuifadhia maiti.

Inspekta Simbeye alikuwa kwenye lindi la mawazo *'Isabel anaweza kufanya hili?'* alijiuliza sana kwa kuwa aliamini kuwa ulinzi aliouweka wodini hapo ulikuwa makini lakini nini kimejiri katika utekaji huo. Lilikuwa swali gumu sana. Simbeye aliuangalia ule mlango mkubwa wa wodi hiyo, bado alikuwa haamini kilichotokea, mbele yake aliiona kazi jinsi itavyomuia ngumu, aliingia kwenye land cruiser ya Polisi na kuondoka.

♠ ♠ ♠

**K**amanda Amata aliketi juu ya kochi kubwa na upande wa pili kulikuwa na Madam S. Pamoja nao kulikuwa na watu wengine wawili.

"Kamanda, mi nakwambia kwenye hili sakata Isabel lazima anahusika" Madam S alimsisitizia Amata juu ya uhusika wake katika mpango hasi,.

"Hapana Madam, mi nafikiri ngoja aondolewe pale kisha tutaenda kuongea nae vizuri"

"Ok! Kamanda…" Madam S alikatishwa na mlio wa simu, akainua mkono wake na kuelekeza sikioni.

"*Yes*, nakusikia…" Madam S alijibishana na sauti ya upande wa pili

*"…"*

“Eee? What?” aliuliza kana kwamba kuna kitu ambacho hajakielewa katika simu hiyo. Alishusha mkono wa simu taratibu na kuupachika kwenye kikalio chake, kisha akainua bilauri ya maji na kujimiminia kinywani. Alikunywa kama mtu aliyekuwa na kiu ya jangwani, kisha macho yake mawili yaliyofunikwa kwa miwani  yalitua kwa wale vijana wawili na kisha kwa Amata. Akatikisa kichwa kuonesha masikitiko yake.

“Isabel” alitamka.

“Isabel? Kafanya nini?” Amata aliuliza

“Isabel katoroka, na isitoshe ameuwa muuguzi na askari wa mlangoni”.

Amata alishtushwa na habari hiyo ambayo kwake ilikuwa ngeni sana na ya kutoaminiwa. Aliinuka kitini na kuliendea dirisha kubwa lililopo hapo. Uso wake ulianza kushikwa na taswira ya gadhabu, *‘Madam yuko sahihi, inaonekana Isabel ni mmoja wao’*. Amata aligeuka na kumtazama Madam.

“Lazima apatikane” Kamanda alijikuta akitamka maneno hayo bila mwenyewe kujua.

“Kamanda, kazi imerudi mikononi mwetu kwa ushirikiano na jeshi la polisi, ila wao watafuata maelekezo kutoka kwetu, kazi njema vijana” Madam S alimaliza na kuelekea kwenye vyumba vya kulala.

Amata alitoka katika jumba lile kubwa *‘shamba’* akaingia kwenye gari lake na kutokomea mjini.

Matairi yake moja kwa moja yalisimama katika jengo la MOI. Kwa mwendo wa haraka alizivuta hatua zake na kuingia kwenye lango kuu kisha moja kwa

moja akaingia kwenye stesheni ya wauguzi. Akawakuta watatu wameketi hapo.

“Habari zenu wadada? Mimi ni afisa usalama” Amata alijitambulisha moja kwa moja bila kujizungusha, “poleni kwa msiba. Lakini naomba mnisaidie kitu kimoja ili kukabiliana na jambo hili”

“Karibu sana” mmoja wa wauguzi hao alimkaribisha

“Ningependa kuona daftari la zamu zenu, hasa wale waliokuwa wanamhudumia Isabel”

Bila kusita muuguzi yule alivuta daftari kubwa na kuliweka mezani. Amata aliangalia orodha ya majina yale na akalifikia jina la muuguzi aliyebadilishana zamu na marehemu ‘*Suzan Crispin*’, alifunga lile daftari na kuwarudishia

“Asanteni warembo” alijibu

“Kaka tutoe hata soda basi” mmoja wa wauguzi alitamka

Amata alitoa *wallet* yake na kutoa noti ya ya sh elfu kumi na kuwapatia, kisha akaondoka zake.

# 8

MADAM S, alibaki akihangaika mawazoni mwake, moyo wake ulijawa hasira, kila mara aliapa kumsaka aliyeweka bomu kwenye gari yake, lakini alimshukuru Mungu kwa kuwa amemuokoa katika hilo. Alitafakari kwa muda mrefu akipanga na kupangua lakini picha haikuja sawa sawa. Polepole alianza kupata hisia na kujua wapi ni pa kuanzia kazi, akiwa katika mawazo hayo alipitiwa na usingizi.

## Asubuhi ya siku iliyofuata

Madam S, aliliendea geti kubwa la gereji hiyo, akasukuma mlango mdogo, haukuleta matata, akaingia na moja kwa moja akafika ofisini.

"Samahani kuna kijana mmoja, jana asubuhi alinitengenezea gari yangu, nina shida nae, ile gari imekorofisha nataka akaiangalie" madam alimueleza fundi mkuu

"Unamjua kwa jina?"

"Hapana ila nikimuona nitamjua kwa sura"

Madam S pamoja na yule fundi walitoka na kuingia eneo la kazi, haikuchukua muda alimtambua kijana

yule, baada ya mazungumzo yote waliondoka pamoja. Madam S alipita taratibu eneo la uwanja wa Taifa.

“Unaijua ile gari iliyochakaa pale?” alimuuliza

“Hapana, ntaijuaje gari iliyoungua vile?”

“Ok, umejibu vizuri. Gari yangu jana imelipuliwa kwa bomu kama umesikia kwenye redio au TV”, Madam akameza mate na kuendelea “Sasa nina wasiwasi mkubwa wewe ndiye uliyefanya kazi hii, ya kuweka bomu na kutaka kuniua siyo?”

Yule kijana akaonekana kuchanganyikiwa, alikaa kimya kwa muda bila kujibu chochote.

“Usiponipa ushirikiano, utalala pabaya leo”

“Mama, utanionea tu, labda gari imelipuka kutokana na mfumo wa umeme”

“Hapana, mimi najua aina za milipuko, lile ni bomu” Madam S alitulia kisha akaendelea “Najua si wewe, ila nambie nani unamuhisi”

Yule kijana alibaki kimya moyo ulimuenda mbio hakujua nini cha kufanya katika hali hiyo. Alijaribu kuvuta kumbukumbu ya siku ile ili angalau ajue ni nani labda alifanya hivyo, *‘Bro Jose’*, alijiwazia mwenyewe.

“Nafikiri nimekumbuka kitu mama, kama ni yeye kuna *bro*’ mmoja tunamwita *Bro Jose*, mara nyingi huwa anakuja pale gereji”

Madam S akatikisa kichwa kuashiria kuwa amekubaliana na kijana huyo.

“Ok, uliona anafanya nini?”

“Alikuja pale, akawa anaisifia gari yako, mi nikiwa narekebisa tairi, ye’ akawa mara anaingia ndani ya gari mara anaagalia *engine*”

“Ok, zaidi ya hapo, hamna kingine?”

“Hapana”

“Sawa, sasa nitampataje huyo Jose?”

“Huyu Bro Jose ni ndugu na mwenye gereji yule uliyekwenda ofisini kwake”

Madam S, aligeuza gari na kurudi mjini, kisha alichukua simu yake ya upepo na kuongea na watu fulani. Alisimama mahali na mara land cruiser yenye vioo vyeusi ilikaribiana nao. Vijana wawili walishuka na kumchukua fundi gereji kutoka katika gari la Madam S na kumuingiza kwenye lile Cruiser

“Sikia, sikufanyii hivi kwa nia mbaya ila utajua baadae, utaenda kupumzika sehemu mpaka nitakavyokuachia” Madam S alimueleza yule kijana, na baada ya hayo “Panda kwenye gari” alimuamuru kupanda kwenye ile *cruiser*. Akiwa ndani wale vijana walimvalisha soksi usoni na kumfunika uso wote, kilichoendelea zaidi ya kupitiwa na usingizi mzito.

♠ ♠ ♠

“Umejiingiza kwenye jambo lisilokuhusu msichana!” Jomse alimueleza Isabel ambaye alikuwa hoi kwa kipigo kutoka kwa jamaa huyo.

“Hata mkiniua, nina uhakika hamtafanikiwa, taarifa tayari zipo kwenye vyombo vya usalama na ninajivuna kwa kufanya hilo, heri mimi nife lakini

niwaokoe maelfu wanaotarajiwa kufa hapo mbeleni" Isabel alizungumza kwa sauti ya kwikwi huku damu zikimtoka mdomoni, mguu wake uliokuwa umeanza kupona sasa ulitoneshwa tena kiasi kwamba hata hakuweza kusimama. Jomse alichukizwa na jibu la Isabel, alimpiga mateke mengi na mikanda ya kijeshi mpaka Isabel akapoteza fahamu kwa mara nyingine.

"Jomse, acha hasira utamuua bure tu huyu na haitatusaidia lolote" Tonton alimwambia Jomse.

"Na we usiwe kama Mandi, badala ya kufanya kazi uliyotumwa unaanzisha mambo mengine, hata nikimuuua huyu mimi napata faida gani, afe tu tutatupa maiti yake porini iliwe na mbwa" Jomse aliongea kwa hasira huku akirusha mikono yake hewani na kuondoka hapo "Muacheni afe apo hapo" aliwaeleza wengine na wote wakaondoka katika chumba hicho na kumuacha Isabel peke yake akiwa hana fahamu.

"Ok! Tuzungumze yajayo, kazi karibu inakamilika *plan A,* japo kuwa jana tumemkosa yule bibi kizee *(Madam S),* kweli ni tukio baya kwa upande wetu. Tunapofanya kosa moja tunajiharibia wenyewe" Jomse aliwaambia vijana wake akiwemo Tonton, akawatupia macho mmoja mmoja kisha akaendelea "Jamaa wapo tayari mipakani, wanasubiri tukamilishe *plan A*, ili wao waanzishe *plan B,* lakini kumkosa yule bibi jana, naomba muwe makini sana" Jomse alimaliza na kujimiminia *wine* yake kinywani. Kabla hajasusha

bilauri yake simu iliita mfukoni, akaitoa na kuiweka sikioni,

“Yeah man” aliitikia

“Eh! Unasema?(…), kama atarudi ni wa kumpoteza tu. We njoo huku watarudi hao” Jomse akashusha simu yake.

“Jamaa wamemkusanya dogo kule gereji” taarifa hiyo iliwashtua wote, kila mtu alionekana kuchanganyikiwa na hilo.

“Du! Eee sasa hapo patamu, tukamilishe mpango huu haraka iwezekanavyo” Ton alitoa rai.

“Sasa ni kuwa makini zaidi, maana tayari watakuwa wameanza uchunguzi juu ya tukio lile, na hivyo kabla hawajatushtukia tuwe tumekamilisha. Ton mkabili bibi kizee ila kuwa makini, sisi watatu tumkabili Kamanda Amata, na roho yake iwe mikononi mwetu leo hii”

Walivunja kikao na kurudi kule walikomuacha Isabel, wakamkuta bado amezirai. Jomse akachukua maji ya baridi kwenye ndoo na kummwagia.

“Amka mpumbavu wewe, na wewe lazima ukutane na Madam Rose akutie adabu” Jomse alifoka na kumuacha Isabel akijivutavuta pale chini.

Ton alikuwa kimya sana, fikra zake zilimfanya akose raha kabisa, aliingia kwenye gari lake tayari kuondoka

“Ngoja nikaonane na Suzan nimpe mzigo wake narudi baadae” Ton alimuaga Jomse

“No! Ton usiende peke yako, huko uendeko hakutabiriki, nenda na Anaconda akulinde” Jomse alitoa amri na ikafuatwa.

Punde si punde walifika katika hotel ya Valley View, Anaconda akashuka kwanza na kuangalia uku na huko kisha akagonga kioo cha dirisha la nyuma kuashiria kitu. Ton akashuka na moja kwa moja akongoza kuelekea hotelini na Anaconda akamfuata nyuma yake.

Tax jeupe lilisimama nyuma kidogo ya gari la akina Ton, mwanadada mrefu kiasi, mwenye mwili wa kawaida, aliteremka na baada ya kuiweka miwani yake vizuri, alivuta hatua taratibu kuielekea hoteli hiyo. Alichukua *lifti* kupanda ghorofa ya nne kisha akaelekea chumba namba saba akagonga mlango kwa staili aliyoelekezwa. Mlango ukafunguliwa.

“Karibu Suzan” Anaconda alimkaribisha

“Upo peke yako?” Ton alidakia kwa swali

Suzan alisita kidogo kujibu “Ee nipo peke yangu”

“Ok haina haja kuchelewa, tunashukuru kwa kazi uliyotufanyia. Na ujira wako huu hapa dola za kimarekani elf moja” Ton alipomaliza kuongea hayo alimkabidhi kitita hiko Suzan, nae akakisunda katika mkoba wake. Suzan hakuamini kabisa anachokishuhudia, pesa zote hizo kwa kazi ndogo, kazi ya kumsaliti Isabel.

“Ok. Mi naomba niende” Suzan aliaga na kusimama tayari kuondoka

“Ok Suzan, *be carefull*” Ton alijibu na kumruhusu Suzan kuondoka.

Suzan aliliendea tax iliyomleta na kuingia mlango wa nyuma wa gari hiyo.

“Ingia! Ukileta fujo nakumaliza” Suzan alitazamana na domo la bastola kutoka kwa Gina, Gina hakuonesha uso wa masihara hata kidogo

“Ingia” alirudia tena na Suzana akaingia ndani, Gina akiwa na *gloves* maalum mikononi aliuchukua mkoba wa Suzan huku mkono mmoja ukiwa bado umeshikilia bastola ile. Aliupekua na kutoa na alipoiona simu yake aliichukua kisha akaitia kwenye kimfuko cha plastiki na kuihifashi. Suzan akatiwa pingu mikononi.

“Haya endesha gari”

“Tunaelekea wapi?”

“*Central police*”

Dreva aliondoa gari na kuelekea alikoagizwa. Walipofika central Suzan alishushwa na Gina akafuata nyuma yake.

“Hifadhi huyu, naomba asihojiwe lolote mpaka mpatapo amri nyingine” Gina aliwakabidhi Suzan polisi waliopo kaunta na kisha yeye akaongoza kuelekea ofisi ya Inspekta Simbeye.

“Kazi uliyonituma imekamilika afande” Gina aliongea kwa ukakamavu mbele ya bosi wake

“Vizuri sana afande, waweza kwenda nitawasiliana na wewe nitakapokuhitaji” Inspekta Simbeye alimueleza Gina. Gina akaonesha ukakamavu wake

kwa kubana mikono yake miwili kuonesha heshima, kisha akageuka na kuondoka.

♠ ♠ ♠

"Suzan, hebu kuwa mzalendo, tueleze, unajua Isabel alipo?" Sergeant Bizibu alimuuliza kwa upole

"Jamani mimi nina mhusiano gani na Isabel? Mimi ni muhudumu wa afya, nimeingia kazini nakuta hiyo habari, mbona mnanionea?" Suzan alilalamika

"Sikia mrembo, hapa hatujaja kukufanyia chochote kibaya, tunachotaka ni wewe kujibu maswali yetu, usitufiche kitu. Tii sheria bila shuruti, lakini ukikaidi utashurutishwa kuitii. Tueleze Isabel ametoroka au ametekwa kwa mawazo yako?"

Suzan alitulia kidogo aliziangalia pingu zile za chuma mikononi mwake. Hakuamini. Aliinua uso wake na kumtazama polisi huyu mwenye cheo cha sajini aliyeketi mbele yake. Aligeuka huku na huko akaona kuwa kumbe wapo wawili tu mle ndani, akajikohoza kidogo

"Sikia afande Isabel alikuwa anaumwa sana hasa mbavu na mguu wake, lakini mimi simjui kiundani anaweza akawa ametoroka au ametekwa kwangu ni swala gumu kwa kuwa sikuwepo kazini na aliyekuwepo ameuawa" Suzan alijibu kisha akainamisha kichwa chake kwenye kijimeza kile kidogo kilichotengenezwa kwa chuma

"Kwa hiyo unatuambiaje?"

"Mi sijui kilichotokea"

Baada ya mahojiano marefu kati yao, sergeant Bizibu alighairisha zoezi na kuamuru Suzan apelekwe chumba cha pili akahifadhiwe kwa muda.

Kilikuwa ni chumba chenye giza kilichojengwa katika chini ya ardhi, Suzan aliingizwa na kukalishwa kwenye kiti maalum mikono yake ikiwa nyuma ya kiti hiko na kusikiliwa na kamba maalum. Suzan hakuona chochote zaidi ya giza nene lililokijaza chumba hicho.

"Jamani huku ni wapi?" aliuliza kwa sauti ya kilio

"Huku ndiyo chumbani kwako kwa muda tu" alijibiwa na WP mmojawapo aliyekuwa akimfunga vizuri katika kiti hiko kisha wakatoka na kumuacha wamemfungia mlango.

♠ ♠ ♠

"Amekataa kutoa ushirikiano" Inspekta Simbeye alimueleza Kamanda Amata aliyekuwa akizungushazunguash akalamu yake vidoleni.

"Au tunamuonea?" aliuliza Amata

"Hapana haonewi mtu, huyu kwa vyovyote anahusika"

"Inspekta, tusifanye mambo kwa hisia, anahusika vipi? Hilo ndilo la msingi. Katika pekuzi zenu kitu gani mmechukua kama kisaida polisi?"

"Ah, tumechukua simu yake ya mkononi."

"Hapo umecheza, hebu lete hiyo simu tuangalie namba zilizopigwa au zilizoipigia, tunaweza kupata jibu" Amata alimaliza kwa maneno hayo.

“Kamanda, sikuwa na wazo kama hilo, mi nilitaka kwenda kampuni ya simu kucheki rekodi za simu na meseji zake”

“Huko mbali Inspekta, umeanza kuzeeka au?” Kamanda Amata alimtania mzee huyo wa makamu amabaye anamkumbuka sana kwa kwata alilompigisha huko CCP Moshi.

Kamanda Amata aliifungua simu ile na sekunde kadhaa ilitoa mlio mkali na kuonesha picha ya bahasha juu ya kioo chake, akaufungua ujumbe huo…

> *‘…umefika salama, kama utahitaji msaada utuambie…’*

Ujumbe ule uliisha hivyo na hakukuwa na namba yoyote zaidi ya maandishi *private number*, Amata alitikisa kichwa na kuendelea kuangalia jumbe zingine. Nyingi alizishuhudia za mapenzi tu ambazo hazikuwa na maana sana kwake, alipotaka kubadili kuangalia simu zilizoingia na kutoka ndipo alipouona ujumbe wa mwisho

> *‘…Valley View hotel Na. 407…’*

Amata hakuona umuhimu wake alijua itakuwa ni sehemu ya kukutania na mpenzi wake, lakini kengele za hatari ziligonga kichwani mwake, akainua mkono kwa kidole chake cha shahada akajikuna pua yake.

“Vipi Kamanda, umegundua kitu?” Inspekta Simbeye aliuliza

“Aaa mapenzi na miadi tu”

Akampa ile simu Inspekta Simbeye aliitupia macho ile meseji, jicho lake la kushoto likamcheza, hatari! Alirudisha simu kwa Amata.

“Kamanda, Valley View.”

“Vipi umehisi kitu, Inspekta?”

“Kabisa, bila shaka”

“Ok, hiyo ni point namba moja, na hiyo itazaa namba mbili. Naomba nikuache Inspekta”

“Hamna shida ukihitaji msaada usisite kunitafuta”

Kamanda Amata alitoka na kuchukua tax kuelekea ofisini kwake ambako alimkuta Gina akiendelea na kazi hii na ile ilimradi siku zilienda.

“Karibu” alimkaribisha

“Asante, hamna jipya?”

“Hamna”

Amata aliketi juu ya kiti chake na kuanza kutafuna karanga zake moja baada ya nyingine huku akiandika mambo Fulani katika kitabu chake cha kumbukumbu.

♠ ♠ ♠

“Kamwe hamtoweza kufisha juhudi za kimataifa, mpango huu umesukwa na kusukika” Jomse alimueleza Madam S maneno hayo huku akiwa kamuelekezea domo la bastola kubwa aina ya *revolver* iliyofungwa kiwambo cha sauti.

“Wewe ni nani?” Madam S aliuliza

“Mimi ni mwanamapinduzi halisi, nipo hapa kwa kazi moja tu ya kuondoka na roho yako” aliongea kwa dharau.

Ilikuwa ngumu kwa Madam S kujitetea mbele ya bastola hiyo ambayo haikuonesha masikhara hata kidogo, alishindwa kumtambua mtu huyu kwa kuwa alikuwa amevaa soksi kichwani kuuziba uso wake na kuruhusu macho tu kuona.

“Umeingiaje ofisini mwangu hali milango yote nimefunga?”

“Kama Yesu alivyoingia kwa wanafunzi wake huku milango imefungwa” alijibiwa. Madam S alipandwa na hasira kwa dharau alizozionesha huyo bwana, alimkazia jicho na kumwangalia kwa hasira.

“Usiniangalie kama unavyomwangalia paka wako, nimeshakwambia nataka kuondoka na roho yako ili mipango mingine iende, na hapa ninavyoongea na wewe kijana wako anayejifanya mtukutu Kamanda Amata yupo matatani, tunataka tupindue nchi hii na hilo kwamwe halipingiki.”

Madam S alishusha pumzi ndefu akimwangalia mtu yule aliyekuwa akijiamini ndani ya ofisi ya watu. Akili ilimzunguka huku na huko, hakujua afanye nini. Kutoka pale alipoketi, Jomse alisimama taratibu, kitendo ambacho madam S alikiona ni udhaifu mkubwa. Kwa wepesi ambao haukutegemewa madam S alijirusha mtindo wa *tick tack* na kuipiga bastola ile. ikatoka mikononi mwa Jomse na kupaa juu. Ikagonga *ceiling board*. Jomse akiwa bado anashangaa akitaka

kuidaka bastola, Madam S alikuwa tayari ameshatua chini. Pigo moja la karate lilitua sawia katika mbavu za Jomse, maumivu yake yalimfanya apoteze muelekeo. Bila kuchelewa Jomse aliachana na wazo la bastola na kumkabili Madam. Patamu! Jomse kwa haraka alimtazama Madam S na kumuona jinsi alivyotulia kumkabili, bila kuchelewa Jomse alicheza *Ashi Barai,(Foot sweep kick),* kwa mguu wa kushoto aliupiga mguu wa madam S ambao ulikuwa umetangulizwa mbele kwa *kuufagia*. Madam S alipoteza *stamina* na teke la nguvu lilitua sawia kwenya sikio la madam S. Mpepesuko wake ulimpeleka mpaka kwenye kabati lililokuwa limejaa mafaili na kabati lile lilishindwa kuvumilia na kuanguka palepale alipoangukia madam S. Kitendo bila kuchelewa madam S alikuwa tayari kajirusha kiufundi na kuondoka eneo lile ambapo kishindo cha kabati kiliwashtua walinzi wa nje nao kwa haraka wakakimbilia ndani kuona kunani. Madam S alijiviringa na kusimama karibu kabisa na kabati lake dogo upande wa pili wa meza kubwa tayari *Colt 45* bastola hadimu ya kimarekani ikiwa mkononi mwake. Kidole kwenye *trigger* kilicheza kidogo tu Colt 45 ikabanja lakini kwa haraka Jomse alishatoka eneo lile kwa sentimeta kadhaa.

Mlango ulipigwa kikumbo na walinzi wawili wakaingia.

“Mikono juu!” askari mmoja wa kampuni ya ulinzi alimuamuru Jomse. Kosa kubwa! Jomse aliinua mikono juu wakati huo tayari alishachomoa kisu chake kidogo

katika mkanda wake na kukirusha kwa ustadi wa hali ya juu, moja kwa moja kilitua katika koromeo la askari yule. Kishindo kingine kilisikika cha bunduki kubwa na kutawanya taa kubwa iliyokuwa imesimamishwa kwenye kona. Jomse aliruka '*back*' na miguu yake ikatua katika kioo kikubwa cha dirisha na kudondoka nje. Madam S na yule mlinzi mwingine walitoka haraka na kukuta tayari Jomse karuka wigo wa waya na kudandia pikipiki yake kubwa *Yamaha* la Kijapani. Wamemkosa.

Madam S aliificha haraka bastola yake kwenye mkanda wake maalum aliouvaa ndani ya koti lake la suti, na kurudi kule ofisini kwake. Walimkuta yule mlinzi akikata roho, mauti yalimfika.

Vitu vilikuwa shghalabaghala ofisini kwa madam S.

*"Bastard !!!"* Madam S alifoka kwa hasira huku kifua chake kikipanda na kushuka. Akachukua simu yake na kubofya namba za Kamanda Amata…

> *'mteja unayempigia kwa sasa hapatikani, jaribu tena baadae'*

"Shit!" aling'aka mwanamama yule na kufungua droo yake. Akatoa *magazine* (kihifadhi risasi) nyingine iliyoshiba risasi. Akatoka nje akiwa anataka kuingia kwenye gari lake. Alishtushwa na sauti iliyomwita pembeni.

"Sellina!" alikuwa ni Inspekta Simbeye.

“Hali ni tata Inspekta”

“Unaenda wapi *boss*?” Inspekta aliuliza.

“Naenda kumsaka hayawani” alijibu huku akiingia kwenye gari.

“Hapana, subiri kidogo akili yako itulie” Simbeye alimbembeleza mwanamama huyo, maana alimuona jinsi alivyopaniki na ule utu uzima. “Nipe bastola” Inspekta Simbeye alimuomba huku akimnyooshea mkono. Madam S alitulia kidogo.

“Kwa kuwa ni kazi yako chukua unikabidhi baadae” alimwambia Inspekta.

Madam S alipiga tena simu ya Amata bado ilikuwa haipatikani. Kijasho kilimtiririka. Hana la kufanya. Alishuka garini na kurudi ofisini kwake. Mlangoni alisipishana na mwili wa yule mlinzi ukiwa ndani ya machela na kufunikwa. Aliufunua na kumtazama kwa huruma. Hakuwa na la kufanya, alimwombea kwa Mola wake kimoyomoyo.

♠ ♠ ♠

Kamanda Amata alifika katika kaunta ya Valley View Hotel. Mwanadada mrembo alimwangalia kijana huyu mtanashati ambaye mwili wake uliojengeka vizuri ulikuwa umetulia vyema kwenye fulana yake nyeusi iliyombana na kuonesha siha yake ya kimazoezi.

“Karibu nikusaidie tafadhali” muhudumu yule alimkaribisha Amata

“Asante sana, nafika chumba namba 110 tafadhali” akili ya Amata ilikuwa inafanya kazi haraka, katika kitabu cha wageni pale mezani alishaona kuwa chumba namba 110 kimechukuliwa na mwanamke hivyo ingekuwa rahisi kwa mhudumu huyo kumruhusu bila shaka.

“Sawa, subiri mtu akusindikize.”

“Hapana, nitakwenda mwenyewe”

Kwa mwendo wa haraka haraka Amata alikwea vidato vya ngazi za jengo hilo mpaka ghorofa ya nne na siyo chumba alichotamka. Baada ya kuzimaliza ngazi zile alifika kwenye korido ndefu iliyotandikwa zuria mwororo jekundu. Alitembea mpaka mlango namba 07. Akasimama kidogo, akaangalia huku na huko na alipoona kuna utulivu, akasikiliza kidogo. Kwa hisia zake akagundua kuwa kuna utulivu wa hali ya juu, akachukua moja ya funguo zake na kutumbukiza kunako tundu husika. Mizunguko miwili-mitatu tu mlango ulilegea na taratibu Amata aliufungua na kuingia ndani kisha kuubana nyuma yake na funguo kurudisha mfukoni.

Kwa hatua za hadhari akihakikisha hagongi kitu chochote alitembea taratibu na bastola yake ndogo ikiwa tayari mkononi, alisita kidogo na kurejesha akili yake chumbani mle. Alisikia maji yakitiririka bafuni, aliuendea mlango wa bafuni taratibu bastola ingali tayari mkononi, kwa mkono wa kushoto alitikisa kitasa cha mlango huo na mlango bila ubishi ukajiachia. Maji yalikuwa yakitiririka, lakini hakukuwa na mtu bafuni.

Amata aligundua hapo kachezwa shere. Hakuingia! Akapuuzia na kurudisha bastola yake kiunoni. Lahaula! Alipoiweka tu bastola yake, kabla hajageuka, pigo moja la haja la karate lilitua shingoni mwake. Kigiza cha sekunde kadhaa kilimtawala. Alijihisi kukosa nguvu lakini nuru ya mwanga ikamrejea tena. Hakuona haja ya kufanya mzaha katika hilo. Akajiangusha chini huku akiipamia meza ndogo iliyokuwa na chupa kubwa ya pombe juu yake. Adui yake akaona huo ndiyo mwanya wa kufanya yake. Akamuendea Amata pale chini. Lakini kabla hajatahamaki, Amata aliinua ile chupa iliyokuwa hapo chini na kumrushia adui yake usoni kwa nguvu zote. Wakati adui yake akiipangua kwa ufundi chupa ile, Amata kwa mguu wake wa kulia, bado akiwa chini alimkanyaga adui yake kwenye zakari na kumfanya atoe mguno wa maumivu. Kwa mruko wa kisarakasi, Amata alijinyanyua na kuwa wima, ngumi nzito ilikuwa ikiuelekea uso wa Amata, naye kwa mchezo wa kitoto akaepa na kuudaka. Bila ajizi akaukunja na kuuvunjia begani kwake. Yowe la nguvu lilimtoka jamaa huyo baada ya kushuhudia mifupa ya mkono wake ikiachana. Amata aliuvuta mguu wake wa kulia na kumpita kidogo kisha kumchota mtama kwa nyuma na jamaa alitua chini kama mzigo na kuivunja meza ya kioo iliyokuwa hapo vipande viwili. Goti la kamanda likatua juu ya tumbo la adui.

“Tulia! Shhhhhh!” Amata alimuonya jamaa kutulia huku akiwa kamshika mkono wake uliovunjika kwa

mkono mmoja na mwingine kashika kipande cha chupa. Damu zilikuwa zikimtoka kinywani, “Nani amekutuma?” alimsaili huku akiuzungusha taratibu ule mkono uliovunjika.

“Aaaaaaaa, unaniumiza, ntasema ntasema..” adui alitoa yowe la uchungu

“Sema!”

“Walionituma siwajui kwa undani” huku akilia kwa uchungu “wapo wengi ila nawajua kwa uchache”

“Wataje majina na wapo wapi?” Kamanda aliuliza kwa hasira, “Hujibu ee?” aliuzungusha mkono kwa nguvu.

“Wapo Burundi, wapo Burundi na wengine Rwanda” alijibu

“Taja majina” Amata alilazimisha

“Aaaa nimeshakujibu tayari” alilalamika

“Bado, na hapa mko wangapi?” Amata aliuliza. Na alipoona jamaa huyo hatoi ushirikiano, aliuzungusha mkono kwa ghafla, yowe la nguvu lilimtoka na Amata akambana mdomo kwa kiganja cha kulia baada ya kukitupa kile kipande cha chupa.

“Tupo wengi, na wengine miongoni mwenu…” alijibu huku akianza kutupatupa miguu huku na huko, Kamanda Amata alimwangalia kwa hasira.

“Shit!” povu lilimtoka mdomoni na macho yake yakageuka kuashiria kuwa uhai haupo tena. Kimbebe!

*‘Tupo wengi na wengine miongoni mwenu’* sentensi hii ilimjengea mwangwi Amata, hata akajikuta nguvu zinamwishia. Alisimama na kumuacha huyo jamaa

hapo chini. Aliiendea meza iliyokuwa na *computer* mpakato, akapekua kwenye droo na kukuta *business card* mbalimbali. Akazikusanya zote na kuzitia mfukoni. Kadi mmweko iliyokuwa ikining'inia katia *laptop* na kitabu cha kumbukumbu akavitia katika begi lake dogo la mgongoni na taratibu akauendea mlango, na kutokomea. Alipita kaunta na moja kwa moja alifika nje kabisa, alikatiza mtaa wa kwanza wa pili na kuingia katika gari lake akaketi.

"Uphhhhhhh," akashusha pumzi kisha akawasha gari na kuingia barabarani akapotelea mjini.

♠ ♠ ♠

Tonton alifungua mlango wa chumba chake, hakuamini alichokiona, Anaconda alikuwa amelala chini chali damu zikiwa zimetapakaa na kuanza kuganda huku chumba chote kikiwa na hewa nzito. Alibaki kutikisa kichwa, hakujua la kufanya alipotupa jicho mezani laptop yake ndogo *(note-book)* haikuwepo, alichanganyikiwa. Alitazama huku na huko na kuichomoa bastola yake kisha kwa mwendo wa minyato aliusogelea mlango wa bafuni ambako bado maji yaliendelea kumwagika. Hakuna mtu. Alirudi na kuangalia kwenye kibaraza cha nje. Bado hakuna mtu, akasonya na kurudisha bastola yake kiunoni. *'Hapa hapana usalama'* alijisemea na moja kwa moja aliliendea begi lake chumbani na kukuta lipo kama alivyoliacha. Alichukua kabrasha zake na hati za safari

na kutoka chumbani mule. Akiwa chini anatoka katika kambarau alipishana na askari polisi wanne wakiingia kupandisha juu. Moja kwa moja akapita na kuondoka zake, njiani alikuwa akiendesha gari huku akiwa na mawazo mengi. Kwanza aliona wazi kuwa ‘bwawa limeingia luba’, hamna la kufanya, alifikiria tu kwanza kufika *chimbo* ili akajipange upya na wenzake waliosalia *chimboni*. Aliiacha barabara ya Msimbazi na kuchukua ile ya Morogoro kuelekea posta lakini katika makutano ya Umoja wa vijana alikunja kulia na kuipita ile ya Lumumba mpaka Nkurumah na kurudi mpaka mataa ya Kamata na kukunja kushoto kuelekea Kurasini. Dakika kumi nan ne zilitosha kuwasili.

Honi za hatari zilipigwa na geti likajifungua lenyewe. Bila kuuliza aliingia ndani na kumkuta Jomse akiwa kajiinamia huku mkono mmoja ukiwa unaminyaminya mbavu zake. Kelele ya mlango ilimfanya kushtuka na kuikamata bastola yake tayari kwa kazi.

“Oh Ton, *bienvenue mon ami*” Jomse alimkaribisha kwa lugha yao ya kifaransa, “Ton, kazi hii imeshatuelemea, yule bibi nimeshindwa kummaliza, sijui itakuaje, sijui nimtafutie wapi, amekuwa mbogo aliyejeruhiwa” Jomse alipigisha viganja vya mikono yake kwa ishara ya kukata tamaa na kutikisa kichwa chake kushoto kulia.

“Jomse, Anaconda ameuawa, nahisi si mwingine ni Amata aliyefanya kazi ile” Ton alifikisha taarifa. Jomse alipatwa na mshtuko mkuu alibaki midomo wazi na

mikono ikimtetemeka, alipiga ngumi mezani na meza ile ya kichina iliyotengenezwa kwa *cheapboard* ailigawanyika vipande viwili. Aliichukua bastola yake na kuitazama kwa makini *'Kisasi'* alijisemea, akiwa kaukunja uso wake kwa hasira.

"Wangu Amata, wako Bibi, Meno ya Mamba atabaki hapa kumlinda Isabel"

# 9

KOMPYUTA ya Kamanda Amata ilikuwa ikiisoma flash aliyoichukua kule hotelini, siri nyingi na za kutisha zilikuwa zikipita katika kioo cha kompyuta ile, Amata alibaki kapigwa na butwaa, akili ilimsimama na meno kumchezacheza, hapa ndipo aligundua hatima ya mpango hasi ambayo katika memory card aliyopewa na Isabel kipande hiki hakikuwapo. Aliendelea kusoma na kupata majina kadhaa ya madigala wa mpango huo duniani, aligundua kuwa kumbe ni nchi za Maghalibi ndizo zinazofadhili mapinduzi hayo kwa faida yao wenyewe, Amata alizama katika lindi la mawazo, akiwaza na kuwazua, akipanga na kupangua.

Alipogeuka kuielekekea simu yake na ndipo alipojikuta kuwa hayupo peke yake.

“Tulia hivyo hivyo!” sauti ilimkoromea kutoka upande ule, Amata hakuwa na la kufanya

“Simama taratibu” aliamriwa na kutii bila shuruti “Kwa mwendo wa taratibu ongoza nje ya nyumba yako kupitia geti kubwa”, Amata alifanya hivyo na kufika nje ambako aliikuta gari ndogo aina ya Toyota Altezza

ikiwa buti wazi “Ingia kwenye buti, ukileta matata nafumua ubongo wako sasa hivi”

Amata alitazama huku na huku “Usijaribu kuleta shida ingia twende”, Kamanda Amata na ujanja wake wote aliingia ndani ya buti ya gari hiyo, Jomse aliruka kwa wepesi na kulifunga buti lile Amata akiwa ndani, kisha akaingia garini na kuondoka kwa kasi.

“Kamanda Amata nimemtia mkononi” Jomse alikuwa akiongea kwa simu na mtu mwingine

“Vema, hakikisha unamhifadhi vizuri mpaka amri nyingine itapotolewa” sauti ya kike kutoka upande wa pili ilisikika

“Sawa Madam, nitahakikisha hilo, hawezi kunitoroka huu ndiyo mkono wa Shetani” Jomse alimalizia kauli yake.

Kamanda Amata akiwa ndani ya buti hakuweza kujinyoosha kutokana na udogo wa buti lile, aliuinua mkono wake wa kushoto uliokuwa na saa kubwa ya kisasa akabofya kitu Fulani pembeni mwa saa hiyo, kidoti chekundu kikawa kinawakawaka juu ya kioo cha saa hiyo, aliisogeza karibu na kinywa chake na kuongea maneno Fulani, kisha akabofya tena sehemu nyingine, sasa kidoti cha kijani kikawa kinawakawaka, akatulia kimya butini akisubiri hatima yake huku akihesabu kona ya kwanza mpaka ya mwisho kulia ama kushoto.

Gari ilisimama, kamanda Amata alihisi geti likifunguliwa na sauti zilizoongea kifaransa zilimfikia masikioni mwake, alielewa yote yaliyoongelewa, na

baada ya sekunde kadhaa gari ile iliingizwa ndani na geti kufungwa nyuma yake, gari ikasimama

“Kuwa muangalifu, hajafungwa huyo” Jomse alimuamuru Meno ya mamba ambaye alibaki pale kuweka ulinzi kwa Isabel na jingo zima kwa ujumla.

“Huyo msichana mpumbavu ameamka?” Jomse aliuliza tena

“Hapana bado hajaamka, na sijui kama ataamka maana hali yake ni mbaya sana” Meno ya mambo alimjibu Jomse.

“Ah Muache afe tu, ijapokuwa Madam Rose alikuwa anamuhitaji lakini hatuna la kufanya” Jomse alimueleza Meno ya Mamba. Amata aliposiki kauli hiyo aliumia sana kwa kuwa aligundua kuwa Isabel lazima atakuwa ametekwa na kuwekwa huku, na kwa vyovyote atakuwa kwenye hali mbaya kutokana na mateso makali.

“Shuka taratibu, usilete makeke, la, hii SMG itakufumua vibaya na mwili wako utakuwa chakula cha samaki usiku huu” sauti kavu ya Meno ya mamba ilisikika masikioni mwa Amata. Kamanda Amata alishuka kutoka kwenye buti ya gari ile na kusimama kwa miguu yake miwili, mikono yake ikiwa juu aliona asifanye makeke yoyote kwani alishajua kuwa Isabel yupo eneo hilo, japokuwa kwake haingekuwa kazi ngumu kuwadhibiti wote wawili.

“Geuka nyuma yako na uongoze njia unayoiona”

Amata alitii na kufuata kijia hiko huku mikono yake ikiwa juu kama alivyoamuriwa. Hatua chache

alijikuta katika ubaraza mpana tu, ukiwa na viti viwili na kighorofa kimoja, chini sakafuni aliona mwili wa binadamu aliolala bila uhai, Amata alipigwa na butwaa aliutazama mwili ule kwa haraka haraka akagundua kuwa si mwingine ni Isabel alikuwa amelala chini na mwili wake kutupwa kama wa mbwa. Hasira kali zilimshika Kamanda Amata hakujua afanye nini, alitamani aukimbilie ule mwili kujua kama una uhai au la, lakini alishindwa japo alikuwa anaumia sana.

♠ ♠ ♠

## Ikulu ya Dar es salaam

Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, akiwa tayari katika suti yake ya kijivu na msafara wake wa watu wa usalama, walijipanga kwa safari ya uwanja wa ndege, tayari kwa safari ya New York ambako alialikwa kwa mkutano maalum wa Umoja wa Mataifa juu ya mabadiliko ya tabia nchi hasa katika bara la Asia na Afrika. Kila kitu kilikuwa kimekwishapangwa, watu wa usalama tayari walikuwa wameandaa kila kinachobidi kwa ajili ya kutekeleza na kuhakikisha kuwa mheshimiwa Rais anafika safari yake salama na kurudi salama, ujumbe anaosafiri nao tayari ulikuwa ndani ya ndege kule uwanja wa ndege terminal 1 karibu kabisa na kambo ya jeshi la anga kikosi namba 603 KJ wakiwa wanamsubiri tu mheshimiwa Rais, kwa ujumla itifaki yote ilizingatiwa.

Ving’ora vilisikika kutoka barabara ya Nyerere vikiingia moja kwa moja uwanja wa ndege, na mara Rais alishuka na kuagana na viongozi, kama mkuu wa mkoa wa Dar es salaam, waziri mkuu, waziri wa ulinzi na makamanda wengine kama ilivyo ada, alifika kwa madam S, alisimama kidogo, akamtazama mama huyu wa makamo ambaye tayari nywele zake ziliznza kubadilika rangi ashukuru tu Wachina walileta piko, akapeana nae mikono na kumkumbatia, “Nchi iko mikononi mwako,” almnong’oneza, hakuna aliyesikia, kisha akakimbia kidogo kwa mtindo wa kutroti na kuingia kwenye ndege kabla hajaishia kabisa aligeuka na kuwapungia mkono wa kwa heri, kisha akapotelea ndani.

Rubani mzoefu wa serikali aliyekabidhiwa jukumu zito la kuibeba serikali ndani ya ndege huyu wa chuma alivaa vifaa vyake maalum vya mawasiliano masikioni mwake na kuwasaidizi wote wakafanya hivyo kisha akabofya mahali Fulani na kuanza kuongea maneno matamu kama haya

“5H-ONE, Gulfsream Aerospace G-V SP G550, ndege ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaomba njia kuruka saa tatu na dakika thelathini usiku huu, kuelekea New York, USA” sauti jiyo ilisikika moja kwa moja katika chombo maalum cha muongoza ndege katika mnara mkubwa wa kuongozea ndege ulio upande wa kusini wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Kambarage Nyerere ‘JNIA’.

“5H-ONE, Gulfsream Aerospace G-V SP G550, unaruhusiwa kuruka kupitia upande wa mashariki” sauti ya muongoza ndege iliruhusu kuondoka kwa ndege ya Rais baada ya kuhakikisha anga yote ipo salama kabisa.

Wakiwa wameketi sawia na mheshimiwa Rais katika kaofisi kake kadogo ndani ya ndege hiyo tayari kwa safari kuelekea New York. Dakika chache tayari ndege ile ilikuwa imeiacha ardhi ya Tanzania na kupasua anga kwenda anga ya kimataifa, ikiwa chini ya uangalizi wa Rubani mzoefu Capt. Maga Jr. na wasaidizi wake watatu.

Madam S, aliiangalia ndege ile inapopotelea mawinguni upande wa Vingunguti, yeye na wengine waliomsindikiza mheshimiwa Rais walianza kuchukua magari yao tayari kwa kurudi kwenye shughuli zao nyingine, mara alihisi saa yake kubwa ya mkononi inamfinya kwa vijimeno maalum vilivyo chini ya saa hiyo, alihisi kuna kitu, akaingia haraka kwenye gari yake na kubonyeza kitufe Fulani pembeni ya saa hiyo, mara ikaanza kupiga ukulele kwa sauti ya chini ikitoa kamkanda kembamba ka plastiki kalikokuwa na maadishi Fulani.

*‘Att:Hakikisha mheshimiwa Rais haondoki, hiyo ndege imetegwa bomu kwenye control box na italipuka akiwa angani, fanya hima, mimi nimetekwa na sijui nilipopelekwa, fanya hima Tena Sana Aisee’*,

Madam S alishuka kwenye gari akiwa kama aliyechanganyikiwa hakuwa anjua afanye nini, alichukua simu yake na kubofya namba Fulani.

“Hallo, naomba urudi uwanjani haraka sana kuna dharula” simu ilifika kwa waziri wa ulinzi aliyekuwa tayari amekwishaondoka lakini gari yake bado ilikuwa njia panda ya air port kuelekea mjini, dreva wa gari hiyo aina ya Toyota Land Cruiser V8 aliligeuza na kurudi uwanja wa ndege, mara gari zilizofuata nyuma, kwa kitendo kile nazo zilirudi hasa zile za usalama.

“Madam nini tena?” waziri wa ulinzi mheshimiwa Machura alimuuliza Madam S ambaye alimkuta nusu kachanganyikiwa akiongea peke yake. Akampa ule mkanda uliotoka katika saa yake, naye akausoma, akashika kichwa, akiwa anajua kinachoendelea akajifanya kuchanganyikiwa na hali hiyo. Walibaki wanahangaika akili zikiwa zimewaruka kwa kiasi Fulani, kizaazaa!

♠ ♠ ♠

Kamanda Amata alisoma kipande cha mwisho cha mpango hasi katika flash disk aliyoichukua kule valley View Hotel, kikionesha kuwa baada ya mauaji ya watu muhimu, wa mwisho kabisa ni Rais wa nchi ambaye atategewa bomu kwenye ndege yake itakayoruka tarehe 26 June 2003 saa tatu na nusu usiku, bomu hilo limepangwa kulipuka dakika arobaini na tano baada ya

ndege kuruka, lilikuwa limetegwa kwenye control box inayosambaza umeme katika ndege hiyo ya kisasa kabisa ambayo hakuna nyingine kama hiyo Afrika, kwa jinsi walivyofunga bomu hilo ilikuwa ni pale rubani anaporuhusu magurudumu kurudi ndani ndipo nalo linajiwasha na kuanza kuhesabu dakika 45 tu na kulipuka.

"Simama apo hapo!" sauti ya Jomse ilimuamuru Kamanda Amata. Meno ya mamba alimsogelea Amata ili amfunge katika kiti kilicho jirani hapo.

"Kaa chini usilete fujo, muda wetu umeisha wa kuwa nchini kwenu, dakika chache tutakuwa ndani ya nchi yetu" Jomse alimueleza Amata ambaye alishikwa na hasira kali, akihesabu dakika za bomu lile lililotegwa katika ndege ya Rais, hakujua kama itawezekana kuokoa janga hilo au la, alitamani kama yeye angekuwa pale uwanjani ahakikishe mwisho wake. Alipohakikisha amemfunga barabara, Meno ya mamba aliirejesha bastola yake kiunoni na kutembea hatua chache na kumsukasuka Isabel kwa mguu wake, Isabel hakutikisika.

Mara simu ya Jomse iliita

"*Mission clear*, popo ameruka, subiri majibu" Jomse alitoa cheko la dharau

"Kamanda Amata, sasa dunia itatikisika kwa hofu kuu kwa kusikia mlipuko mbaya wa ndege ya Rais wako, ha ha ha ha" alijigamba, "Sisi ndiyo wanamapinduzi, unakumbuka Rwanda na Burundi mwaka 1994, tulimtungua Rais Abiyarimana na

mwenzake Ndadaye!? Mliiona kama hadithi ee! Ni sisi na sasa tuko hapa Tanzania, kamwe hamuwezi kukomesha juhudi, nakuwekea TV hapa uone dakika 40 zijazo *breaking news*" sauti hiyo ilimkosesha raha Amata alitamani amrukie na kumg'ata ama kumeza kabisa kiumbe huyo. Waziwazi Amata alifura kwa hasira, akaanza kupumua kwa nguvu na kifua chake kipana kikipanda na kushuka, akiwatazama kwa macho ya hasira watu hawa wakati wanamuwekea TV mbele yake umbali wa mita kama saba hivi.

Jomse alichukua simu yake iliyokuwa mezani wakati huo na kubonyeza namba Fulani kisha akaweka sikioni.

"*Yes*. Hello, kutoka point A mission Clear, panga vikosi kuanza kazi mara moja pindi nikikupa taarifa" alikata simu na kuiweka mfukoni.

"Unasikia we mbwa, tayari majeshi ya waasi yameshakaa katima mapori ya Nyakanazi, na mengine yapo hapa Dar, tukitangaza tu nchi inapinduliwa dakika moja tu, na wewe ukishuhudia halafu utakuwa maiti, na yule bibi kizee wako muda si mrefu ataletwa hapa, na mtu wa kuwaua yuko Burundi anakuja, ha ha ha ha!" Jomse aliongea kwa daharau ya hali ya juu.

Kamanda Amata kwa nguvu zote alijinyanyua kitini na kukinyanyua kiti kwa miguu yake na kukirusha kwa kukipiga mbele, kumbe kiti kile kilikuwa hakijafungwa pamoja naye, kilinyanyuka kwa kasi na kutua kichwani kwa Meno ya mamba, akiwa sasa mikono yake iliyofungwa pamoja imebaki nyuma, alimuona Jomse

akija kwa kasi pale alipo, Kamanda Amata lijikunja kwa kuruka na kuipenyeza miguu yake ndani ya wigo wa mikono iliyofungwa kuelekea nyuma na sasa mikono ile ilikuwa mbele, alinyanyuka kwa kasi na kupiga double kick iliyotua kifuani mwa Jomse na kumpepesua hata bunduki yake kumtoka mikononi na kudondokea mbali, alipotua tu sakafuni kwa miguu miwili alipigwa mtama wa nguvu ambao ulimnyanyua juu na kabla hajatua aliichanua miguu yake na kuwatandika wote wawili kila mmoja teke la nguvu la mguu wake. Meno ya mamba alitema meno kadhaa.

Kamanda Amata alijiviriga kutoka pale alipokuwepo na kuiwahi bastola iliyokuwa chini, kabla hajafika alipigwa teke la sikio na kumfanya kupoteza uelekeo, alijigeuza chali na kumuona Jomse akiwa na shortgun mikononi mwake, Amata hakujali, akiwa bado yupo chini alimpiga Jomse teke la nguvu nyuma ya vivigino lililomfanya aanguke chali kama mzigo kabla hajatulia, mguu uleule ulitua juu ya tumbo la Jomse, ukelele wa maumivu ulisikika, wakati Meno ya mamba akija kwa kasi kumkabili Kamanda Amata ambaye alikuwa amelala pale chini, alishuhudia kichwa cha Meno ya mamba kikitawanyika vibaya na mwili wake kurushwa mita kadhaa ukiwa hauna uhai, hatari!

Gina, akiwa bado hajasusha mkono wake wenye bastola yake aina ya Makarov, bastola ya kirussia iliyotengenezwa mwaka 1949 na bwana Nikolay Makarov na kuanza kutumika rasmi mwaka 1951 ilishafanya kazi yake kama ilivyoamuriwa.

“Freeze, bastard” Gina alimuamuru Jomse aliyekuwa akijaribu kujitutumua pale chini, Jomse alijifanya asikii na kutaka kuichukua ile short gun mara Makarov ya Gina ilicheua tena na kuvunja mkono wa Jomse, yowe la maumivu lilimtoka.

Gina alitoa ishara ya mkono kama anayeita kitu, mara polisi kadhaa waliingia ndani ya jengo lile wakiongozwa na Inspekta Simbeye, walimfungua kamanda Amata na kumchukua Isabel baada ya kugundua kuwa bado alikuwa na uhai, haraka sana wakamkimbiza Hospitali ya jeshi la wananchi Lugalo.

“Naomba muhakikishe huyu mtu anafika makao makuu ya polisi leo kwa mahojiano hata kama ana maumivu ya mkono sijali, mimi naelekea uwanja wa ndege, kuna muasi mmoja bado hajakamatwa na hayupo hapa” kamanda Amata alitoa amri huku akiingia katika gari ile iliyomleta, Toyota Altezza na kuigeuza kwa kasi na kuondoka eneo lile kuelekea uwanja wa ndege.

Kwa maelekezo ya Amata, Inspekta Simbeye alitoa amri kwa redio call maeneo muhimu yote yawekwe ulinzi ili kumnasa muasi huyo, kuanzia stendi ya Ubungo, Posta eneo zinaoondokea boti za Zanzibar, Uwanja wa ndege wenyewe. Mji wa Dar es salaam ulijawa na askari kanzu kufanya msako huo, mawasiliano ya redio za polisi muda wote yaligubikwa na habari za wapi ameonekana au wapi kuna dalili. Maelekezo machache waliyoyapata jinsi alivyo

yaliwafanya watu wa mtindo huo kuishi kwa shida usiku huo

♠ ♠ ♠

Tonton akiwa bado hajui kilichompata Jomse na Meno ya Mamba bado alikuwa katika harakati za kumsaka Madam S, ama awe hai au maiti, aliiangalia saa yake aliona inakaribia saa nne za usiku, akiwa amepaki gari yake katika njia panda ya uwanja wa ndege terminal one, bomu la mkono aina ya grunet lilikuwa juu ya kiti cha gari yake huku akijifanya anatengeneza tairi akisubiri msafara ule wa wanausalama utoke kule uwanja wa ndege ili afanye yake. Alikuwa hakika amejizatiti kwa kila hali, walktalk yake iliita akaichukua na kupata maelekezo Fulani kisha akairudisha kitini na kusubiri kidogo akiwa ndani ya overall. Akiwa katika kushangaashangaa mara mbele yake ilipita Toyota Altezza nyeusi kwa kasi ya ajabu ikielekea uwanja wa ndege, Ton aliiangalia kwa makini akaingiza mkono mfukoni na kuinua simu yake na kubofya namba Fulani na kuiweka simu yake sikioni, lakini simu ile haikujibiwa, aliipiga tena hali ilikuwa ileile, akachanganyikiwa afanyeje maana aliona Jomse kaelekea airport na gari yake sasa akawa katika njia panda kama alipo, amfuate au asubiri pale kadiri ya maelekezo aliyoyapata, alizunguka huku na huku akiwa kama mtu aliyechanganyikiwa.

♠ ♠ ♠

**M**abishano makali yalikuwa kati ya Madam S na waziri wa ulinzi, Madam S aling'ang'ani ndege ile ishuke haraka iwezekenavyo wakati waziri wa ulinzi akisema kuwa hawana la kufanya ndege imeshakwenda hakuna jinsi ya kuiokoa. Akiangalia simu yake dakika thelathini zilikuwa zimekatika tangu ndege ile iache ardhi.

Matairi ya Toyota Altezza zililalamika katika lami Amata alipokuwa akiingia uwanjani pale,

"Vipi Madam? Bado nimewaambia ndege ile ina bomu itue hapa tufanye kinachowezekana, ah!" Amata aliingia kwenye gari yake na kuondoka kwa kasi kuelekea katika mnara wa kuongozea ndege, alipaki gari na kukwea ngazi huku akikimbia, aliingia akiwa anahema.

"Samahani, naitwa Kamanda Amata kutoka idara ya usalama wa taifa kitengo maalumu," alitoa kitambulisho na kuwaonesha maofisa hao.

"Tukusaidie nini Kamanda?"

"Naomba muamuru ndege ya Rais irudi haraka sana, bila kuchelewa"

"Sasa unajua...." Mdada mmoja alitaka kutoa hoja zake za kitaaluma.

"Unapoteza muda, harakaaaaa..." Amata alimkatisha kwa ukelele na kutaka kumkata kibao.

“5H-ONE, Gulfsream Aerospace G-V SP G550, kitendo bila kuchelewa unaombwa kuirudisha ndege uwanjani kwa sababu za kiusalama”

“5H-ONE, Gulfsream Aerospace G-V SP G550, Captain Maga Junior amekusikia, naomba njia”

Lugha zaidi za kitaalamu zilifanyika na ndege ile ilikunja kipande cha mkia wake na kuelemea upande mmoja ikigeuka kurudi ilikotoka.

Simu katika chumba cha rubani iliita, captain aliipokea na kujibu maswali aliyoulizwa na wana usalama waliokuwa kwenye msafara wa Rais kuelekea New York, wote wakatulia vitini wakisubiri kujua nini kilijiri.

“Kama Kamanda Amata ameamuru, basi kuna jambo.” Mmoja wao alimueleza mwingine, kijasho chembamba kiliwatiririka walio ndani ya ndege hiyo.

♠ ♠ ♠

Gari za zima moto na zile za uokoaji tayari zilikuwa zimewasili katika eneo la uwanja wa ndege wa jeshi tayari kukabili lolote, makomandoo kadhaa wa jeshi walikuwa tayari eneo lile, kwa ujumla hali ilikuwa tete uwanjani pale, ndege za abiria zilizotakiwa kuruka na kutua zilizuiliwa kwa muda ili anga ibaki nyeupe na kuziacha nyota na mbala mwezi tu.

Barabara ya Nyerere itokayo uwanja wa ndege ilifungwa na kubaki haina gari hata moja ili kuharakisha huduma za haraka.

Gari mbili za zimamoto zilikuwa mwanzo wa barabara itumikayo kwa kuruka au kutua zikiwa tayari kabisa kwa kazi hiyo.

Kamanda Amata akiwa na Madam S, waliangalia saa zao kwa pamoja ilikuwa ni saa nne usiku na dakika moja, zilibaki dakika kumi na nne tu ili bomu lile lililotegwa lifanye kazi yake, akili ya Amata ilikuwa ikismama kila wakati, alijiuliza kwa nini wamalize kazi yote halafu iwaharibikie mwisho, haikuingia akilini. Kwa mbali waliona taa ziking'aa upande wa Kipawa, kuashiria kuwa sasa kazi ya hatari inaamka, kila mtu alijipanga sehemu yake tayari kwa kazi hiyo, kamanda Amata alisogea karibu na wale makomandoo wa jeshi tayari kwa kazi ya uokoaji.

Saa nne na dakika sita, 5H-ONE ndege ya kisasa ya serikali kwa matumizi ya Rais, ikiwa inaongozwa na rubani mzoefu kwa kazi hiyo Captain Maga Junior, ilikanyaga ardhi ya Dar es salaam na kwa kasi ya ajabu ilipitiliza mpaka maeneo ya Kipunguni kisha kukunja kona na kurudi pale uwanja wa jeshi si kwa mwendo ule wa maringo tena, bali kwa mwendo wa kasi kidogo, gari za zima moto zilishaizunguka alkadhalika na zile za wagonjwa zilikuwa pale. Milango ya ndege ilifunguliwa na ngazi maalumu ya plastiki linalojazwa upepo lilifyatuliwa na mtu wa kwanza kutolewa ni mheshimiwa Rais, na moja kwa moja alichukuliwa na kuondolewa eneo lile kwa gari maalum, kisha wakafuatia wengine.

Kamanda Amata alikuwa tayari katika chumba chenye mitambo ya umeme ya ndege hiyo, *control room*, bomu lile lilikuwa limefungwa sambamba na na nyaya zinazosambaza umeme katika ndege ile, nyaya zaidi ya mia mbili ziliingia na kutoka eneo lile na nyaya sita ziliingia kwenye lile bomu na kutokea upande wapili kisha kufungwa katika fyuzi fulanifulani. Kijasho chembamba kilimtoka Amata hakujua nini cha kufanya, saa ya bomu lile ilisoma bado dakika mbili ili ifike muda wake. Akiwa na koleo ya kukata nyaya ya umeme alishindwa waya upi auanze, mwekundu au mweusi, wa njano au buluu au ule mweupe, kweli alichanganyikiwa.

Kawaida huwa kuna nyaya tatu lakini kwa nini bomu hili lina nyaya sita, hilo ni jambo lililomchanganya, alijaribu kukumbuka kanuni aliyofundishwa alipokuwa mafunzoni huko Cuba jinsi ya kutegua mabomu lakini alijikuta ameisahau. Saa ya lile bomu ilionesha kuwa imebaki dakika moja na sekunde kadhaa, Amata alikuwa ameloa jasho mikono ikimtetemeka, sasa alioamua lolote na liwe, maana ukataji wa nyaya hizo unatakiwa uende kwa mpangilio maalum na ukikose utafanya muda wa bomu lile uishe haraka na kusababisha mlipuko. Alitazama haraka haraka na kuugundua waya wa kwanza ***primer***, akaukata, bado saa ile iliendelea kwa mwendo wa kawaida, akatafuta waya wa pili waya wa ***reactor***, akaupata na kuukata, sasa zilibaki nyaya nne, alijihisi kama kujikojolea maana saa ya bomu lile ilisoma bado

sekunde hamsini, hamna muda wa kufikiria iliyobaki ni kukata zote.

♠ ♠ ♠

Katika uwanja ule ukimya ulitawala usiku ule utafikiri hakuna mtu, ni mingurumo ya gari tu iliyosikika lakini binadamu wote walikuwa kimya wakasubiri hatima ya ndege hiyo ya gharama iliyozua makelele kutoka kwa vyama vya upinzani kwamba kuinunua ni kupoteza hele za Watanzania lakini aliyekuwa nadarakani wakati huo hakujali aliinunua na sasa ndiyo hiyo ipo hatarini pamoja na kamanda Amata aliyepo ndani yake, kila mtu alisali kwa dini yake, Ee Mungu iokoe Tanzania. Madam S alibubujikwa na machozi akiwa anauma meno hakujua afanye nini alibaki kutazama tu saa yake iliyomwambia bado sekunde takribani kumi, hakuna Amata wala dalili za kuonekana kwake nje. Alipogeuka nyuma hakumuona waziri wa ulinzi, ambaye muda wote alikuwa hapo nyuma yake. Hakulifuatilia hilo macho yake yote yalikuwa juu ya Amata na ile ndege ya Rais yenye thamani kubwa kabisa Africa *'Airforce one ya Tanzania'*.

♠ ♠ ♠

**K**amanda Amata, huku mikono ikimtetemeka alikata waya wa kwanza kati ya zile nne, saa bado

inasoma, wa pili, saa bado inasoma, akageuza badala ya kukata ule wa tatu akahamia wane akaona labda ameikosea ile series akakata wa nne, saa bado inakwenda sasa ikaongeza kasi bila kufikiri akaubana ule wa tatu na alipoukata tu ***'Ignition Timer'*** saa ile ilisimama na kuacha kutoa ule mlio wake ikiwa imebaki sekunde moja kulipuka, saa ile ilisimama ikiwa imejiandika 00:00:01.

Amata alishusha pumzi ndefu, alijishika mikono kifuani moyo wake ulikuwa ukienda mbio, alijihisi kama mtu aliyetoka mautini.

Huko nje, ilipobaki sekunde tano makomandoo wa jeshi waliamuru watu wote kulala chini, na zilipokwisha bado hakuna mlipuko uliotokea. Walianza kuinua vichwa mmoja baada ya mwingine wakitanguliw na kamanda wao.

Madam S sasa alitokwa na machozi ya furaha alipomuona Amata akitoka katika ule mlango wa ndege mkononi akiwa amekamata lile bomu ambalo limeshindikana kulipuka.

Hakuna aliyeamini anachokiona, waandishi waliokuwa wamesimama mbali walisogea na kupata picha za shujaa huyu na kumhoji maswali mbalimbali, ilikuwa fujo uwanjani hapo.

Kamanda Amata aliingizwa kwenye gari ya deraya ya kijeshi na kufungiwa milango na gari ile iliondoka eneo lile.

♠♠♠

Gari aina ya Toyota Altezza ilisimama karibu kabisa na ile gari ndogo iliyofanywa kama imeharibika tairi, Tonton alitoka kwenye kichaka cha michongoma na kuisogelea kwa hadhari kubwa kwa maana aliijua ile gari ilikuwa ikitumika na Jomse.

“Hali si nzuri tuondoke haraka,” waziri wa ulinzi bwana Machura alimwambia Tonton na wote wakaingia ndani gari hiyo na kutokomea pande za Gongo la mboto.

“Mzee vipi?” Ton aliuliza

“Mambo si mambo kijana, hapa ni kujiokoa tu, na jinsi ninavyojua nchi hii si ajabu wameshabana kona zote”

“Oh God” Ton alisikitika. Gari ile iliendeshwa kwa kasi sana, walipita Pugu na kufika Chanika kisha mvuti mpaka mitaa ya Samvula Chole.

♠ ♠ ♠

“Madam S, naomba uombe kibali cha kumuweka chini ya ulinzi mheshimiwa Machura” Amata alimueleza madam S huku akifyatua kiti kujilaza.

“Kwa nini?”

“Naomba utekeleze hilo haraka madam, wewe ndiye mwenye sauti, si mimi.”

Bila kupinga madam S alipiga simu kwa mkuu wa polisi msaidizi baada ya kifo cha IGP na kuomba kibali hicho, bila kipingamizi kibali kilitolewa. Defender ya

polisi ikiwa na polisi wenye silaha nyumbani kwa Machura, waziri wa ulinzi, walipigwa na butwaa nyumba ilikuwa tupu, hakuna mtu, si familia wala yeye mwenyewe, ni mlinzi tu ndiye alikuwa amebaki pale. Maelezo waliyoyapata kutoka kwa mlinzi yule yaliwakata maini, walielezwa kuwa familia ya Machura iliondoka yote jana asubuhi, lakini haikujulikana ni wapi ilielekea, taarifa ilifikishwa kwa haraka mahali husika.

Akiwa njiani kuelekea kituo cha polisi kati, kamanda Amata aliipata taarifa ile kupitia simu iliyopigwa kwa madam S.

“Shiiiit” Amata aliongea kwa hasira, “Hawezi kutukimbia hata kidogo,” alichomoa simu yake mfukoni na kubofya namba fulani, kisha akaiweka sikioni.

“Hello … sio kivile… sasa sikia naomba uwasiliane na watu wa uwanja wa ndege ikiwezekana upate orodha ya abiria walioondoka jana kwa kila ya kila kampuni, haraka tafadhali” akakata simu mara tu baada ya kumaliza kuongea.

Madam S aliipaki gari yake pembeni kidogo ya kituo cha polisi, haraka Amata alishuka na wote wawili wakaelekea ndani.

“Upande huu tafadhali” afande aliyekuwa kaunta aliwaelekeza kuwa waingie kushoto, huko walimkuta Inspekta Simbeye akiwa amefura kwelikweli na Jomse akiwa kwenye kiti cha chuma akiwa na hali mbaya.

“Bastard!” Madam S aling’aka kwa hasira alipomuona Jomse, “Ulifikiri hii nchi ni ya baba yako?!, *‘Mimi mwanamapinduzi, mxiuuuuui, kawapindue hao hao’*” alimuiga kwa sauti ya kubana pua.
Jomse hakuweza hata kuinua kichwa kwa jinsi alivyokuwa na maumivu makali, aliisikia tu sauti ya mwanamama yule aliyempa kibarua kigumu kule ofisini kwake. Wakiwa katika majadiliano hayo waligundua kuwa Jomse hali yake ilizidi kuwa mbaya.

“Hebu pelekeni Muhimbili, hakikisheni anapona ili atumikie kifungo chake ndani ya nchi hii” Amata alisema hayo na kutoka akifuatiwa na madam S. Baada ya kupata ripoti ya kuwa Isabel tayari yuko hospitali ya jeshi, Amata na madam S walifarijika, wakaagana na Inspekta Simbeye “Kama kuna lolote basi tutakutaarifu”, kisha wakaondoka zao.

Simu ya Amata ikaita.

“Yes, niambie…”

“*Tayari nimepata orodha zote, amri nyingine tafadhali”* sauti ya kikakamavu ya Gina ilisikika.

“Vizuri, msichana mrembo, tukutane ofisini sasa hivi, bila kuchelewa.” Dakika tano tu wote walikuwa ofisini pamoja na madam S, Amata akiwa na madam S walizipitia orodha zote, wakiwa karibu na kukata tamaa, chati ya mwisho kabisa ya shirika la ndege la Kenya ndipo waligundua majina ya familia ya Machura, ilionesha wametoka Dar kwenda Kigali kupitia Nairobi.

Madam S alitikisa kichwa chake juu chini kuonesha amegundua kitu.

“Madam, mheshimiwa Machura, waziri wa ulinzi anahusika kwa kiasi kikubwa sana katika kuandaa mapinduzi haya ushahidi upo, kwa nini aondoshe familia yake? Alikwishajua kuwa *kitakaponuka* familia yake iwe salama wakati Watanzania wanateketea”

Madam S alionekana kushikwa na hasira mpaka paji la uso wake likawa na mikunjomikunjo kadhaa, alipiga ngumi mezani na kujishika kiuno akimwangalia Amata.

“Hakuna kuchelewa, mpigie simu Simbeye msako uanze mpaka atiwe nguvuni kabla jua kuchomoza, kisha sisi twende kwa mzee ametuita haraka sana”

Dakika chache tu nchi nzima ilikuwa kwenye tahadhari kubwa hasa sehemu za mipakani ambako ilisemekana kuwa tayari kuliandaliwa majeshi ya waasi ambao walipata mafunzo maalumu katika misitu ya Nyakanazi, mpakani kabisa mwa Tanzania na Burundi, operesheni maalum ikatangazwa na kwa kuwa vijana wetu wa JWTZ walikuwa makini kazi hiyo haikuwa na mzaha hata kidogo, huku vijana wa polisi wakiwa wamelibana jiji la Dar es salaam katika kila uchochoro unaotoka nje ya jiji hilo ili Machura asitoroke.

♠ ♠ ♠

**M**heshimiwa Rais, alionekana kuchanganyikiwa kwa namna Fulani, hakuamini ni nini kinachoendelea. Akiwa amekaa kwenye meza yake kubwa na ile ya mbele walikuwapo waziri wa mambo ya ndani, jeshi la

kujenga taifa, mkuu wa kitengo maalum usalama wa taifa madam S, na pembeni yake alikuwapo Kamanda Amata, kiti kimoja kilikuwa wazi.

Mheshimiwa Rais aliwaangalia wote kwa zamu.

“Asante sana kijana pamoja na boss wako pale, si kwamba mmeniokoa mimi bali mmeliokoa Taifa, ambapo lingeingia kwenye mapinduzi na mauaji ya kimbali ambayo yangesababishwa na watu wachache wenye uchu wa kutawala dunia” alinyanyuka na kuwapa mikono, “Naomba nipate taarifa fupi ya yote haya ili sasa tujue kama tumemaliza au la” macho yote ya waliokuwa kikaoni yakaelekea kwa madam S na kamanda Amata.

Taarifa fupi ilitolewa na kila mtu katika kikao kile alibaki mdomo wazi.

Mheshimiwa Rais alielezwa kila kitu na hatua zilizochukuliwa na vyombo mbalimbali vya usalama nchini, kwa hatua hizo alitoa pongezi za dhati kwa wote, lakini kama kuna jambo lilimuuzi ni juu ya waziri wa ulinzi, hakuamini kabisa kama mzee huyo aliyeheshimika sana angeweza kuingia katika wimbi hilo la kupanga mapinduzi. Mheshimiwa alitikisa kichwa kwa masikitiko.

“Naomba kwa udi na uvumba, akamatwe ili aje ajibu maswali yake” Rais alitoa msisitizo.

## Miaka mine nyuma
## Kinshasa-DRC

**M**kutano uliowakutanisha mawaziri wa ulinzi wote wa nchi za SADC ulifanyikia katika hoteli ya kimataifa ya Hilton mjini Kinshasa. Kama kawaida ya mikutano hiyo ilikutanisha watu wa aina mbalimbali, Tanzania iliwakilishwa na mheshimiwa Godfrey Francis Machura mzaliwa wa Kigoma, ambaye kiasili kabisa wazazi wake walihamia Kigoma wakitokea Congo, yeye alisoma na kujenga maisha yake yote hapo hata kujiunga na siasa katika chama cha TANU enzi hizo mpaka sasa CCM.

Jioni moja katika hoteli hiyo alikutana na wageni asiyowatarajia, wanaume watatu wa kizungu, mmoja akiwa kama chotara, pamoja na mwanamama mmoja wa Kiafrika mwenye maringo ya kuvutia mwanaume yeyote rijali.

Walikuwa na sera kubwa moja tu, kumhadaa mheshimiwa huyu ili kuweza kuipenya ngome ya kiulinzi ya Tanzania na kuweza kutekeleza mpango wao dhalimu walioudhamiria kama walivyofanya katika nchi kadhaa hapa Afrika. Kwa pesa nyingi walizo nazo, walimuahidi yeye mwenyewe kupata utajiri wa hali ya juu kama hilo lingetekelezwa.

Baada ya mkutano ule, mheshimiwa Machura hakuishiwa na ziara za mara kwa mara kwenda Kigali na Bujumbura, huko ndiko walikokuwa wakipanga huo *Mpango Hasi*. Ilishapangwa kuwa pindi tu mambo

yakiwa sawa yeye na familia yake wangeenda kuishi Kigali ambako alishapewa nyumba kubwa na yenye hadhi. Tamaa ya pesa iliufanya moyo wake kuwa tayari kulisaliti taifa lililomlea na kumpa njia ya maisha, hakika shukrani ya punda ni mateke.

♠ ♠ ♠

Kama kuna habari iliyomfariji mheshimiwa Rais katika kikao kile ni juu ya msichana Isabel.

"Bado taifa lina wazalendo, kama msichana huyu angepuuza juu ya hilo nini kingalitokea?!" aliuliza kwa mshangao.

Wote walibaki kimya, hakuna hata aliyekohoa katika kkao kile, kwa kila mmoja wazo tofauti lilikuwa likipita kichwani mwake akiwaza hiki na kuwazua kile kule. Kila mtu kwa muda huo alikuwa amekodolea ukutani ambapo kwa kutumia *projector* waliweza kuusoma mpango hasi hatua moja baada ya nyingine. Na walipomaliza kusoma kila mtu alishika tama kwa msikitiko, kimya kikatawala.

Baada ya kimya cha muda mheshimiwa aliuvunja ukimya huo "Sasa naomba turudi kwenye majukumu, halafu nitwaomba tena tukutane baada ya mambo haya kutulia, siku za usoni" alimaliza na kunyanyuka, wote walinyanyuka na kutoa heshima zao kisha kupeana mikono na kuondoka eneo hilo nyeti.

## Kigali – Rwanda

**C**HIBA aliipaki gari yake katika maegesho, kabla hajashuka katika gari hiyo aliiweka tayari bastola yake na kuibana sawia katika mkanda maalumu uliofungwa kwa kifuani, aliivaa miwani yake myeusi yenye uwezo wa kuona nyuma na kurekodi sauti ya mtu anayeongea naye. Alipoona kuwa amejikamilisha aliinyanyua simu yake ya upepo na kuwasiliana na watu walio nje kidogo ya maegesho hayo ambao walikuja kwa kazi moja tu, kazi muhimu. Alipoona kuwa wako tayari, aliteremka na kuliendea ghorofa moja wapo kati ya mengi ya yaliyojengwa eneo hilo kwa madhumuni ya kupangisha watu, bila kujua kuwa wengine wanaowapangisha hawana utu hata kidogo. Alikwea ngazi kwa kukimbia kidogo mpaka ghorofa ya pili, milango mingi ilimzunguka aliinua macho na kusoma vijinamba vilivyobandikwa milangoni.

*'B 6T'*, akatikisa kichwa kuonesha kuwa ni sahihi kama alivyoelekezwa, alichomoa earphone yake na kuipachika sikioni kwa minajiri ya kuwasiliana na wale walo nje, kisha akabonyeza kitufe chekundu kilichopo mlangoni hapo. Sekunde kadhaa, mlango ulifunguliwa na msichana wa kadirio la umri wa miaka ishirini alijitokeza kichwa tu.

"Karibu, nikusaidie nini?" alimkaribisha Chiba kwa lugha ya Kinyarwanda. Msichana huyu mwenye mwili mwembamba na shingo ndefu alitoa tabasamu ambalo lilimfanya Chiba atulie kwanza baada ya *network* zake

kukatika ghafla kwa kukutana na binti mwenye shingo ya upanga.

“Naitwa Tonton, nimemkuta madam Rose?” Chiba aliongopa jina.

Yule msichana alisita kidogo akamwangalia kijana huyo ambaye mkono mmoja wa kulia ulikuwa ndani ya koti lake kana kwamba anataka kutoa hela katika mfuko wake wa shati.

“Hayupo,” alijibu msichana yule huku akirudisha mlango kuufunga, Chiba aliweka mguu na kuuzuia.

“Msichana! Nina shida ya muhimu, nahitaji kumuona madam Rose sasa hivi”

“Nimekwambia hayupo”

“Amekwenda wapi?”

“Mi sijui, nimemuona akiondoka tu.” Chiba alibaki hana la kufanya, alitafakari kwa muda kidogo na kupata uamuzi.

“Ok” akageuka kuondoka, hamad, domo la bastola lilikuwa likimtazama usoni pindi tu alipogeuka.

“Tulia! Toa bastola yako” amri ilitoka kwa mtu huyo chotara, Frank, aliyekuwa tayari katika nyumba hiyo. Chiba aliitoa bastola yake na kuiweka chini, kisha yule msichana akaichukua.

“Ingia ndani,” amri ya pili ilifuata na Chiba akatii.

Katika sebule ile kubwa Chiba aliketishwa kwenye moja ya sofa zilizo hapo na Frank akaketi kwenye sofa lingine kwa mtindo wa kutazamana.

“Mmemuua Mandi, na wengine, mmeona haitoshi sasa mmekuja hadi huku, mnajifanya FBI au

Interpool?" Frank alimuuliza Chiba huku akinyooshea ile bastola iliyoonekana wazi haina masikhara.

"Zaidi ya hapo" Chiba alijibu kwa dharau. Frank alichukizwa na jibu lile na kufayatua risasi moja iliyochimba kwenye sofa lile sentimeta chache katikati ya mapaja yake, Chiba alitetemeka na kijasho cha ghafla kilimtoka kwa mbali.

"Ha ha ha ha kumbe unaogopa kufa, ha ha ha ha!" Frank alicheka kwa dharau, "Kwa taarifa yako Madam Rose, hivi tunavyozungumza bado dakika kumi tu apae kuelekea Belgium kwa mapumziko, madam ni *untouchable,*" alipokuwa akisema hayo Chiba hakupoteza muda, alijisukuma kwa nguvu pamoja na lile sofa na kupindukia upande wa pili, sofa lile likamfunika, kitendo hicho cha haraka kilimchanganya Frank, akaweka vizuri bastola yake na kufyatua risasi kadhaa kwenye sofa lile lakini tayari Chiba alishaliacha sofa lile peke yake. Hakuwa na silaha, alinyanyua bilauri iliyokuwa mezani na kuirusha, moja kwa moja ilitua katika uso wa Frank na kumpoteza malengo, yule msichana kule jikoni alikimbilia sebuleni ndipo alipodakwa na Chiba na kuwekwa ngao, huku Chiba akiwa tayari na kisu kutoka mikononi mwa msichana yule.

"Weka bastola chini, au la nakata koromeo la Malaya huyu" Chiba aliongea kwa gadhabu wakati huo tayari matone ya damu yalioneka yakidondoka sakafuni, kisu kile kilianza kuikata ngozi ya juu ya shingo la msichana yule. Frank hakuwa na ujanja

aliiweka bastola chini, kisha Chiba alimuamuru kutoka eneo lile na kuuelekea mlango, naye akatii. Chiba hakuujua ujanja wa Frank, alipoufikia mlango kitendo bila kuchelewa aliichomoa bastola iliyokuwa upande wa nyuma wa suruali yake na kufyatua risasi mbili mfululizo, la, Chiba alijitupa upande wa pili na kuikamata bastola aliyoiacha Frank. Risasi za Frank ziliishia kifuani mwa yule msichana, akajibwaga chini akiwa marehemu. Frank aliduwaa alionekana wazi kachanganyikiwa kwa kitendo kile.

"Roooooosssseeee! Madam Roooooseeeee" alilia kwa uchungu, ndipo Chiba alipogundua kuwa kumbe yule alikuwa ndiye madam Rose lakini alipata shaka kutokana na picha aliyopewa ofisini. *'Ni yeye au si yeye?'* alijiuliza, mara akakumbuka kuwa yupo katika mapambano.

"Freeze" alimpigia kelele Frank, "Weka bastola chini" alimuamuru na Frank akatii. Mara mlano ukafunguliwa na watu wawili wakaingia, kwa ishara waliyopewa na Chiba wakamtia pingu Frank.

"Tuambie huyu ni nani?" Chiba alimuuliza Frank huku akielekeza mkono wake kwa yule marehemu msichana. Frank hakujibu alibaki kumwangalia tu usoni, "Nakuuliza wewe!" Chiba aling'aka lakini alichokipata ni kutemewa mate usoni kitendo kilichomuudhi sana, kwa hasira alimvamia Frank na kumchoma na peni ya chuma eneo la shingoni, Frank alitoa yowe la uchungu.

“Sema, madam Rose yuko wapi?” Chiba aliuliza tena. Lakini kabla hajapata jibu simu iliyokuwa juu ya kikabati kidogo ikaita kwa sauti kali, Chiba akaiendea na kuinyanyua *‘madame Rose’* ilijiandika kwenye kioo, Chiba aliichukua na kumpelekea Frank.

“Ongea naye, kwa lugha yenu ya kawaida, weak loud speaker wote tusikie mwambia aje hapa haraka, ukigeuza neno nautawanya ubongo wako” Chiba alimaliza na kutegua kiguu cha usalama cha bastola yake na kuruhusu risasi kuingia chemba kisha akainyooshea kwa Frank usawa wa paji la uso.

“Yes, Madame” Frank alipokea

“Hey Francoise, unikute hapa Kichukiro highway, nimeshapata ndege ya kukodi tuondoke joni hii”

“Sawa madame lakini tuna…”

“…Mna nini Francoise, mambo yameharibika kama kuna kinachoshindikana acha njoo wewe”

“Eh madam hali ya dada ako ni mbaya uje mara moja” mara simu ikakatika. Frank akanyanyuliwa na kuwekwa juu ya sofa kubwa pamoja na wale watu wawili, wakawasha television na kusubiri windo lao.

Ama kweli ndege mjanja hunasa kwenye tundu bovu, madam Rose aliingia kwenye maegesho kwa kasi ya hatari na gari yake aina ya Rambolghin, akapaki na kutembea harakaharaka kuelekea ngazi za jengo hilo, hakushtuka kabisa alipompita mwanaume mmoja katika ngazi hizo akiongea kwa simu huku akicheka, moja kwa moja aliuendea mlango na kuufungua kuingia ndani, nusura azimie baada ya kulakiwa na

mwili wa marehemu uliyolala bila kuguswa kwenye dimbwi la damu mbichi.

“Uuuuuuiiiiiii !” alipiga ukelele wa mshtuko na kujikuta akidakwa na watu asiyowajua na kutiwa pingu, kisha kuwekwa juu ya sofa lingine na kumuona swahiba wake Frank akiwa amelowa damu katika shati lake.

“Idara ya usalama wa taifa Tanzania kushirikiana na idara kama hiyo ya nchini Rwanda tunawaweka chini ya ulinzi kwa jaribio la kufanya mapinduzi huko Tanzania.” Madam Rose alishindwa afanye nini alibaki mdomo wazi, kapatikana. Hakuamini jinsi alivyonasa kwenye mtego wakijinga wakati amekwishakwepa mbinu nyingi za watu kama hawa sehemu mbalimbali za ulimwengu.

Bila ubishi, waliongoza chini na gari maalum yenye vyoo vyeusi na vinene visivyopitisha risasi lilifika hapo na kuwapakia.

“Mnatupeleka wapi?” madam Rose aliuliza.

“Hupaswi kujua, utaona ukifika” Chiba alimjibu. Safari hiyo ikaishia uwanja wa ndege, wakiwa na soksi katika vichwa vyao hawakuweza kuona hata wapi wanaelekea, walipakiwa kwenye ndege maalum na safari ya kwenda Dar es salaam ilichukua nafasi yak echini TSA namba 2, Chiba wa Chiba.

♠ ♠ ♠

“Ina maana hamnijui mimi? Mbona mnaleta mambo ya ajabu?” Machura aliongea kwa hasira aliposimamishwa na askari wa checkpoint maeneo ya Igumbilo, Iringa. Alikuwa akijaribu kutoroka kwa kutumia njia hiyo mpaka Mbeya ambako angeweza kuingia nchi jirani lakini alipofika hapo check point gari yake haikuwa na budi kusimama kutokana na mageti yaliyowekwa hapo kuzuia njia. Ilikuwa ni saa nane usiku, kibaridi kikali kikipuliza.

“Nitapiga simu kwa RPC wenu na ninyi wote mtimuliwe kazi” aliendelea kung’aka huku akiwa anazungukazunguka huku na kule. Mabishano yalipokuwa yamezidi, Machura alipiga simu kwa RPC Kamuhanda wa Iringa, kweli akili ni nywele. RPC Kamuhanda aliona simu yake ikiwakawaka alipoiinua kwenye kioo alikuta jina la mheshimiwa mkubwa serikalini, akaitazama kisha akaiweka sikioni na kuipokea.

“Hello mheshimiwa waziri …”

“…Yes, .. a a a … Kamanda, vijana wako wananizuia njia hapa Igumbilo, hawajui kama nipo katika majukumu ya kiserikali? Naomba uwaamuru haraka waniruhusu kupita na kisha hawa wote walio zamu sasa hivi wachukuliwe hatua za kinidhamu”

“Ok, naomba ngoja niwapigie mara moja, hawana nidhamu kabisa kwa nini wakuzuie, wana kigezo gani? Lazima niwaadabishe,” RPC Kamuhanda aliikata simu ya Machura na kuivuta simu yake ya upepo tayari kutoa taarifa hiyo.

“Na mtaona sasa…ninyi hamjui kuwa mimi namuwakilisha Rais!” alimaliza kuongea huku akiingia katika gari yake.

“Vipi?” Ton aliuliza.

“…*Check point* Igumbilo, iruhusu gari ya mheshimiwa ipite mara moja ni amri, ova”

“….Tumekusoma, tunatekeleza, ova”

Geti likafunguliwa na gari ile ikapita kuendelea na safari, huku Machura akiwaoneshea kidole cha kati askari wale.

Karibu kabisa na njia panda ya kupandishia Iringa mjini, Land Rover Defender ya kituo cha polisi Iringa ilisimama katikati ya barabara ikwa imewasha taa zote full, juu ikiwa na vijana wawili wenye SMG na chini kulikuwa na vijana wanne wenye silaha pia. Ton aliendesha kwa mwendo wa taratibu,

“Aaaggghhh! Shit, nini tena!” Machura alipiga kelele huku akipigapiga mikono yake kwenye mapaja yake kwa hasira.

“Unaombwa kujisalimisha, wewe pamoja na uliyekuwa naye garini” sauti ilisikika kutoka nyuma, Machura alipogeuka alikuta Land Cruiser ya buluu ya polisi ikiwa nyuma yao, mbio za sakafuni huishia ukingoni.

“Unaombwa kujisalimisah, kwa kutoka nje ya gari hiyo mikono hewani, tii sheria bila shuruti” sauti ile ilirudia tena kutoka kwenye *megaphone.*

“Napambana!” Ton alimueleza Machura huku akimuonesha bomu la kurushwa kwa mkono.

“Ha ha ha ha…” sawa kijana umejiandaa vyema nakuaminia.

Ton alifungua mlango na kutoka nje huku mikono ikiwa hewani lakini ilikuwa ni vigumu kumgundua kama kashika kitu mkononi, walipotaka kumfuata alirusha bomu lile kwenye Land cruiser na kishindo kikubwa kilisikika, ile Cruiser ikanyanyuliwa kama box tupu lipeperushwavyo na kimbunga, hali ya mkanganyiko ilitwaa nafasi badala ya utulivu, Ton na bastola yake mkononi alijaribu kuwalenga polisi wale, kwa shabaha yake nzuri aliweza kumpata wa juu katika defender iliyosimama upande wa pili. Machura alishindwa kuvumilia alitoka garini na bastola mkononi akijaribu kufyatua hewani huku akijitahidi kukimbia lakini tumbo lilimzidi uzito.

Moshi ukiwa umetapakaa kila mahali, ving’ola vya gari za faya na polisi vilisikika kutoka Iringa mjini. Machura alimshuhudia Tonton akichakazwa kwa risasi kutoka kwa polisi aliyefika na pikipiki, hapo akaona hapamfai bora aiponye nafsi yake, alianza kutimua mbio kufuata barabara ya kuelekea Mbeya lakini hakufanikiwa, alipoambiwa asimame aligeuka na kumfyatulia risasi polisi yule ambaye alibwagwa chini na kupoteza uhai, kabla Machura hajajiweka tayari alijikuta akichakazwa na risasi zilizotoka katika SMG ya polisi mwingine aliyebaki juu ya defender na kumlaza juu ya daraja hilo akiwa hana uhai.

“Mwanaharamu we! Nani aliyekwambia unaweza kuukimbia mkono wa dola?” ilikuwa ni sauti ya RPC alipokuwa akiuangalia mwili wa Machura ukiwa kwenye machela tayari kuhifadhiwa kwenye chumba cha maiti cha hospitali ya mkoa wa Iringa.

# 10

## Baada ya mwezi mmoja
## Lugalo hopspitali

ISABEL alikuwa akifanya mazoezi ya kutembea katika korido za hospitali ya jeshi ya Lugalo, huku akifuatiwa kwa ukaribu na daktari wa mifupa wa hospitali hiyo Meja Kihanga.

“Naona sasa unapata nafuu sana Isabel” alimwambia Isabel ambaye alikuwa mbele yake akitumia fimbo maalum za kutembelea.

“Ee dokta, leo si kama siku zilizopita, hata naweza kukunja mguu”

“Usijali utatembea tena”

Isabel aliendelea kufanya mazoezi, leo hii alifanya mazoezi kwa bidii sana, moyoni akiwa na furaha ya ajabu, hakujua furaha ile ilitokea wapi, alifarijika kuowaona ndugu na rafiki zake waliokuja kumsalimu mara kwa mara. Alipoona inatosha alirudi wodini kupumzika.

## Baada ya masaa machache

“Isabel, kuna wageni wanataka kukuona” muuguzi aliyevalia sare nadhifu za kazi alimpa ujumbe huo Isabel.

“Waambie waje”

“Wewe ndiye unayetakiwa kwenda kuwaona walipo”

Isabel alisita na kukaa kimya kwa muda, alionekana wazi kuwa woga umemuingia ghafla.

“Usiogope Isabel, hapa ni sehemu salama sana, jiandae nikupeleke” yule muuguzi alimuambia Isabel. Isabel alijiandaa na kisha alijinyanyua tayari kwa kwenda kuonana na wageni hao. Yule muuguzi alipotaka kumpa kiti cha magurudumu, Isabel alikataa na kutaka kutembea mwenyewe. Kwa mwendo wa taratibu akisindikizwa na yule muuguzi Isabel alijikongoja mpaka chumba kidogo kilichokuwa na viti sita vilivyoizunguka meza kubwa ya chakula, aliketi kwenye moja ya viti hivyo lakini mpaka muda huo alikuwa ni yeye na yule muuguzi tu.

Mara mlango mwingine ukafunguliwa watu watatu wakaingia ndani ya chumba hicho aliyetangulia alikuwa na sare za kijeshi zilizochafuka kwa vyeo vingi vingi, ilionesha wazi kuwa alikuwa mtu wa cheo cha juu sana jeshini, nyuma yake kulifuatiwa na mwanamke wa makamo alivalia nadhifu suti ya rangi ya jani la mgomba na nywele zake zilikuwa ni mchanganyiko nyeusi na nyeupe, mtu ambaye Isabel

angestahili kumwita mama au hata bibi kabisa, mwisho kabisa alimalizia kijana mtanashati, akiwa ndani ya suti ya khaki ya mtindo wa *codroy*, fasheni ya vijana. Isabel alitua jicho lake kwa kijana huyu ambaye alimtambua mara moja bila kificho, Kamanda Amata.
Wote walichukua nafasi zao na kuketi.

"Isabel !" yule mwenye manyota alimuita na kumgutusha kutoka katika lindi la mawazo, "Samahani kwa kukusumbua, tumekuja mara moja kukusalimu, mbele yako mimi naitwa Meja Jenerali Chipatikila, kutoka hapa hapa Lugalo, huyu unayemuona hapa anaitwa Madam S pamoja na kijana Amata nadhani unamfahamufahamu" yule Meja alimaliza kutambulisha upande mmoja wa meza ile. Wote walimwangalia Isabel ambaye tabasamu lake halikujificha usoni mwake.

"Mimi ninaitwa Isabel kutoka Kigoma" Isabel alijitambulisha kwa kifupi tu.

"Isabel, kwanza pole sana kwa misukosuko yote uliyoipata katika sakata hili ambalo ulijikuta ndani yake" Madam S aliongea kwa pozi kama kawaida yake "Mimi na ofisi yangu tutanatoa shukrani sana kwa msaada wako katika hili, hatuna muda wa kuzungumza mengi ila hapa kuna ujumbe tuliokuletea, ujumbe muhimu sana, usome mwenyewe tafadhali". Kamanda Amata alimpatia Isabel bahasha maalum nyeupe.

Isabel aliipokea na hakujua nini kilichopo ndani yake, kilichomshtua ni nembo kubwa iliyoonekana

hapo juu iliyopambwa kwa rangi nzuri, yenye picha ya bibi na bwana walioshika pembe za ndovu, ngao ya Taifa, aliigeuzageuza. Kisha kwa mikono ya kutetemeka aliifungua kwa makini na kutoa karatasi iliyokuwa ndani yake, karatasi kubwa kidogo iliyoandikwa kwa mashine maalumu.

> *'…Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeuthamini mchango wako wa uzalendo, wa kuwa tayari kuutoa uhai wako kwa ajili ya Taifa lako (…). Kutokana na hayo yote mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anakupa mualiko maalum siku ya tarehe 25 Julai, katika viwanja vya Ikulu saa kumi jioni katika hafla fupi ya kutunuku nishani mbalimbali kwa wananchi waliofanya makubwa katika kupigania taifa lao, na wewe ukiwa mmoja wao…'*

Iliandika sehemu ya barua hiyo na mwisho kumaliziwa na saini ya Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Isabel alishusha pumzi, kijasho chembamba kilimtoka mwilini, alihisi tumbo lake kama linalegea, hofu kuu iliujaza moyo wake. Maishani mwake hakuwah kufikiri hata siku moja kama atakuja hata kuliona tu jingo la Ikulu ya nchi, hakuwahi kufikiria hata kama atakuja kumuona Rais wan chi sembuse kumshika mkono! Aliirudisha bahashani barua ile na kumkabidhi Madam S.

"Samahani mama, utanikabidhi siku nikiondoka" alimwambia madam S.

♠ ♠ ♠

## Siku ya Mashujaa
## Viwanja vya Ikulu – Dar es salaam

**M**uziki laini wa tarumbeta ulikuwa ukisikika kutoka katika *brass band* ya jeshi la Magereza kutoka Ukonga, waliopendezeshwa kwa sare zao nadhifu zenye rangi ya kijani na fito za njano, wote wakiwa wamevalia *gloves* nyeupe mikononi mwao na kuketi katika mtindo wa kupendeza, kila mmoja akikitumia chombo chake kwa ustadi huku macho yakisoma michoro fulani katika karatasi zilizo mbele ya kila mmoja, wimbo unaoitwa *Mashujaa* uliotungwa na hayati Marijani Rajabu ulikuwa ukipigwa na kikundi hicho kwa ufundi wa hali ya juu.

Wageni mbalimbali walikuwa wakiingia katika viwanja hivyo kadiri ya mialiko waliyopelekewa, mabalozi na wawakilishi wa taasisi mbalimbali walimiminika katika viwanja hivyo, alkadhalika milio hadimu ya ndege wa kupendeza aina ya Tausi ilikuwa ikiongeza utamu wa shughuli hiyo.

Punde kidogo iliwasili BMW nyeusi iliyong'azwa kwa rangi safi, metallic, ikiwa inatembea taratibu kuelekea viwanja hivyo nyuma ilikuwa inafuatiwa na gari moja ya polisi na gari kadhaa binafsi ambazo zote

zilikuwa zimewasha taa za vimulimuli vya kibuluu kwenye show za mbele za gari hizo. Ile BMW ilisimama katika zuria jekundu mlango ukafunguliwa, kila mtu alisimama akijuwa kuwa sasa mheshimiwa anaingia, walisahau kama mheshimiwa wanayemtarajia yumo ndani hapo.

Msichana mfupi, mnene mwenye macho ya duara na mashavu yenye kubonyea atabasamupo aliteremka kwenye gari hiyo, akiwa anasaidiwa kwa kutembea kwa fimbo maalum ya kutembelea aliweza kuvuta hatua fupifupi juu ya zuria hilo huku nyuma akifuatiwa na kijana mmoja nadhifu aliyetulia kwenye suti kali nyeusi na mwanamama wa makamo ambaye alionekana kuwa bado kijana kimawazo.

Walimsindikiza kwa mwendo wa taratibu kwa sababu ya ile fimbo yake, huku umati wa watu ukimpigia makofi binti huyu, aliketi kwenye kiti cha mbele kabisa na nyuma yake kulikuwa na hao wapambe wake, muziki uliendelea, waandishi wa habari, wapiga picha za mnato na mjongeo walikuwa bize kuchukua picha ya kupamba magazeti yao ya siku inayofuata, picha bora ya Isabel aliyekuwa ameketi hapo ambaye tangu mwanzo walishindwa kuipata picha hiyo.

Mara muziki ulinyamaza na watu wote wakasimama, kutoka mlango mkubwa wa Ikulu, mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alionekana wazi, mwenye tabasamu la bashasha kama kawaida wake, alisalimiana na watu

waliokuwa mbele kabisa ambao ni vigogo wa serikali, kisha kabla ya kusema lolote aliteremka ngazi na kwenda kumpa mkono Isabel, alimuuliza mawili matatu ikiwa na kumjulia hali, kisha akarudi sehemu maalum aliyoandaliwa kwa ajili ya kutoa hotuba yake.

> *'(…) leo hii taifa letu lingekuwa kwenye hali mbaya ya mauaji, damu isiyo na hatia ingezijaza barabara zetu na majumba yetu. Ni hali inayoudhi lakini wengine huifurahia. Si kila mtu ni adui wa taifa lake, wapo wenye mapenzi na uzalendo wa kweli, wapo tayari kupigania hata kufa kwa ajili taifa lao, hao ndiyo tunaowataka katika Afrika na dunia yote*.(makofi ya nguvu*). Wote mtakuwa mashahidi, mmesikia juu ya mapinduzi yaliyopangwa kufanyika, lakini vyombo vyetu imara vya ulinzi vimeweza kuidhibiti hali hiyo, ninavishukuru sana kwa niaba ya Watanzania wote.*
>
> *Lakini kila jambo lina mwanzo, safari hii msichana mdogo, msichana mbichi kaonesha uzalendo wa hali ya juu wa kulipigania taifa lake, aliona ni bora afe yeye lakini mamilioni ya Watanzania waokoke na janga hilo. Tunahitaji watu kama hao, huyu ni mfano kwetu sote Watanzania.'*

Ilikuwa sehemu ya hotuba ya Rais iliyopigiwa makofi na vigelele na wote waliopo katika hafla hiyo.

*‘(…) tumekusanyika hapa si kama mlivyozoea, leo ni siku ya pekee, tunaposherehekea mashujaa wa taifa letu, tunatoa nishani moja tu ya uzalendo kwa msichana huyu shujaa, na jina lake litaandikwa katika kitabu cha mashujaa, na kumbukumbu yake itaingia katika makumbusho na historia adhimu ya taifa letu tukufu la Tanzania.*

*Kwa niaba ya Watanzania napenda kutoa shukrani za dhati kwa dada Isabel na kuwataka vijana wote kuwa na moyo huohuo na si kushabikia tu siasa.*

*Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika, Mungu mbariki Isabel.’*

Vifijo na nderemo viliisindikiza hotuba hiyo tamu. Baada ya mshereheshaji kuongea kidogo, Isabel alinyanyuka kitini na kusindikizwa kuelekea eneo maalum lililotengwa kwa tukio hilo, vimulimuli vya picha vilimulika kila upande.

Isabel alisimama mbele ya Rais, WP aliyeandaliwa alisogea kwa ukakamavu na kupiga mguu mmoja chini kisha akanyanyua kisahani kidogo, mheshimiwa Rais alichukua kitu Fulani chenye rangi ya dhahabu na kukipachika upande wa kushoto wa kifua, katika suti ya Isabel, kisha akachukua kitu mfano wa cheti kilicho ndani ya fremu maalum na kumkabidhi Isabel, kishapo akampa mkono na kusimama naye sambamba wakitazama kule kwenye nembo kubwa ya Taifa,

pembeni yao kukiwa na bendera ya taifa upande mmoja nay a Rais upande mwingine, wiimbo wa Taifa ukasikika ukipigwa kwa madaha kabisa huku bendera zile zikipepea kwa upepo mwanana wa baharini, Isabel aliangusha machozi hakuweza kuyafuta kwa sababu hutakiwi kujitikisa wimbo huu muhimu ukipigwa, baada ya hapo walitulia kwa picha. Baada ya wapiga picha kupata picha za kutosha, Isabel, kamanda Amata na madm S walifuatana na Rais ndani ya ukumbi wa Ikulu dhifa maalum pamoja na wageni waliofika.

Baada ya tukio hilo ikiwa kama shukrani, serikali ilijitolea kumlipia masomo Isabel ndani na nje ya nchi, kuwajengea makazi bora na ya kisasa yeye na wazazi wake huko Kasulu, Kigoma. Na alipopona kabisa alirudi chuoni kuendelea na masomo yake na heshima aliyopewa na taifa iliendelea kubaki naye daima, tangu kwa wazee hata watoto.

## HATIMA

Baada ya yote hayo, sheria ya Tanzania iliwahukumu kifungo cha maisha na kazi ngumu madam Rose, Frank na Jomse katika magereza tofauti tofauti ndani ya Tanzania baada ya makubaliano kati ya serikali hizi tatu.

Mwili wa Machura ulizikwa kwao Kigoma bila heshima yoyote ya kiserikali, mwili wa Tonton

ulisafirishwa na ndugu zake kurudi kwao Burundi kwa taribu za maazishi.

♠ ♠ ♠

“Asante sana kamanda Amata” Isabel alimshukuru Amata na kumpa mkono

“Nikushukuru wewe kwa kutuokoa katika hili, kutuokoa dhidi ya Mpango Hasi” Amata aliirudisha shukrani ile.

Wote wawili walinyanyua bilauri zao zilizojaa mnvinyo aina ya St Anne na kugonga cheers huku madam S akiwapiga picha ya kumbukumbu.

**≈ MWISHO ≈**